# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report Of

## DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL – BURA CONSTITUENCY, HELD AT BURA TANA

## ON

**17TH OCTOBER, 2002**

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL – BURA CONSTITUENCY HELD AT BURA TANA.**

**Present:**

1. Com. Ibrahim Lethome - in chair

**Secretariet in Attendance:**

1. Hassan S. Mohammed - Programme Officer
2. Halima Amran Adam - Verbatim Recorder

The meeting started at 10:25 AM with Commissioner Lethome in chair.

**Mohammed Wario**: Tafadhali mkae ili tuanze programme yetu. Kabla hatujaanza chochote nafikiri tutapata kwanza Sheikh mmoja atuombee. Councillor Hirmani tafadhali simama utuombee ili tufungue mkutano wetu.

**Cllr. Hirmani:** *Bismillahi Rahmani Rahim, haya tuombe. Allahuma adinal hakka hakka warzuknal tibaa, waadinal batila batila warzuknal tinaba, wasalla llahu ala sayidna Muhammad. AMIN.*

**Mohammed Wario:** Okay, nafikiri sasa tutaanza. Tunashukuru sana wageni wetu wamefika kwa wakati unaotakikana kwa hivyo kabla sijarudisha usukani kwao ningependa kujulisha wana kamati wa sehemu ya wakilishi Bungeni ambao wanawakilisha sehemu hii ya Bura Constituency. Nikianza na mimi mwenyewe ambaye ni mwenyekiti wao, nafikiri wengi mnanijuwa Mohammed Wario, niko na Hassan Bagana Kurawa hapa ambaye anatoka sehemu ya Madogo. Niko na Ibrahim Arrale Adan kutoka Bangale, tuko na Osman Bonaya Habatano, niko na Hawa Adan alikuwa hapa sijui ametoka nje, nafikiri anatayarisha mambo na Elizabeth Wanjiku, ndiyo ambao wamefika hapa.

Mwanakamati mmoja ni Mheshimiwa Galgalo hayuko, tuko na Salat Garacha amabaye ni mwenyekiti wa Tana River County Council, naye hayuko hapa. Kwa hivyo, Co-ordinator wetu pia ametuma salamu angependa kuwa hapa lakini kuna Commissioner Prof. Idha Salim ambaye ako Galole na hapo ndiyo headquater ya District kwa hivyo, imebidi yeye awe huko na mimi ndiye nitamuakilisha pengine atatupata tukiwa tunaendelea na programme.

Kwa hivyo, bila kupoteza wakati, nita-hand over kwa mgeni wetu ambaye ni Commissioner Ibrahim Lethome ili atujulishe walio

andamana nao na aendelee na programme yetu asante, karibu Ibrahim Lethome Commissioner.

**Com. Lethome**: Asante sana Bwana Wario. *Bismillahi Alhamdullillah, Assallatu wasalamu ala sayidina Muhammed wa ala alihi was'habihi ajmain ama baath. Assalaam Aleikum Wa-Rrahmatu Llahi Wa Barakatuh.* Tunamshukuru Mwenyezi Mungu (S.W.T.) kwa kutupa hii fursa na kutuwezesha kufika hapa, tunaomba msamaha kwa kuchelewa lakini ni kwa sababu ya shughuli zingine, sisi tumewasili jana kutoka Mandera.

Ningependa kuwajulisha wale walioandamana na mimi, kutoka katika makao makuu ya Tume ya Marekebisho ya Katiba. Anayesimama hapa anaitwa Hassan Sheikh, yeye ni Programme Officer kutoka katika makao yetu makuu Nairobi, tuna dada yetu kule nyuma Halima Amran Adam ambaye ni verbatim recorder, yeye kazi yake ni kusajili yale yote ambayo tutazungumza leo kutumia mashini na kama mlivyoambiwa mimi ni ndungu wenu Commissioner Ibrahim Lethome.

Nafikiri tayari mshajulishwa sababu ya sisi kuja hapa leo hii, kama tulivyofanya katika sehemu zingine. Tulianzia Dadaab tukaenda juu hadi Mandera na leo tuko hapa. Mmeshiriki katika shughuli hii ya marekebisho ya Katiba tangu ilipoanza na tulianza kwanza kwa kuelemisha watu juu ya haki zao za kiraia, civic education. Nafikiri mlipata kutembelewa na watu wa kuwajulisha Katiba ni kitu gani? Na wewe kama mwananchi wa Kenya una haki gani na una wajibu gani? Serikali ina wajibu gani juu ya mwananchi? Baada ya hapo tukazunguka tena kuchukuwa maoni ya wananchi, na ninafikiri mliwahi kutoa maoni yenu. Mlitoa maoni ama hamkutoa ninyi? Mlitoa maoni?
**Audience:** Tulitoa.

**Com. Lethome:** Mlitoa maoni yenu. Baada ya kukusanya maoni yenu sisi kama Tume ya Marekebisho tulikaa chini na kuweza kuandika mswada au *mswadda* kwa lugha ya kiarabu au bill au mapendekezo kwa lugha nyingine ambayo tungependa yawekwe katika Katiba mpya. Sababu ya kurudi kwenu tena ni kuwa kulingana na sheria iliyobune Tume ya Marekebisho ya Katiba, haya maoni ambayo tumeweka katika mapendekezo ya katiba mpya, sio maoni yetu kama tume sisi watu ishirini na tisa ni maoni yenu nyinyi kama wananchi na ndiyo sababu, sheria imetulazimu turudi kwenu kabla ya maoni haya hayajapelekwa katika kongamano la kitaifa au mkutano wa kitaifa ambao unaitwa National Constitutional Conference, ambao pengine Mungu akipenda utaanza tarehe ishirini na nane mwezi huu na baada ya hapo, yapelekwe Bunge na tuweze kupata Katiba mpya.

Sheria imesema lazima mrudi kwa wananchi wenyewe, wenye maoni mjadiliane na wao muwajulishe ni mapendekezo gani ambayo mmeweka katika Katiba mpya. Na ndiyo haya niliyokuja nayo, hii file ambayo nimebeba hapo ukiangalia imeandikwa Draft, draft yaani ni mapendekezo sio sheria na ndiyo kuna kijitabu au makaratasi ya gazetti ambayo Programme Officer amewapa baadhi yenu, hatuna ya kutosha ya kuonyesha hiyo draft. Na draft yenyewe ni kulingana na maoni ya wananchi na ninafikiri kuna file ndani ya gari, programme officer ataitoa atawaachia, inaonyesha mapendekezo ya watu wasehemu hii ya wakilishi bungine.

Kwa hivyo, kwa ufupi haya yote tuliyokuja nayo hapa kuna section karibu mia tatu, hizi ukurasa zote ambazo unaona hapa ni maoni ya wananchi Kenya nzima, yakiwemo maoni yenu nyinyi watu wa hapa Bura Tana, kwanza sijui Kiswahili changu kinafahamika ama hakifahamiki?

**Audience**: Kinafahamika

**Com. Lethome:** Unajuwa changu ni cha ki-Masaai Bwana, sasa chenu najuwa ni cha Pwani pengine changu na chenu kidogo kinagongana. Kama lugha haifahamiki mniambie haifahamiki, mnaifahamu vizuri eh?

**Audience**: Sana.

**Com. Lethome:** Haya, kabla sijaingia kuangalia ni yapi tuliyopendekeza katika Katiba mpya, ningependa tu kuwagusia baadhi ya mambo ambayo ilikuwa ni muhimu, usifukuze watoto tafadhali sikija ndungu yangu, hii Katiba ni ya watoto pia, asifukuzwe mtu yeyeote. Hii katiba ni ya kila Mkenya akiwa mdogo au mkubwa, watoto pia wana haki ya kusikiza mambo ya katiba, wasifukuzwe, hii ni yao sisi tunaondoka bwana na wao ndiyo itawatawala hii miaka mingi, sisi twaenda.

Kuna baadhi ya mambo ambayo ilikuwa ni lazima tuyazingatie au tuyatilie muhimu wakati wa kukusanya maoni ya watu na kutayarisha mapendekezo ya Katiba mpya. Baadhi ya mambo haya ambayo ilikuwa ni muhumu sana ni umoja wa nchi hii, ilikuwa ni lazima tunapofanya kazi hii ya kukusanya maoni na kuandika mapendekezo ya katiba mpya, tuzingatie au tutilie umuhimu umoja wa nchi hii kama Kenya. Sio kuwa tufanye kazi mwisho wake, wakenya wawe ni makundi makundi, North Eastern peke yao, Coast peke yao, wa Pokomo peke yao, wasomali peke yao, la. Tunataka tukimaliza hii shughuli, wakenya wawe na umoja zaidi, hilo ndiyo moja katika mambo ambayo ni lazima tuyazingatie.

Ya pili, kuwashirikisha watu wote, na ndiyo sababu kila mahali tunapokwenda tunampa nafasi tajiri, masikini, mdogo, mkubwa, mzee, kijana hata na wasiojiweza. Wale ambao tunawaita pengine vilema, pia tumewapa nafasi na ndiyo sababu, utaona hata katika mapendekezo yetu, tumefikiria wale ambao ni wakenya lakini hawawezi kusoma kwa sababu pengine hawaoni, vipofu. Tumetayarisha pia kwa lugha inayoitwa Braille kwa hivyo, tunasema Bwana Chairman wa 3C's kama kuna mtu yeyote ambaye anaweza kusoma Braille, tumekuja na nakala moja ya sehemu inayohusiana na haki za binadamu ambayo imeandikwa kwa lugha ya Braille, lugha ambayo husomwa kwa kupapaswa.

Hii ni kuonyesha kuwa sisi tumezingatia ama tumetilia umuhimu kumshirikisha kila Mkenya katika shughuli hii na ndiyo sababu kila tunapokwenda tunataka wakina mama waweko, wazee waweko, vijana waweko, kila mtu tajiri na masikini kwa sababu, hii shughuli ni ya wakenya wote. Tunataka tuwe na Katiba ambayo ni kinyume na Katiba inayotutawala hivi sasa ambayo haikushirikisha maoni ya wakenya, bali ni Katiba iliyotengenezewa nje ya nchi hii, mahali panapoitwa Lancaster tukaletewa ndiyo imetutawala miaka thelathini na tisa na hivi sasa tunataka kutawaliwa na Katiba ambayo imebuniwa juu ya misingi ya wananchi wenyewe.

Jambo lingine ambalo ilikuwa ni lazima kulizingatia katika shuguli hii ni kuwa, lazima kuwe na amani katika nchi. Kwa hivyo, katika kazi zeto tumejaribu kadiri ya uwezo wetu kusiwe na vurugu au kuchochea upande wowote. Na ndiyo sababu tulikuwa tukienda katika vikao tunawaambia watu, mna uhuru ya kusema mtakayo, ama hamkuambiwa hivyo walipokuja hapa Commissioners? Mna uhuru wa kusema mnalolitaka kama ni kuhusu ofisi ya Rais, ofisi wa Mkuu wa Mkoa, ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ofisi ya Mkuu wa Tarafa, una haki ya kusema unavyotaka bora tu usitukane wala kuchochea, wala usituletea siasa za chama chako cha kisiasa. Lakini una haki ya kusema utakalo, kwa sababu tulikuwa tunajiepusha na vurugu, hatutaki vurugu tunataka nchi iwe na amani.

Kama nilivyowaambia haya mapendekezo yote yako hapa, yamebuniwa ama yametolewa katika maoni ya wananchi. Tumezunguka kila sehemu ya uakilishaji Bungeni Kenya nzima tukakusanya maoni ya watu na mtu mwenye shaka yeyote ana haki ya kuja katika makao yetu makuu na kuangalia wananchi wamesema kitu gani.

Katika pia kupendekeza Katiba mpya, tumezungiatia jambo ambalo kila tunapokwenda tunasikia wananchi wanalalamika kutokuwa na usawa. Leo hii nafikiri kila mmoja anajuwa ukiwa maskini na kuna mwenzako ambaye ni tajiri na iwe pengine mnakesi na yeye kortini, mara nyingi ni nani ambaye atapata haki atashinda ile kezi?

**Audience:** Tajiri.

**Com. Lethome:** Tajiri, utakuta hakuna usawa. Mara nyingi utakuta maskini ndiye anayedhulumiwa, sheria inamuangalia tu maskini, tajiri anapita tu, tajiri akipita na gari lake maadamu ni gari kubwa kama hili nililokuja nalo la serikali, hata kama ana vitu vya kuibiwa ndani, atasimamishwa na polisi?

**Audience**: La.

**Com. Lethome**: Atapigiwa saluti apite, maskini na mkokoteni wake wa punda akipita hapa, anabeba chakula cha watoto wake ndiyo anayedhulumiwa. Tajiri atakuwambia nipeleke unakotaka ama sivyo? Si hiyo lugha wanayotumia?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome**: Nipeleke unakotaka, utanipeleka wapi wewe ama sivyo?

**Audience:** Ndivyo.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo tumezingatia sana mambo ya usawa katika mapendekezo yetu tumejaribu kuhakikisha kuwa, hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria, maskini, tajiri, kiwete, mtoto mdogo, mtu mzee, wote ni sawa mbele ya sheria. Na pia uadilifu, na utakuta pia katika wale wanaonyanyaswa sana ni kina mama, kina mama utakuta wanadhulumiwa sana, sehemu nyingi tumekwenda unasikia watu wanasimama, tunawauliza mna maoni gani kuhusu Katiba mpya? Sehemu zingine wanasema, tunataka sheria ambayo haitamruhusu mwanamke kuridhi mali, babake akifa mwanamke asiridhi. Hata mashamba? Eh hata mashamba wasiridhi, apate wapi mwanamke? Aridhi kwa mumewe, na asipoolewa? Basi apelekwe kwenye mbunga za

kuhifadhi wanayama akakae huko. Angalia, mwanamke amedhulumiwa sana kwa hivyo, tumeangalia pia haki za mwanamke kwa sababu mtoto wa kike amedhulumiwa, mwanamke amedhulumiwa kwa hivyo, tungependa sheria ambayo itamuinuwa mwanamke na kumtoa katika dhulma anayofanyiwa. Sijui kama nyinyi watu wa Bura pia mnawadhulumu wakina mama?

Swali moja, kwa mfano mzee akiwa na watoto wawili mmoja wa kiume na mwingine wa kike na awe hana uwezo wa kuwasomesha wote wawili, ana uwezo wa kumsomesha mmoja atamsomesha yupi?

**Audience:** Kijana.

**Com. Lethome:** Mvulana si ndiyo. Kwa nini atachaguwa kumsomesha mvulana? Anakuambia kwa sababu huyu ndiye atakayenirithi, huyu ndiye atakaye ni saidia nikiwa mzee. Mtoto wa kike hawezi kukusaidia ukishakuwa mzee? Wewe ndiyo Mwenyezi Mungu unayejuwa ni yupe atakaye kufaa? Humjui atakaye kufaa Mwenyezi Mungu ndiye anayejuwa atakaye kufaa. Kwa hivyo, tumeangalia sana mambo ya mwanamke kunyanyaswa.

Haki za binadamu, kuna haki ambazo hakuna mtu amekupa. Kuna mtu aliyekufa wewe kuwa binadamu Sheikh? Kuna mtu ambaye alikupatia ruhusa ya kuwa binadamu ama kibali cha kuwa binadamu au haufahamu Kiswahili? Kuna mtu?

**Sheikh:** Hakuna

**Com. Lethome**: Hakuna, hata serikali haikukupa utu wako, umepewa na Mwenyezi Mungu. Na kuna haki ambazo Mwenyezi Mungu amekupa hakuna binadamu anaweza kuzichukuwa hata serikali. Kwa hivyo, utakuta tumezingatia sana, tumetilia umuhimu haki za binadamu kwa sababu tumeona miaka thelathini na tisa, kuna watu ambao wamenyanyaswa kufikia kiwango cha kuwa hata haki zao za utu, kuwa mtu ni banadamu ana haki fulani, hizo haki haziangaliwi. Na tumeangalia haki hizo hata mtu akiwa jela, ina maana mtu akishashikwa akiwekwa kwenye cell ya polisi, si binadamu tena amekuwa ni mnyama ama ni binadamu bado? Mtu akishashikwa na polisi ni binadamu ama si binadambu?

**Audience:** Ni binadamu.

**Com. Lethome:** Utakuta wakati mwingine mtu anawekwa katika mazingara ambayo hata mbuzi wako huwezi kumweka, ama sivyo? Amenyimwa haki zake za binadamu, ana zinanyanyaswa. Mtu akiwa masikini inakuwa hana haki, kwa hivyo, tumezingatia sana na utaona katika mapendekezo yetu sehemu kubwa sana imezungumzia juu ya haki za binadamu kwa Kiingereza zinaitwa Human Rights, fundamental rights, haki za kimsingi ambazo ni lazima kila serikali iweze kuziangalia ni kama hizi. Utakuta sehemu zingine za North Eastern na pengine sehemu kama hii ya Pwani, binadamu wanaishi mahali ambapo wakitaka maji, akihitaji maji ya kunywa, inabidi atembee masafa marefu sana ya kutafuta maji. Ni haki ya binadamu, mtu akiwa binadamu lazima atakunywa maji na mifugo yake inahitaji maji, ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa binadamu kama huyo ana maji.

Yasikitisha, tumekwenda sehemu zingine unakuta nyani na binadamu wanapigania kisima cha maji. Mahali panaitwa Takaba

ilitokea kisa kama hicho, mwaka wa sitini na sita, binadamu na nyani ilikuwa wanapigania shimo la maji. Ama unakuta mahali barabarani maji kama haya yaliyo mwagika ya mvua machafu, nguruwe anaoga ndani, binadamu anakuja kumfukuza nguruwe aweze kuyateka yale maji. Amenyimwa haki yake ya binadamu, ni binadamu na kuna haki za kimsingi lazima apewe, kwa hviyo, tumezingatia.

Jambo lingine ambalo tumelizingatia katika kazi yetu ni kuhusu amani na usalama. Hivi tumekaa hapa kama kungekuwa hakuna usalama tungeketi hapa kusikiza mambo haya? Ingekuwa saa hizi kila mmoja roho mkononi, mara risasi zinafyetuka huko, hatuna usalama. Maendeleo yanaweza kupatikana bila usalama? Ndiyo tumezingatia hapa tukasema ili wananchi waweze kujishughulisha na mambo ya maendeleo, lazima kupatikane usalama na ndiyo tumezingatia sana katika mapendekezo yetu mambo ya usalama ya mwananchi na mali yake.

Mambo mengine ambayo tumezingatia sana katika Katiba ni kuhusu kuhifadhi katiba yenyewe. Kwa sababu, huenda tukaandika katiba nzuri sana kwa wino wa dhahabu, lakini isipofuatwa hiyo katiba ina faida yeyote? Ina faida yeyote?
**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Itakuwa haina faida yeyote au ikiwa inafuatwa na masikini tu na tajiri hafuati, ina faida yeyote? Au mkubwa hafuati sheria, anayetakuwa kufuata sheria ni mbodo, itakuwa na faida yeyote? Kwa hivyo, tumezingatia hapa tumeweka baadhi ya sehemu ambazo zinalazimisha watu wote wafuate sheria, mkubwa na mdogo, kiongozi na mwenye kuongozwa. Wote wafuate sheria mpaka Rias wa nchi afuate sheria kwa sababu, isipofuatwa sheria inakuwa haina faidia yeyote, hata wale ambao mnasoma Qur'ani, Mwenyezi Mungu (S.W.T.) amekupa Qur'an mwongozo katika maisha yako yote, je usipoifuata itakusaidia?
**Audience**: La.

**Com. Lethome**: Itakuwa haikusaidii, ikiwa Qur'an yako ni ukiisoma ijumaa unaifunga na kitambaa unaiweka juu kule, unakwenda kufanya kinyume nayo, itakuwa haina faida yeyote na wewe. Hivo hivo katiba isipofuatwa, itakuwa haina faida yeyote, kwa hivyo, tumezingatia maswala ya katiba kufatwa, tumeweka baadhi ya vikwazo ambavyo vinahakikisha kuwa kila mmoja anafuata sheria. Yale mambo ya kusema kuwa, mimi ni mkubwa sifuati sheria tumeondoa katika katiba mpya.

La mwisho kabisa ni kuwa, katiba hii au mapendekezo haya ya katiba mpya yametokana na maoni ya wananchi na ili katiba hii iweze kufaulu na kutekelezwa, tunawarudishia wananchi wenyewe. Kwa hivyo, kila mmoja wetu lazima abadilishe msimamo wake kuhusu mambo ya sheria ili iweze kufanya kazi. Lugha tunayotumia mara nyingine ama msimamo wetu kuhusu mambo ya sheria, ndiyo mara nyingine huleta matatizo katika nchi. Kwa mfano, kuna ufisadi katika nchi ya Kenya ama hakuna, ufisadi corruption? Mambo ya kitu kidogo si iko?
**Audience**: Ndiyo.

**Com. Lethome:** Kuna sheria ambayo inaruhusu mambo ya kitu kidogo?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Lakini imekuwa ni tabia zetu, mwenendu wetu na tumechukulia kama ni jambo la kawaida sisi. Tunasema maadamu mkubwa anakula kitu kidogo na mimi pia wacha nile kitu kidogo ama sivyo?

**Audience:** Ndivyo.

**Com. Lethome:** Na ndiyo leo hii mzee tukikuchaguwa wewe, uende Bunge halafu uchaguliwe kuwa waziri, kama ulikuwa ukitembea na baisikeli ukiendelea kutembea na baisikeli tutasema mjinga huyu, tumempeleka huko kula ameshindwa kula ama sivyo tunavyosema? Ama sio lugha tunayotumia?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo, sisi wenyewe ndiyo huwa tunavunja sheria kwa sababu ya msimamo wetu, au unasema ikiwa mkubwa anavunja sheria hata na mimi nitavunja sheria. Kwa hivyo, la mwisho ni kusema kuwa wananchi wenyewe ndiyo watakaoipa nguvu hii sheria au kuivunja sheria.

Sasa baada ya kuzungumzia kwa ufupi sana kuhusu baadhi ya mambo ambayo tumeiangalia katika kupendekeza mambo ya katiba mpya. Tulianza kwa kuandika katika mapendekezo yetu, jambo ambao hakuna katika hii sheria, hii ndiyo sheria inayotutawala, ndiyo katiba yetu tangu mwaka wa sitini na tatu. Haina kitu ambacho kinaitwa utangulizi, na utangulizi ni muhimu, hata katika maisha yetu ya kila siku huwezi kukutana tu na Haji njiani halafu kabla hata hujamuamkua, hujamuambia wewe ni nani mara ushamuambia bwana lete zile pesa zangu. Atakupa hizo pesa kweli? Hawezi mpaka kawaida ni, ama mila zenu sijui hapa Bura lakini kule ninakotoka na kule ninakojuwa watu huamkuwana kwanza, kisha wakaulizana hali hata mkaingia katika mambo ya mvua, kunanyesha siku hizi ama hakunyeshi halafu ndiyo unamuambie, sasa mimi ni fulani nimetoka mahali fulani na nimekuja kwa jambo kadha, nataka hili ama sivyo?

**Audience**: Ndivyo?

**Com. Lethome:** Huo unaitwa utangulizi, kila jambo huwa lazima liwe na utangulizi. Hata sisi tulipokuja tunajuwa tumekuja mkutano wa katiba, lakini hatukuja tu, tumeanza kuamkuwa watu pale tunakwenda mahali fulani sisi ni kina fulani, ndiyo muweze kutupokea. Kama tungekuja tu na kuvamia na kukaa hapa, mngekubali kutusikiza kweli? Sasa tumeangalia katiba yetu ya zamani tukaona kuwa haina kitu kinachoitwa utangulizi.

Imeanza tu kwa kusema kuwa Kenya ni Jamhuri, Jamhuri hii hatujui ina binadamu ndani yake na kama ni binadamu ni binadamu wa aina gani ama ina wanyama ndani yake. Inafuata philosophia gani inatoka wapi, inaelekea wapi? Hakuna, ukiangalia katiba za nchi zote ulimwenguni zina utangulizi yetu tu haina utangulizi na ndiyo tukasema katika katiba mpya ikiwezekana, lazima kuwe na utangulizi ndiyo sababu tukaweka utangulizi ambayo kwa lugha ya ki-sheria inaitwa, Preamble. Preamble ni utangulizi na

mambo yale ambayo tuliweka katika utangulizi wetu ni yafuatayo, swali je katika nchi hii ya Kenya tuna kabila moja? Kenya ni nchi ya kabila moja?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Wazee nataka mshirikiane na mimi ndiyo tuendelee vizuri, sio nchi ya kabila moja. Ndani yake kuna Mpokomo, kuna Wardei, kuna nani wengine? Kuna Maasai kama mimi, kuna Msomali, kuna Kalenjin, kuna Mkikuyu. Hawa wote ni wakenya ama si wakenya?

**Audience:** Ni wakenya.

**Com. Lethome:** Ni wakenya, Mwenyezi Mungu mwenyewe alitaka hawa wote makabila tofauti tofauti na wawe katika nchi ya Kenya. Haya dini, Kenya sisi watu wote tunafuata dini moja?

**Audience:** La.

**Com. Lethome**: La, hapa nimesikia mmoja aki-test mic amesema haleluyah, Mkristo huyo. Kuna mwingine hapa amesema *Assallam Aleikum, Bismillahi*, Muislamu huyo. Kuna mwingine utakwenda mahali pengine atakuambia, nafuata dini ya babu zangu, Muafrika huyo anafuata mila za babu yake. Utakwenda utakuta Mkenya mwingine ameweka rangi nyekundu kichwani hapa, Mhindi huyo, kuna mwingine anaingia kwenye synagogue, Myahudi huyo. Hawa wote ni wakenya ama sio wakenya?

**Audience:** Ni wakenya.

**Com. Lethome:** Haya mila, mila zetu ni moja ama ni tofauti tofauti?

**Audience:** Tofauti.

**Com. Lethome:** Nyinyi mna mila zenu ama sivyo? Wewe una mila yako mimi nina mila yangu, Msomali ana mila yake, Mluo ana mila yake, kila mmoja ana mila yake. Hizi mila zote ni za Kenya ama sio za Kenya?

**Audience**: Ni za Kenya.

**Com. Lethome:** Sasa ndiyo tukasema hivi, hakuna mambo ya kutorokea kabila lako ama kutorokea mila yako au pengine dini yako la. Tambua kuwa wewe unafuata dini fulani, kabila lako ni fulani, mila yako ni fulani lakini sote ni wakenya. Kwa hivyo, tukasema sheria lazima itambue kuwa Kenya ni nchi moja lakini katika hiyo nchi moja kuna binadamu wanaoshi wanaitwa wakenya, dini zao ni tofauti, makabila yao ni tofauti, mila zao ni tofauti, lakini wao ni wa moja. Kwa Kiingereza tunasema,"*unity in diversity*". Umoja pamoja na hizi tofauti zetu, nilipokuwa nikiangalia sehemu hii, nilikumbuka aya fulani katika Qur'an ambayo inasema, "*wajaal nakum shuuban waqabaila.*" Mwenyezi Mungu asema, nimewajaalia nyinyi kuwa makundi makundi na kabila tofauti tofauti. Sasa ni kabila lipi bora Kenya nataka mniambie saa hizi watu wa Bura? Ukifikiria unaona ni kabila gani ambayo ni bora zaidi Kenya ambayo inafaa tuitukuze zaidi kuliko makabila mengine?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Mimi nitawaambia kuna kabila moja lafaa kutukuzwa kuliko mengine, niwaambie ni lipi?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Lethome**: Masaai bwana, mnaonaje tutuze wamasaai kuliko wengine. Haya mwingine mzee wa kipokomo anasema hapana bwana, wapokomo bwana, kila mmoja hupenda kuvutia kwako ama sivyo? Ni tabia ya mwanadamu hivyo, lakini tunasema sheria yataka itambue kila mmoja na kabila lake na hakuna kabila ambalo ni tukufu kuliko lingine au mila ambao ni tukufu kuliko nyingine. Kwa hivyo tumeweka katika utangulizi jambo kama hilo, Kenya nchi moja makabila mengi, dini nyingi na mila tofauti tofauti.

Ya pili, maslaha ya mwananchi anayeishi katika nchi hii ni kitu muhimu sana. Lazima yatangulizwe maslaha ya mwananchi kwa sababu, tunaweza kuwa na nchi bila ya kuwa na wanadamu ndani yake? Tunaweza kuwa na nchi?

**Audience**: Hapana.

**Com. Lethome:** Na tunaweza kuwa na Rais bila ya kuwa na watu ambao yeye anawatawala?

**Audience**: Hapana.

**Com. Lethome:** Leo hii tungeweza kuwa na mkutano bila ya watu kuwa hapa? Haiwezekani haitakuwa mkutano, unaweza kuweka hii microphone nijizungumzie mwenyewe. Kwa hviyo, tumesema sheria itambue kuwa maslahi ya mwananchi ni muhimu sana, aangaliwe mwananchi, iangaliwe na family yake na pia community yake, jamii yake aliyotoka ndani yake. Kwa mfano, kama Mohammed aangaliwe, familia ya Mohammed iangaliwe pia kisha jamii ya Mohammed kama ni jamii ya Kipokomo au ya Ki-Orma au ya Ki-Wardhei iangaliwe vizuri na sheria. Kwa hivyo, tukaweka katika utangulizi kuwa sheria hii tangu mwanzo hadi mwisho, lazima itilie umuhimu maslahi ya mtu, familia yake na jamii yake.

Kisha katika utangulizi wetu tumesema sheria lazima itambue kuwa wakenya, wakiwemo wanawake na wanaume, hamu yao kubwa ni kutawaliwa na serikali wanaitaka wao wenyewe ama sivyo? Si ndiyo tunapiga kura ama mnakwenda kupiga kura kwa nini?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Lethome:** Kwa sababu mnataka kuchaguwa viongozi ambao watawa tawala, kwa hivyo, katika sheria hii yote haya mapendekezo yote, tumetilia umuhimu sana juu ya jambo hilo kuwa wakenya wangependa kutawaliwa kwa kupitia njia ya democracia, wawezi kuhakikisha malengo yao. Kisha Kenya ni nchi huru, tungependa kuamrishwa na nchi nyingine yeyote sisi kama Kenya? Tungependa kuwa tunapewa amri kutoka nje sisi kama wakenya?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Nafikiri utawala wa ukoloni ulikwisha. Sisi ni nchi ambayo inajitawala kwa hivyo katika sheria yetu tunatambuwa kuwa Kenya ni nchi ambao ni huru na hakuna mtu ambaye anaweza kuja kutunyanganya huo uhuru wetu. Kisha tumekubali kuwa hii ni katiba ya nchi yetu.

Mwisho kabisa tumekumbuka kwa sababu ya kuwasikiza wakenya wengi wakizungumza, kuwa kuna jambo ambalo limesahaulika hapa ambalo ni muhimu sana kwa watu ambao wanaamini kuwa kuna Mungu, nalo ni Mwenyezi Mungu. Katika hii sheria yetu ambayo inatuhukumu hivi sasa, hakuna mahali Mungu ametajwa hata moja, na ninafikiri wakenya pamoja na kuwa dini zao ni tofauti tofauti, wote utasikia wakimtaja Mungu. Hata babu yangu ambaye alikuwa si Mkristo si Muislamu, alikuwa akimtaja Mungu ambaye anaitwa engai, anakumbuka kuna Mungu. Kwa hivyo, wakenya wote wanajuwa kuwa kuna Mungu kwa hivyo, tukasema katika sheria yetu mpya tumtaje Mungu, kwa hivyo tunamalizia utangulizi wetu kwa kusema "God Bless Kenya", Mungu ibariki Kenya, *Allahuma Barik Kenya*. Kwa Kisomali utajuwa utaiweka vipi na kwa Kipokomo unajuwa vile utavyoiweka sawa? Ama ki-Malakote pia naona kuna mzee wa Madogo huko pengine ni Mmalakote yeye.

Kwa hivyo, huo ndiyo utangulizi ambao tumeweka katika Katiba yetu na utangulizi una maana kuwa, yale yote yaliyomo katika hii sheria kuanzia ukurasa wa mwanzo hadi wa mwisho, lazima yazingatie hayo yaliyo katika utangulizi. Jamani tuko pamoja ama niko peke yake tu? tuko pamoja eh mpaka hapo tumefahamu sasa?
**Audience**: Ndio.

**Com. Lethome**: Kwa hivyo mmejuwa kabila tukufu ni Masaai Kenya, mmekubali? Tumekubaliana?
**Audience**: Hatuku kubaliana.

**Com. Lethome:** Hatuku kubaliana, tumekubaliana kuwa sote ni sawa, haya tuendelee sasa. Naingia katika sura ya kwanza katika hii sheria lakini ninawaambia hatutaweza kusoma kila kitu, mimi ninawapa tu kwa ufupi baadaye mtaweza kujisomea, mtaweza kuyaangalia. Mkikaa kwenye vikao vyenu vya kucheza dumna ama vikao vyenu vingine, mnaweza kupitiapitia mjadiliane, mimi nitawapa tu yale ambao ni ya muhimu kwa ufupi sana kwa sababu tukikaa hapa tukiangalia kila kitu, mpaka kesho na kesho tuko katika shughuli zingine.

Sura ya kwanza tumewapa wananchi kipao mbele, yaani tumewapa umuhimu kwa sababu tumesema sheria bila ya kuwa na wananchi, hiyo sheria haina faida yeyote. Hakuna nchi ambayo inaweza kuwa ni nchi bila ya kuwa na wananchi kwa hivyo, tumesema mamlaka yote katika nchi ni mamlaka ya mwananchi yanatokana na mwananchi. Swali, kuna yule mheshimiwa wa sehemu hii yenu, mnamuitaje mheshimiwa nani? Galgalo si ndiyo? nani aliyempeleka Bunge, Nani aliyempeleka Bunge?
**Audience**: Sisi.

**Com. Lethome:** Ile kura yako ile ambayo iko mfukoni ninajuwa hata saa hizi iko umeshika tayari kwa sababu siku karibu.

Ndiyo ulimpa ukampa uwezo wa kwenda Bunge kwenda kukuwakilisha ama sivyo?

**Audience**: Ndio.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo Bunge na mamlaka ambayo yanatumiwa na Bunge kutengeneza sheria yametoka kwa nani?

**Audience**: Mwananchi.

**Com. Lethome:** Kwa mwananchi, kwa hivyo tukasema lazima sheria itambue kuwa mamlaka ya Bunge ni mamlaka ya mwananchi, wale walioko kule ni wawakilishi wa mwananchi na ndiyo sababu katika hii sheria mpya tumependekeza wananchi baada ya kutoa mamlaka hayo kwa kiongozi akawaakilishe, ikiwa hawakuridhika na yeye na kazi anayofanya, tumependekeza baada ya kuwasikiza wakenya kuwa wananchi waweze kumrudisha kumwambia 'bwana sikiza, tumekupeleka kule utuwakilishe utufanyie kazi lakini tunaona kuwa haukuifanya kazi tunavyotaka, rudi hapa.' Kuna sehemu kama hiyo utaisoma mahali utaona kuwa tumependekeza jambo kama hilo na ni wananchi wenyewe wametaka hivyo.

Sehemu nyingine utakuta kuwa mwakilishi wa Bunge tangu alipochaguliwa mpaka mwaka wa tano anapokuja kutaka kura tena, haonekani kabisa, mnamsikia tu alionekana akipita kule, gari lake lilionekana kule. Kuna jambo lolote unaweza kumfanyia?

**Audience**: Hakuna.

**Com. Lethome**: Hakuna, utangoja tu mpaka miaka mitano iishe. Tukasema pia katika sababu moja ambazo zinaweza kumfanya mtu kama huyo kurejeshwa na wananchi ni kutowatembelea wananchi waliompigia kura na kujuwa matatizo yao na mambo mengine mengi ambayo tutaona baadaye. Kwa hivyo, tumesema pia hata mamlaka yanayotumiwa na chombo tunachokiita chombo tawala, Executive, Rais na Mawaziri. Nani alimchaguwa Rais, alijichaguwa mwenyewe ama alichaguliwa? Rais amejichaguwa ame amechaguliwa?

**Audience:** Amechaguliwa.

**Com. Lethome:** Amechaguliwa, kwa hivyo hata yeye na mamlaka aliyonayo pia tumesema yarudi kwa mwananchi, lazima yatambuwe kuwe yametokana na mwananchi. Mamlaka yanayotumiwa na Jaji anapohukuma, yametokana na mwananchi. Kwa hivyo, tumesema mtu yeyote ambaye anashikilia madaraka katika nchi ya Kenya, sheria itambuwe kuwa madaraka hayo ayatumie kwa maslaha ya mwananchi, asipoyatumia kwa maslaha ya mwananchi kulingana na Katiba, basi anaondolewa. Tumeweka sehemu nyingi sana za kuonyesha namna ya kuondoa watu kama hawa, leo hii nafikiri ukienda mahali katika ofisi yeyote ya serikali usipo hudumiwa ama ukidhulumiwa na ofisi ya serikali kuna mahali unaweza kuenda? Kuna mahali unaweza kuenda?

**Audience**: Hapana.

**Com. Lethome:** Kwanza utaambiwa hii ni kirauni Bwana, usicheze na kirauni. Sasa tumesema kirauni na ikiwepo ni muhimu kirauni ni ala ya nchi yetu lakini kirauni kimtumikie nani mwananchi. Kisipomtumikia mwananchi hatuna haja nacho kitachukuliwa hatua chini ya sheria mpya na ndio tumeweka pia mapendekezo ya kuonyesha kuwa, mtu akiyatumia madaraka

yake vibaya awe ni polisi, Chief, Assistant, kuna Chief hapa? Chief, Assistant Chief, DO, DC, PC nani wote, anaweza kuchukuliwa hatua tumebuni ofisi ambayo tumeiita, mlinzi wa watu. Unaweza kuenda kusema nimenyanyaswa na mtu fulani kwa sababu ameyatumia madaraka yake vibaya, leo hii polisi akikupiga kofi hapa kimakosa utakwenda kulalamika wapi? Utasema tu basi ninamwachia Mungu tu, ndiyo tunasema dua ya kuku haimpati nani?

**Audience**: Mwewe.

**Com. Lethome:** Haimpati mwewe lakini sasa tumesema mwewe hapatikani pia, kuwe na mahali ambapo mwananchi anaweza kuenda na kulalamika na kushtaki na yule achukuliwe hatua. Hakuna aliye juu ya sheria wote ni sawa, kama ni 'utumishi kwa wote', watumikie wananchi wasipo watumikia wananchi wachukuliwe hatua. Pia tumezingatia sana katika sura ya kwanza juu ya katiba kama nilivyotangulia kusema, katiba hata tukiandika kwa rangi ama wino wa dhahabu isipofuatwa haina faida yeyote. Tumeweka sehemu nyingi za kulazimisha kuwa sheria ifuatwe, na isipofuatwa na mtu yeyote lazima atachukuliwa hatua.

Tumetambuwa kuwa Kenya lazima tuwe na lugha yetu ya kitaifa na itiliwe mkazo sana, kwa hivyo tumesema katika vyombo vyote vya serikali, makaratasi yote nyaraka zote zinazotoka kwa serikali lazima ziwe katika lugha mbili, lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili. Lakini pia tunajuwa kuna ndugu zetu wengine, dada zetu wengine hawawezi kusoma lugha ya Kiingereza ama ya Kiswahili ama lugha nyingine yeyote kwa sababu pengine ni kipofu au ni kiziwi, ni wakenya ama sio wakenya?

**Audience**: Ni wakenya.

**Com. Lethome**: Wanafaa kujuwa sheria yetu ama hawafai, kwa hivyo tukasema pia sheria zote na nyaraka zote za kiserekali na mahali popote penye kuwa hudumia wananchi, lazima kuwe na lugha pia ya vipofu ambao tunaita Braille na lugha ingine ya visiwi ambayo tunaita sign language, lugha ya ishara ya kuashiriana. Leo hii kwa mfano, mtu ambaye ni kiziwi akitaka kusikiza habari katika radio atazipata hizo habari? Atazipata habari katika radio anataka kujuwa Nairobi kunatokea nini akifungulia radio yake atapata habari?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo, tunasema ni jukumu ya serikali kuhakikisha kuwa mtu kama huyo habari pia zinamfikia. Kipofu anaweza kusoma gazetti? Anaweza kusoma gazetti kujuwa habari zinazotokea katika nchi?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome**: Yeye ni Mkenya pia kwa hivyo, aweze kuhudumiwa. Kiziwi akifungulia Television kutizama ataiona picha na midomo ya watu atajuwa wanasema kitu gani? Ukienda nchi nyingine utakuta kwenye ile screen ya TV pale kando kuna mtu mwenye kutumia ishara ili na huyu Mkenya ambaye hasikii aweze kufuata na kujua habari zinazoendelea katika nchi. Kwa hivyo, utaona tumetilia sana mkazo kuhusu huduma au mwananchi anavyotakiwa kuhudumiwa na sheria.

Nitaruka niingie katika sura ya tatu ambayo inazungumzia juu ya uraia, citizenship. Watu hasa wa sehemu za mipakani huwa na

matatizo sana, hata utakuta wengine badala ya kuwa na kitambulisho kimoja analazimika kubeba vitambulisho viwili, kimoja kinaitwa screening card sijui kama hapa mna screening card nyinyi?

**Audience:** Iko.

**Com. Lethome**: Iko, kwa hivyo tumesema hapa wananchi wote wa Kenya ni sawa na hakuna mambo kusema huyu ni wa mpakani ama si wa mpakani. Ni jukumu la serikali kujuwa ni nani Mkenya na ni nani si Mkenya, kwa hivyo kila mmoja apewe haki sawa na wengine. Leo hii mimi nikitembea na Msomali Nairobi tukikutana na polisi atasimamishwa Msomali nitawachwa mimi, kwa nini na sote ni wa Kenya? Unaamiwa huyu ni waria toa kitambulisho waria, akishatoa kile cha kawaida anaambiwa toa ile ingine ya ma waria, kama kuwa si Mkenya au sivyo? Kwa hivyo, tumesema ubaguzi kama huo au mwanamke wa Kiislamu anavaa bui bui lako ataanza kuulizwa maswali mia moja na pengine ni Mkenya kutoka hapa hapa Bura. Kwa hivyo tumesema wananchi wote au raia wote wa Kenya ni sawa na uraia ni tofauti tofauti kuna uraia wa kuzaliwa, mtu aliyezaliwa Kenya ama aliyezaliwa mahali popote lakini amezaliwa na wazazi ambao ni wa Kenya au pengine mama ni Mkenya, baba si Mkenya au baba ni Mkenya mama si Mkenya. Sheria imetambuwa mtoto kama huyo ni Mkenya.

Kuna uraia mwingine ambao unapatikana kwa ndoa, hivi sasa sheria hii ambayo tunafanya kazi nayo hivi sasa, imembagua mwanamke Mkenya, imempaa haki zaidi mwanaume Mkenya hivi kwamba mwanaume Mkenya akimuoa mwanamke kwa mfano, huyo mwenzangu hapa akivuka ama akimleta msichana kutoka ngambo ile, Somalia, ama sehemu nyingine yeyote basi yule mkewe baada ya muda atatambuliwa kuwa ni Mkenya ana haki ya uraia ndiyo sheria hii inavyosema. Na watoto mtakaozaa wana uraia wa Kenya, kinyume na hivyo msichana Mkenya akiolewa na mtu ambaye si Mkenya hata wakija kuishi naye hapa Kenya, sheria inasema yule mume hana haki ya uraia na hata watoto watakosa haki ya uraia, utakuta hapo sheria imembaguwa mwanamke Mkenya.

Mapendekezo ya sheria mpya ni kuwa, mwanamke Mkenya ana haki pia ya kumpa mumewe ambaye si Mkenya haki ya uraia na mtoto wake pia ambaye amemzaa na mtu ambaye si Mkenya anampa haki ya uraia. Kwa hivyo, kuna usawa baina ya mwanamke na mwanaume, najuwa wazee wengine wanasema lakini hii itatuletea matatizo, watu wengi watatoka katika nchi yao yenye fujo wanakuja kuoa mabinti zetu ili wapate uraia ama sivyo mzee unajiuliza hilo swali? Kabla huJajiuliza mimi nina kujibu, kukuambia kuna kitu ambacho tunaita administration utawala. Ni juu ya serikali kuweka sheria za kuhakikisha kuwa ruhusa kama hii ambayo imetolewa haitumiwi vibaya, kila ruhusa ikitumiwa vibaya huwa ina madhara yake kwa hivyo, ni ruhusa tu imetolewa lakini ina madhara yake ni juu ya serikali kuhakikisha ni nani anaitumia vibaya na ni nani ambaye haitumii vizuri. Hata chakula ukiitumia vibaya kitakudhuru ama sivyo? Chakula ukikitumia vibaya hakikudhuru?

**Audiecne:** Kitakudhuru.

**Com. Lethome:** Itakudhuru bwana utavimbiwa ukila sana, ukila mihogo mingi sana tumbo itafura, sasa kila jambo na mipaka yake ama sivyo? Kwa hivyo hata hii, hili lina mipaka yake.

Kuna uraia mwingine ambayo tunaita citizenship by naturalization, uraia wa kujiandikisha mtu yeyote ambaye ameishi Kenya kwa muda wa miaka saba au zaidi mfululizo, ana haki pia ya kusajiliwa kama Mkenya akitimiza masharti yanayo takikana, sio pengine jambazi tu limetoroka huko limefanya uhalifu limekuja huko lataka kufanya uhalifu limekaa miaka saba halafu lipewe uraia. Ni juu ya serikali pia kuhakikisha wanaopewa uraia ni watu wa kisawa sawa, kwa hivyo, baada ya miaka saba mtu ambaye si Mkenya anaweza kujiandikisha.

Mtoto ambaye anapatikana katika eneo la Kenya chini ya umri wa miaka minane, hajulikani wazazi wake hajulikani alikotoka, kwa sababu ya kuifadhi haki za binaadamu mtoto kama yule atachukuliwa kama kuwa ni Mkenya. Kuna watu wengine ambao pengine huchukuwa watoto kwa njia ambao tunaita kwa kizungu adoption, yaani kumchukuwa yule mtoto ambaye si wako na ukamuandikisha kama mtoto wako kwa Kiarabu wanaita *Attabani*, sijui kwa lugha za kwenu huku mnaitaje. Kumchukuwa mtoto ambaye si wako ukamuandikisha kama mtoto wako, hiyo inafahamika hapa lakini? Kuna wazazi pengine hawakujaaliwa kupata watoto ama wametaka tu kumlea mtoto wanamchukuwa wanamuandikisha kwa kizungun tunaita adoption. Mtoto kama yule akiwa kwa mfano, si Mkenya lakini amechukuliwa na Mkenya na yule mtoto hajafikisha miaka kumi na minane ama zaidi, basi yule mtoto atachukuliwa kuwa ni Mkenya.

Jambo lingine ambalo wananchi wengi wamelizungumzia ni kuhusu uraia wa nchi mbili, dual citizenship. Leo Kenya hauwezi kuwa raia wa Kenya na raia wa nchi nyingine yeyote, lazima itabidi upoteze uraia wa nchi moja. Nchi zingine wanakubalia raia wao wawe na uraia wa nchi mbili, tumependekeza pia chini ya sheria mpya Mkenya aweze kuwa na uraia wa nchi mbili. Iwe kwa mfano, unaweza kuwa na Passport ya Somalia, Ethiopia, Uganda pamoja na Kenya au ya Uingereza na Kenya, Marekani na Kenya, inatokea katika nchi nyingi. Isipokuwa tu ukiwa kiongozi basi hatuta kubali mtu ambaye ana uraia wa nchi mbili, kwa mfano, Rais wetu hapa Kenya pia na raia wa nchi nyingine, haiwezekani kwa sababu huenda ikawa anafuata amri za kule kuliko huku. Kwa hivyo, chini ya sheria mpya kutakuwa na kitu kinachoitwa dual citizenship, ni juu ya serikali kuhakikisha kuwa ruhusa hii ambayo imetolewa na sheria haitumiwi vibaya.

Sheria pia imependekeza chini ya sura ya tano, Chapter Five ambayo ndiyo muhimu sana sisemi sehemu zingine sio muhimo lakini hii ndiyo muhimu zaidi kwa sababu inaangalia haki za binadamu. Hii ndiyo ile ambayo inaitwa chini ya katiba yetu ya sasa na pia katika mapendekezo yetu the bill of rights, sheria kuhusu haki za kimsingi, haki za binadamu, haki ambazo hata serikali haiwezi kukunyanganya. Haki ambazo hata ukiwa jela uko nazo, ukiwa katika cell ya polisi uko nazo, hata maiti baada ya kufa ana haki za binadamu maiti yake ihifadhiwe kwa sababu, maiti ya binadamu na maiti ya mnyama ni tofauti, mzoga wa punda utatupwa kule tu, unaweza kutupa maiti ya binadamu hivyo?

**Audience:** La.

**Com. Lethome:** Kwa sababu ni binadamu kuna haki fulani alizo nazo kwa hivyo, utaona hiyo ndiyo sehemu kubwa zaidi katika mapendekezo haya ya sheria mpya imechukuwa zaidi ya ukurasa karibu hamsini katika sheria hii mpya. Na sababu ya kuzingatia hizi sheria na kuzitilia mkazo sana hapa ni kuwa bila ya hizi sheria zinazo angalia haki za msingi za binadamu, hata

mambo ya maendeleo hakuna. Mambo ya usalama katika nchi itakuwa hakuna, mambo ya umoja katika nchi itakuwa hakuna, kwa mfano, nikuweke hapa mchana mzima bila chakula mpaka kesho, tutasikizana hapa, mtakubali kunisikiza hapa tena?

**Audience**: Hapana.

**Com. Lethome:** Kwa sababu kuna haki ya msingi bwana binadamu lazima ale hata gari lazima itiliwe petroli, itakwenda bila petroli? Ni haki ya msingi ya gari ipate petroli na ni haki ya msingi ya binadamu apate chakula, au pengine mtu ni mgonjwa anaumwa na malaria atakaa hapa anisikize kweli? Hawezi kukaa hapa anisikize kwa hivyo, utaona afya ni haki ya msingi ya binadamu. Kwa hivyo tutaziangalia hizo haki ni zipi, haki ya kwanza ningependa hebu tushirikiane mniambie ni zipi ambazo mnafikiria ni haki za msingi za binadamu yeyote, nani ataniambia mfano mmoja wa haki za msingi za binadamu? Haki ambazo uko nazo wewe kwa sababu wewe ni binadamu, sio kwa sababu serikali imetaka.

**Audience:** Haki ya chakula.

**Com. Lethome:** Haki ya chakula, hiyo ni haki moja. Haki ya msingi chakula, nyingine?

**Audience:** Afya.

**Com. Lethome**: Afya, nyingine?

**Audience:** Kuvaa

**Com. Lethome:** Kuvaa nyingine?

**Audience:** Maji.

**Com. Lethome:** Maji, nyingine?

**Audience:** Makazi

**Com. Lethome:** Makazi, hakuna binadamu anaishi kwenye mti kama tumbiri au ndani ya shimo. Huwezi kuzipata, vijana huko nje ni haki yetu pia ya msingi mnyamaze mnasikia waria? Hebu wanyamazishe hawa vijana tuna recordi kule bwana. Haki ya kwanza ambayo bila hiyohaki huwezi hata kuzifurahia haki zingine ni haki ya uhai, bila ya kuwa hai utafurahia haki zingine? Na uhai wako kuna mtu ambaye amekupa, kuna mtu aliyekupa uhai?

**Audience**: Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna, sio serikali iliyokupa wala kiongozi wala MP wala nani, umepewa na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, sheria ihifadhi uhai wa binadamu ni haki ya msingi na ndio baadhi ya watu wengi wamependekeza kuwa, ile sheria iliyoko hivi sasa kuwa mtu akiuwa auawe, ahukumiwe kunyongwa iondolewe, mtu akiuwa ahukumiwe kufungwa kifungo cha maisha.

Mambo ya usawa ni haki ya msingi kuwa nisibaguliwe kwa sababu mimi ni Masaai na nimekaa sehemu za Wamalakote, ni haki yangu ya msingi nisibaguliwe. Ni haki yangu ya msingi nisibaguliwe kwa sababu mimi ni masikini kwa sababu mimi ni Muislamu

au Mkristo au dini nyingine au kwa sababu ya mila yangu. Usawa wa watu wote na nisibaguliwe kwa sababu mimi ni mwanamke au ni msichana kwa sababu tuseme mwanamume ni bora kuliko mwanamke la. Sheria inasema watu wote ni sawa kwa hivyo, usawa ni haki ya msingi hasa usawa mbele ya sheria.

Freedom on discrimination pia, uhuru wa kutobaguliwa kwa misingi tofauti tofauti kama vile kwa sababu ya kabila la mtu kwa sababu ni mwanamke ama ni mwanamume, kina mama si mnabaguliwa sana kwa sababu ni wanawake?
**Wanawake:** Ndio.

**Com. Lethome:** Unaambiwa mwanamke anasema nini mbele ya wanaume ama mzee amefariki amewacha watoto wa kike na wa kiume. Mali yote inapewa nani, mali ina kwenda kwa nani?
**Audience:** Vijana.

**Com. Lethome:** Msichana anaambiwa huna haki ya kuridhi wewe, tunasema hiyo ni discrimination ni ubaguzi au ana baguliwa kwa sababu ni mja mzito, ana kwenda kutaka kuajiriwa kazi anaambiwa wewe ni mja mzito huwezi kuajiriwa kazi hapa ama hatutaki kumuajiri mtu ambaye bado anazaa, atatupatia taabu hapa ya maternity leave. Huko ni kubaguliwa chini ya sheria mpya unaweza kumshtaki mtu akikubaguwa kwa sababu ya msingi kama huo. Kwa sababu ya kuwa pengine haujaoa unaambiwa hapa haingii mtu ambaye hajaoa, kutooa si dhambi na pengine time yake bado au kwa sababu ya rangi yake, umri wake hasa wazee wanabaguliwa sana. Sehemu nyingi utakuta mzee kama huyu anabaguliwa anaambiwa wewe mzee kaa huko kando bwana hapa ni mahali pa vijana na unasahau hata wewe kijana unaelekea huko huko ama mzee ni Mkenya ama si Mkenya? Mzee si Mkenya?
**Audience:** Mkenya.

**Com. Lethome:** Kwanza yeye ndiyo tunamuita senior citizen, ndiyo mwananchi wa kwanza kabisa huyu kama si yeye hatungepata yale tuliyonayo hivi sasa. Kwa hivyo, asibaguliwe kuna watu wengine ambao wanabaguliwa sana sana vilema, hawa wanabaguliwa sana sana. Utakuta hata hivi tulivyokaa hapa tumewabagua ukiangalia pale mlangoni wa kuingia hapa ndani, kilema ambaye pengine anakuja na lile gari lake la kujikokota anaweza kuingia pale, anaweza?
**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Mpaka abebwe na watu wengine pale hawezi kuingia, utakuta kilema anakwend afisini anataka kumuona PC, PC yuko katika gorofa ya tatu, hakuna lift ya kwenda huko kuna ngazi kilema anayetembea kwa mikongojo ile anaweza kupanda mpaka kule juu?
**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Wanabaguliwa, tunawabuaguwa kwa njia nyingi sana mpaka majumbani kwetu kila mmoja anajijuwa hapa, ukiwa na mtoto kiwete ama kilema ama kidogo akili zake zimepungua, wageni wakija unamficha ama sivyo tunavyofanya

wazee? Tunamficha huko, ni mwanadamu ama si mwanadamu? Amependa yeye kuwa hivyo? Amependa?

**Audience:** Hakupenda.

**Com. Lethome:** Hakupenda tunawabaguwa, sheria imesema ni makosa kumbaguwa mtoto au mtu yeyote kwa sababu ya kuwa ni kilema awe ni kipofu ni kiziwi, lazima tuangalie haki zao na kuna sehemu ambayo inazungumzia juu ya haki za watu wenye vilema kuanzia lugha tunayotumia, tusitumie lugha ambayo ni ya kuwadharau wale watu. Hata lugha ya Kiswahili nafikiri wale waliobuni lugha ya Kiswahili hawakuchaguwa maneno mazuri ya kuwazungumia wale ambao wana vilema. Kwa mfano, tunasema kiti viti, wale ambao ni wajuzi wa lugha ya Kiswahili, vitu ambavyo havina uhai ndiyo tunaviita KI-VI, kiti viti, kiatu viatu, kiazi viazi ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Haya tuingie katika watu wenye vilema, kipofu vipofu ama sivyo, kiziwi viziwi, kilema vilema. Tumewafanya kama kuwa si wanadamu, tunawaita majina ambayo ni ya kuwavunjia utu wao na katika mila zingine utakuta akipita mtu kilema mahali hata watoto wanamrushia mawe ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Tunamchukulia kuwa si mwanadamu, haki zake haziangaliwi kabisa. Katika kikao kama hiki tunasahau kuwa pengine kuna mtu ambaye hasikii vizuri, angependa kuwa na mtu wa ishara wa kumonyesha tunasema nini, au mwingine ana kwenda, tunapata habari tunapotembea anakwenda kwa ofisi, nataka kumuona DO ama DC, DO akishaambiwa ni yule msichana kiwete ama ni yule mvulana kiwete anasema, ah shauri yake azungumze na secretary huko kisha atoke. Anadharauliwa kwa sababu, ni kilema, utakuta kama ni booth ya telephone zinatengenezwa hivi kwamba mtu ambaye ni kilema hawezi kuifikia ile booth mahali ilipo hawezi kupiga simu, hana haki ya kupiga simu? Leo hii mtu kiwete aje kwako anataka kuposa msichana wako, utamuoza? Utamuoza niambie? Itakuwa shida sana yeye kupata mtu wa kuoa ama wakuolewa, msichana wako akiwa kilema basi ndiyo haolewi tena kabisa. Ni nani, yule kiguru, aha. Hiyo yote tunaita ubaguzi, discrimination na tunasahau Waswahili wanasema na nyinyi ni waswahili hapa watu wa Coast, "*mwanadamu haishi kuumbwa maadamu yuko hai*", ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Na njiani nimeambiwa na mwenzangu Wasomali pia wana msemo kama huo kuonyesha kuwa unaweza kuwa leo wewe ni mzima, kesho ukapatikana na ajali ukawa wewe ni kilema si mmeshaona watu kama hawa, umezaliwa na miguu miwili, umeishi na migu miwili mara unapatikana na ajali, inakuwa huna miguu unakuwa ni mtu wa kujikokota. Ulikuwa na mikono miwili moja ukakatika, ulikuwa na macho unaona, yakapotea ukawa ni kipofu, ulikuwa unasikia ukawa ni kiziwi. Kwa hivyo, tunapoanga haki za watu wasiojiweza vilema, na sisi pia tujuwe kuwa dakika yeyote unaweza kuingia hapo ama sivyo? Dadika yeyote unaweza kuwa kilema wewe ukaingia hapo, hiyo nimeitilia mkazo sana kwa sababu, tuna maradhi katika jamii yetu kama wakenya ya kuwabaguwa watu kama hawa.

Mambo ya kubaguliwa kwa sababu ya dini na lugha ya mtu au kwa sababu ya mahali alipozaliwa pia imepigwa marufuko. Wanawake ni watu ambao wamebaguliwa sana katika nchi ya Kenya, kwa hivyo, tumesema wanawake wapewe haki zao katika kila nyanja kama ni nyanja za elimu, za kisiasa na kila mahali wapewe haki zao. Najuwa kuna zile za kidini pia sizivunjwe kwa mfano, mwanamke wa Kiislamu ana haki ya kuridhi kama mwanaume lakini kiwango chake cha kuridhi ni tofauti kwa sababu ya majukumu aliyonayo mwanaume, lakini asinyinmwe haki yake. Nyinyi watu wa hapa sijui mwanamke ana ridhi ama haridhi kimila, nataka kujuwa kimili anaridhi?

**Audience:** La haridhi.

**Com. Lethome:** Kwa nini haridhi ndungu yangu? Kwa nini mwanamke haridhi? Atapeleka uchumi kwingine, na wewe si vijana wako wataleta pia uchumi kutoka kwingine? Kwa hivyo, mambo kama hayo yaangaliwe. Watu walio wakongwe mtu aliyefikisha miaka sitini na zaidi ana ..

**Interjection:** Hata elimu hawapewi.

**Com. Lethome:** Hata elimu hawapewi, hata Waislamu hawapewi elimu na tunaambiwa katika hadithi ya Mtume (S.A.W.) kuhusu kutafuta elimu, ametengewa mwanaume peke yake ama ni wote?

**Audience:** Wote.

**Com. Lethome:** Wote wawili wamelazimishwa wafuate elimu, kwa hivyo ni makosa na Mtume (S.A.W.) amesema katika hadithi moja kuwa, '*yeyote atakaye ruzukiwa ma binti wawili au zaidi kisha akawapa malezi mazuri na masomo mpaka wakawa watu wazima, zawadi yake ni nini? Aljanna, pepo."* Haya ni maneno ya Mtume (S.A.W.) si yangu bwana, haya maneno sikuyatoa kule masaini nimetoa katika vitabu vya dini bwana. Kwa hivyo, angalieni huku na huku bwana tunavunja dini tunavunja hata na mila wakati mwingine tunazivunja kwa sababu mtu ni mwanamke, sheria imekataa mwanamke kubaguliwa.

Watoto pia wapewe haki zao wasibaguliwe na katika haki ya msingi ya mtoto ni kupewa elimu na ndiyo sababu, chini ya sheria mpya tumesema elimu ya msingi imekuwa ni compulsory lazima, mzee atalalamika aseme na kama sina uwezo wa kumpeleka mtoto ama sivyo hali ilivyo hivi sasa, mtu unataka kumpeleka lakini huna uwezo imekuwa unaambiwa school fees hakuna lakini kuna mambo sijui ya kulipia mjengo, sijui pesa za harambee, nafikiri hata zimekuwa juu ya fees tuliyokuwa tukilipa zamani ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa tumesema ni juu ya serikali kuhakikisha ikienda kufikia miaka miwili kila mtoto Mkenya anapata elimu ya bure ya msingi ambao ni ya lazima. Maana yake ni nini, mzazi asipompeleka mtoto wake aliyetimia umri wa kusoma, anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa sababu, huyo mtoto usipo mpeleka kusoma unamuharibia maisha yake, hata kama ukimuachia mali millioni ngapi bila ya kumpa elimu, umemdhulumu yule mtoto. Kwa hivyo, tumesema ni haki ya kila mtoto

kupata elimu, mtoto kama amekosa asifungiwe na watu wazima kuwe na sehemu maalum ya kuwafundisha watoto ambao ni watundu watukutu waweze kufundishwa warekebishwe tabia zao.

Ni haki ya mtoto pia kupata malezi mema kutoka kwa mzazi, kuna wazazi wengine hataki kujisumbuwa na ndiyo maana katika mitaa yetu utakuta kuna wale watoto ambao tunawaita chokora. Machokora wamezaliwa na binadamu ama hawakuzaliwa na binadamu? Amezaliwa ana baba na mama, kuna watu wawili ambao waliwazaa hawa watu lakini kwa sababu hawataki majukumu yao ya kuangalia wale watoto ndiyo wameachilia. Kwa hivyo, tumesema chini ya sheria mpya lazima wapewe haki hizo. Familia pia ina haki kwa hivyo, ni juu ya serikali kuhakikisha kuwa familia zimelindwa utukufu wa familia na heshima ya familia ilindwe.

Persons with disability: Watu wenye vilema ni lazima wapewe haki zao zote kwa sababu ni wanadamu kwa hivyo, sheria lazima izingatia kuwa wanahesima fulani ambayo lazima wapewe kama wanadamu wengine. Pia wakenya wote wafundishwe juu ya mambo yanayo sababisha ulemavu, kama nilivyowaambia sasa, usimuangalie yule mlemavu na usahau kuwa wewe pia unaweza kuwa mlemavu au unaweza kuzaa mtoto mlemavu. Kwa hivyo, jamii iweze kuelezwa sababu za ulemavu, wahakikishiwe wanapata elimu wazungu wana msemo ambao unasema “disability is not inability”, kuwa ulemavu sio kutojiweza, ulemavu sio kutojiweza sisi katika Commission yetu aliyekuwa naibu wa mwenyekiti wa kwanza amefariki hivi sasa juzi juzi, Dr. Oko Ooko Ombaka alikuwa ni kipofu ama mlijuwa hivyo? Alikuwa ni kipofu lakini nafikiri katika hiyo Tume yote hakuna mtu ambaye Mwenyezi Mungu alimpa akili kama yake, nafikiri Kenya nzima pengine watu wawili, watu walikuwa na elimu aliyokuwa nayo yule bwana, kipofu haoni.

Kwa hivyo, mtoto wako akiwa ni kipofu ni kilema mpe elimu, kuna sehemu ambapo utakuta Nairobi kuna Jaji ambaye yuko katika mahakama kuu ambaye ni kiwete anakwenda kwa magurudumu kortini na ni Jaji amesoma. Kwa hivyo, serikali ihakikishe kuwa wanapewa elimu na wahakikishiwe kuwa wanafikia huduma zote, kwa hivyo hata tunapojenga majumba yetu, lazima tuwafikirie pia hawa watu, leo hii akija mtu kilema na gari lake la magurudumu anataka kuingia hapa kunywa chai, atawezaje kuingia hapa? Mwenye kujenga hili jengo afikirie, PC anapokaa kwenye ofisi yake afikirie mtu mlemavu akitaka huduma yangu atanifikia vipi huku juu niliko mimi? Wanaojenga mabaraza ya miji, wanapojenga vyoo waangalie huyu kilema anayetembea kwa miguu, anayetambaa kwa mikono na miguu akitaka kujisaidia katika hiki choo atajisaidia vipi? Kilema huyu akitaka kuingia katika Posta ama sehemu nyingine ataingia vipi? Kwa hviyo, wafikiriwe katika huduma zote za nchi.

Lugha ambazo zinawafaa watu walemavu kama vile lugha ya Braille ya vipofu, sign language ambayo inatumiwa na watu ambao hawasikii wala hawawezi kuzungumza pia ifanyiwe. Vyombo vyetu kama vile Bunge na ma baraza ya miji, kuwe na muakilishi mtu ambaye anawakilisha matatizo ya watu ambao ni walemavu yaani kwa ufupi wasibaguliwe, wana haki kwa sababu wao ni wanadamu.

Kuna uhuru wa mwanadamu, kila mmoja yuko uhuru kufanya anavyotaka maadamu tu asivunje sheria na pia kila mmoja

anahitaji amani. Imependekezwa ni jukumu la serikali kuangalia kuwa kila mmoja ana amani na uhuru wake lakini usiende kuvunja sheria halafu ukadai unataka uhuru wa amani ama uhuru wa kutembea unavyotaka. Huo uhuru utaufurahiya tu ikiwa unafuata sheria, isiwe kwa mfano wewe, useme mimi ninataka uhuru wa kuenda kupora ngombe wa hili kabila karibu na nyinyi mnaliitaje? Hawa walio karibu na nyinyi ni kina nani?

**Audience:** Wasomali.

**Com. Lethome:** Useme mimi ninataka freedom sheria imenipa freedom ya kuenda ninapotaka kwa hivyo, ninaenda kupora ngombe wa wasomali, utachukuliwa hatua ya sheria bora tu usivunje sheria.

Mambo ya utumwa, nyinyi kwa lugha yenu mnaitaje mtumwa?

**Audience:** *Adhon.*

**Com. Lethome:** *Adhon*, ala mimi nilikuwa nishavuka North Eastern nimewachana na Adhon huko, iko kumbe hata hapa. *Botha* sheria imevunja hayo mambo ya kusema mtu ni mtumwa slavery, *adhon* ama *botha* hakuna. Ama kazi za kulazimishwa kwa mfano, mzee ana lorry lake aniambie wewe ni dereva? Ndio, nataka wewe gari langu ukiliaendesha mpaka Hola ama Malindi na ukirudisha hapa mshahara kiasi fulani, ukisema la? Ana haki ya kunilazimisha? Ana haki ya kunilazimisha hata mfanyikazi wako nyumbani huna haki ya kumlazimisha kwa hivyo, mtu afanye kazi kwa hiari yake.

Mambo ya uhuru wa kuhifadhiwa kile tunachoita siri ama privacy ya mtu, kwa mfano, kuna mtu anaweza kutaka akiwa bafu anaoga aingiliwe na mtu mwingine yeyote? Utakubali mtu yeyote akuone ukiwa bafu ukioga?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Labda uwe hapa kidogo kuna upungufu fulani, lakini hapa kukiwa timamu, hakuna mtu hata mtoto mdogo yule hakubali anataka siri zake. Kuna baadhi ya siri ambazo binadamu lazima ahifadhiwe nazo. Ama nyumbani kwako unavyoishi na mke wako, ungependa kila mtu ajue unavyoishi na mke wako? Hiyo ni haki yako kama mwanadamu siri yako ya nyumbani ihifadhike, ama ungependa barua unayomuandikie mke wako, mtu mwingine aje aisome ungependa ama ije iwekwe pale barazani imetundikwa pale kila mtu anaisoma, ungependa? Unapenda hivyo mzee?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Ama simu unazungumza Hallo na mama watoto kisha kuna mtu mwingine anasikiza huko, utapenda ama mtu kuingilia nyumba yako hata kama ni polisi ama nani, kuingilia huko akute kina mama hawajavaa nguo vizuri, kuna mtu atapenda kitu kama hicho?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Hiyo ni haki yako ya kimsingi haifai kuvunjwa na mtu yeyote hata serikali wakitaka kuingilia huko kuna utaratibu fulani wanafaa kufuata. Kwa hivyo, hiyo tunaita privacy lazima iheshimiwe hata unapofanyiwa search kwa mfano, unasafiri wewe na mke wako ufike mahali kwenye barrier, nimeona hapa kuna barrier moja hapa hivi, utakubali yule askari mwanaume aanze kumpapasa mke wako kila mahali anafanya search?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Eh, wazee wengine atatoa kisu hapo aseme afadhali kufa bwana ama vipi?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Eh bwana this is too much, haiwezekani kama mnataka kum-search mke wangu, kwa adabu bwana tafuteni askari mwanamke afanye hiyo kazi. Hata wewe mwanaume utakubali askari akushikeshike kila mahali ati anafanya search, utakubali?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo, tumesema haya mambo yote yaweze kuhifadhiwa na sheria.

Uhuru wa dini hapa tuna Waislamu, tuna Wakristo, tuna dini zingine kuna mtu amekulazimisha kuwa Muislamu Sheikh, umelazimishw ana mtu yeyote? Kwanza ndiyo inakuambia '*Lla ikraha fi din'*, kwanza dini ya Kiislamu sijui walichukuwa kutoka katika Qur'ani hiyo,'*Lla ikraha fi din'*, hakuna kulazimishana mambo ya dini. Na hakuna mtu kuniambia no, usiende Msikitini kuswali, tutapambana na yeye sasa anaingilia uhuru wangu wa dini. Sheria imesema hapa kila mmoja ana uhuru wa kuabudu, kila mmoja ana uhuru wa kufuata dini anayoitaka. Hiyo ndiyo Kenya tuliyo nayo kila mmoja ana uhuru wake wa kuabudu na hakuna mtu ambaye anaweza kuingilia dini ya mtu mwingine na kama nitakavyo waeleza baadaye kila uhuru una mipaka yake. Hata huo uhuru wa dini, kuna wakati hufika inakuambia sasa hii imezidi sana, ikiwa katika wewe kutekeleza uhuru wako wa dini unamvunjia mtu mwingine haki yake, huo uhuru utazuiwa. Kwa hivyo, wewe una uhuru wa kuabudu unavyotaka, kufuata dini unaotaka bora tu, usingilie dini yangu bwana wala usiingilie haki yangu pia. Una haki na mimi nina haki pia tukae balance ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo, sheria wale ambao watasoma zile nyaraka zetu mtaona kuwa tumeeleza kwa kirefu kuhusu maswala ya kuabudu.

Freedom of Expression: Uhuru wa kujieleza ni kama hivi sasa mnajieleza yale niliyonayo hamwezi kujuwa mpaka nijieleze kwa hivyo, tunasema sheria itoe uhuru wa kila mtu, ni uhuru ama ni haki ya kila mwanadamu kujieleza. Hata ukienda hospitali bila ya

kuzungumza daktari atajuwa unaumwa na wapi?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Lazima useme mimi ninaumwa na hapa bila ya kulalamikia mkubwa atajuwa una matatizo gani? Kwa hivyo ni haki wakenya wasilazimishwe kunyamaza ati usizungumze hakuna ruhusa ya kusema la. Kama kibaya ni kibaya watu waseme bora tu tusifanye fujo kama kitu ni kizuri ni kizuri, hatumtaki kiongozi fulani tufanyeni maandamano tueleze kuwa hatumtaki, tuandikeni katika magazeti, tuelezeni katika vyombo vya habari. Uhuru wa kujieleza bora tu, usiutumie ule uhuru wa propaganda ama kueneza fitina kuchochea, kwa mfano, nije hapa mimi niseme nina uhuru wa kujieleza niwaambie, sasa bwana watu wa Bura hapa, watu wa ile Bura nyingine kule wale ma waria wanajitayarisha kuja kuvamia mali yenu hapa, hapo nitakuwa nimechochea ama sikuchochea?

**Audience:** Umechochea.

**Com. Lethome:** Nimechochea kwa hivyo, utumie uhuru wako wa kujieleza bila ya kuchochea na bila ya kuvunja sheria.

Haki nyingine ambayo tumesema ni, access to information. Kuna baadhi ya habari ambazo ziko mikononi mwa serikali au ziko mikononi mwa watu wengine lakini ni muhimu kwa kila mwananchi kujuwa. Kwa mfano, tunajuwa kuwa kuna wakati kulitokea fujo watu wakauawa wengi sana Likoni ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Molo kuna wakati watu wengi sana waliuliwa, Wajir kuna mahali panaitwa Wagalla, watu waliuawa. Kuna pahali pengine panaitwa Markamali watu waliuawa, baada ya watu hawa kuuawa kuliundwa Tume ya uchunguzi, Commission of enquiry ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Matokeo yake mpaka leo hii nani anajuwa? Kuna mtu anaijuwa?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Hakuna mtu anaijuwa hata ndiyo jana naona kuna mtu amekwenda kortini amepata order kuhusu mambo ya Likoni fujo zilizotoka Likoni, serikali inalazimishwa na korti itoe hiyo information. Kwa sababu ni haki ya wananchi kujuwa matokeo yake ni yapi, kulitokea nini ili watu waweze kukaa kwa amani na kujuwa kuwa kukitokea jambo serikali itafanya uchunguzi na tutajuwa matokeo ya lile jambo. Mara nyingi utakuta mambo kama hayo ina kuwa ni siri ya serikali, kuna baadhi ya mambo ambayo ndio ni siri ya serikali ni muhimu yawe ni siri ya serikali kwa sababu, pengine atahatarisha usalama wa nchi lakini kama hayakuhatarisha usalama wa nchi, inakuwa ni haki ya kila Mkenya kujuwa mambo kama hayo.

Kama mambo ya devil worship, kumuabudu shetani mshasikia mambo kama hayo? Kuliundwa tume ya kuchunguza na

wakaandika reporti. Reporti yenyewe tunajuwa mpaka sasa matokeo yake? Hakuna, kwa hivyo tunasema ni haki ya kila Mkenya kuweza kupata habari kama hizo.

Freedom of Association and Assembly: Haki za kujiunga na kundi lolote unalotaka kwa mfano, mimi ni mtu ambaye nafuata chama fulani cha kisiasa, hakuna mtu ana haki ya kuniambia la, toka katika hicho chama nenda katika chama kingine au nimejiunga hapa na kundi la wazee, kuna wazee hapa wamejiunda wana kundi lao la wazee wa Bura. Hakuna ruhusa chini ya sheria kwa mtu yeyote kuja na kuwaambia la, nimevunja kikao kama hicho. Ama kikao kama hicho chetu tulichokaa hapa, hivi sasa sisi tunatumia haki yetu, freedom of assembly, haki ya kukusanyika pamoja na kufanya jambo tunalotaka maadamu hatukuvunja sheria.

Kwa hivyo, sheria zile za kikoloni lazima uwe na permit, lazima upige reporti mahali fulani maadamu hatufanyi fujo tuna haki ya kukusanyana. Nina haki pia ya kujiunga na kundi lolote ambalo ninataka, hiyo ni haki yangu kama binadamu. Binadamu anaweza kuishi peke yake? Hawezi kuishi peke yake, hata wale wengine wataalamu wanasema, 'mwanadamu is a social animal' ni mnyama ambaye lazima aishi na wengine, hawezi kuishi peke yake na ndiyo sababu, hapa kati kati utakuta msitu hakuna mtu anaishi ndani. Mtu anataka kuishi karibu na watu wengine, leo hii ploti hapa town ni ghali na jee kule msituni ploti, hata kuna mtu anataka kunua ploti huko? Unaishi huko uishi na nani? Kwa hivyo, kila mmoja ana uhuru huo.

Uhuru wa kisiasa, mzee wewe unafuata chama yeyote ya kisiasa? Chama gani wewe ni mtu wa chama gani?
**Mzee:** KANU.

**Com. Lethome:** KANU, kuna mtu alikulazimisha kujiunga na KANU, kuna mwingine wa DP, mwingine wa NDP, Ford Kenya, Ford Asili, Rainbow na nini. Hiyo ni haki ya kisiasa ya kila mmoja ama sivyo? Mimi nina chama changu kingine, ukijaribu kunilazimisha nitoke, tutapambana, hiyo ni haki yangu bwana chini ya sheria. Ama unilazimishe na kuna wengine wazee wanalazimisha bibi yake wanasema, sisi mama watoto, mimi ni mwanacham wa KANU damu na wewe lazima nyumba hii ni KANU dmau yote, utakuwa unawavunjia haki zao. Si kuna wazee wengine hivyo, ati kura lazima upigie mtu fulani, usipopigia utaniona utajuwa nani jogoo nyumba hii. Hiyo unamvunjia haki yake ya kisiasa, mama ana haki yake ya kisiasa, wewe una haki yako, akisikizana na wewe, akikubali kufuatana na wewe sawa. Asipokubali muache afuate chama kingine chochote, utasikia hapa wazee wanapelekwa kortini siku moja wewe ngoja.

Uhuru wa kutembea, freedom of movement na kuishi mahali popote. Kwanza hapa Bura kuna plot zinapatikana hapa? Iko? Mimininataka kuja kukaa hapa kuishi hapa kuna mtu ana haki ya kunizuia? Kuna mtu?
**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Nina haki ya kuishi mahali popote Kenya na nisibaguliwe kama vile wewe una haki ya kuenda kwa wajaluo uishi ama kwetu masaini ukaishi ama mahali pengine popote. Freedom of movement and residence, bora tu usivunje sheria.

Kuna watu weingine ambao tunawaita wakimbizi kwa sababu ya matatizo katika nchi zao wanakimbilia katika nchi yetu kwa sababu kuna usalama, ni binadamu ama si binadambu? Kwa hivyo tumesema kuwe na sheria pia za kuangalia watu kama hawa waangaliwe haki zao lakini pia wale wenyeji wa pale wasidhulumiwe ama mazingara yasiharibike lakini wapewe haki zao.

Haki za kufanya kazi, mzee sijui Chairman unafanya kazi gani wewe hebu tuambie, kazi yako ni ipi? Kazi yako ile unajitafutie riziki nayo ni ipi?

**Chairman:** Sina kazi.

**Com. Lethome:** Huna kazi kuna mwingine ambaye ni mfanyi biashara ama sivyo? Kama huyu bwana nafikiri ni mfanyi biashara wa hizi vyombo ama sivyo? Kuna mtu anayekulazimisha kufanya hiyo kazi bwana? Ama ni mapenzi yako, sasa mimi ninataka kuanzia leo ninakulazimisha uachane na mambo ya microphone hizi bwana wacha, utakubali? Huwezi kukubali ni haki ya binadamu kufanya kazi anayoichaguga mwenyewe, mmoja ni mwalimu, polisi, mkulima, mfanyi biashara wa mifugo bora tu isiwe ni kazi ambayo ni kinyume na sheria kama kusema na mimi kazi yangu ni kuvamia watu njiani, aha, hiyo sheria itakufuata itakushika. Lakini kazi nyingine yeyote tunasema ni haki yako kama mwanadamu kuchaguwa kazi unayoitaka mwenyewe ama ambayo itakufaa wewe haiwezi kukudhuru.

Haki ya kumiliki mali: Una haki ya kumiliki mali ni haki yako kama mwanadamu na hakuna mtu ambaye anaweza kukuzuia au kuchukuwa mali yako bila haki hata serikali. Kwa mfano, leo tuseme mimi ninakuja na gari ya GK bwana ninakuambia hizi mashini zako weka pale ndani naenda nazo kwa nguvu utakubali?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Itakuwa nimekwenda kinyume na sheria bwana hata kama ni GK lakini nichukuwe kwa sheria. Serikali inataka kutengeneza barabara hapa na lazima ipitie hapa hapa kwenye hii hoteli hapa hapa, ina haki ya kubomoa hiyo hoteli? Ikiwa ni lazima barabara ipitie hapa, mwenye hoteli alipwe ama sivyo? Kwa hivyo ni haki ya kila mwananchi kumiliki mali mahala popote na mali yake ihifadhiwe na serikali kwa sheria na kama itachukuliwa kwa nguvu ni serikali kwa sababu ya mahitaji ya umma kujenga skuli, kujenga hospitali basi alipwe kiasi ambacho ni sawa na gharama aliyoingia pale asipate hasara yeyote.

Hizo ndiyo haki mbali na haki za kimsingi haki zingine ni haki ya wafanyikazi, utakuta sehemu nyingi wafanyikazi wananyanyaswa sana, kwa sababu mfani kazi mara nyingi ni maskini mwenye kazi yule tajiri mara nyingi ni tajiri. Anawaajiri watu mshahara anayowapa si ya kibinadamu, nyumba anayowapa wafanyikazi waishi ndani yake haifai kabisa. Kazi anavyo wafanyisha kazi labda punda ndiyo hufanya kazi hivyo, kwa hivyo tumesema sheria lazima ihifadhi haki za wafanyi kazi na wengi wetu ni wafanyikazi.

Social security: kuna wakati ambapo mtu hajiwezi, hawezi hata kujilisha hawezi kulisha jamii yake kwa sababu ya maradhi pengine au uzee au sababu nyingine yeyote pengine kumekuwa na ukame. Nyinyi hapa ni wakulima ama sivyo?

**Audience:** Ndio

**Com. Lethome:** Si kuna wakati huwa kuna ukame hata hakuna mavuno yeyote, watu wana njaa hakuna mahali pa kulisha mifugo, tunasema wakati kama huo ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa kuna kitu kinaitwa social security, kuwa wasiojiweza wanaangaliwa na serikali. Health, matibabu: hapa mtu akiuguwa saa hizi, nikiuguwa saa hizi hapa mtanipeleka wapi? Wapi?

**Audience:** Health Centre.

**Com. Lethome:** Hapa hapa karibu, mna bahati nyinyi. Kuna wengine mtu akiuguwa pengine asafirishwe kilometer arobaini afikie hospitali, pengine unasikia mama mja mzito alikuwa akijifungua, amejifungulia juu ya mgongo wa ngamia au mgongo wa punda, mtoto amekufa ama na yeye amekufa huko. Kwa sababu, hapati matibabu, sehemu nyingine bila shilingi hata kama unakufia hapo nje ama sivyo?

**Audience:** Ndivyo.

**Com. Lethome:** Huwezi kuingia mpaka ulipe, tumesema ni haki ya kila Mkenya kila mwananchi kwa sababu ni mwanadamu apewe matibabu ya kutosha. Na wakati wa dharura wakati wa emergency, isiwe ukosefu wa pesa ni sababu ya yule mtu kunyimwa matibabu. Elimu kama nilivyotangulia kusema tulipozungumzia habari za haki za mtoto, kila Mkenya ana haki ya elimu ya msingi, kila mtoto ana haki ya elimu ya msingi na serikali ihakikishe kuwa, elimu zingine kama za secondary na university zinapatikana kwa urahisi.

Makazi: mwanadamu haishi kwenye mti ama kwenye shimo, serikali ihakikishe kila mwanadamu ana makazi yanayofaa, chakula kinachokubalika. Serikali ihakikishe hakuna mtu anayekufa kwa njaa ni jukumu la serikali kuhakikisha. Na chakula chenyewe kiwe ni cha kukubalika, kwa mfano, kuna baadhi ya vyakula ambavyo ni vyakula sehemu fulani lakini sehemu nyingine si vyakula kwa sababu ya mila au dini. Kwa mfano, kuna chakula fulani ambao watu wa hapa hawawezi kula, wa Malakote hawawezi kula wanasema hii hawawezi kula mila yao imezuia. Kuna kitu ambacho hawali? Mzee kama nguruwe kwa mfano Malakote ana njaa halafu serikali ilete nyama za nguruwe chukuweni chakula, hicho ni chakula kwao ama kwa Muislamu sio chakula. Mchina anakula pengine chura, akipelekewa chura ni chakula kwake wewe ukiletewa chura ni chakula kwako?

**Audience:** La.

**Com. Lethome:** Si chakula ni najis kwa hivyo, chakula chenye kukubalika, maji pia ni haki ya msingi, usafi pia ama mazingara ambayo yanazingatia usafi na afya ya mwanadamu iangaliwe.

Haki za wenye kutumia bidhaa zinazotengenezwa kwa mfano, hii soda ni bidhaa ambayo imetengenezwa na kampuni ya Coca

Cola, sheria lazima inilinde mimi kama mtumiaji wa hii sprite isiwe ni yenye kunidhuru na wasije wakaitangaza bidhaa hii kwa njia ya kunihadaa mimi. Nihadaike na ile bidhaa na kumbe sivyo ilivyo kwa mfano, wavutaji wa sigara, ukiangalia kwenye TV ama kwenye magazetti inapotangazwa inatangazwaje kwanza, kuna mahali inatangazwa kuwa sigara inakudhuru? Inaonyesha kuwa ukiwa kijana ukivuta sigara utakuwa na nguvu sana utakuwa na mbio kama farasi ama sivyo ndivyo inavyotangazwa?

**Audience:** Ndivyo.

**Com. Lethome:** Ama utakuwa kijana mwenye sura nzuri sana ukipita mahali wote wanakufuata ama sivyo? Katika kawaida ni kweli ukivuta sigara inatokea mambo hayo?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Inatokea kinyume na hayo, utakuwa na harufu mbaya ingine unakuwa na kifua unakohoa huwezi kukimbia ama sivyo? Kwenye pakiti ya sigara unaandikiwa maandishi makubwa sana Sportsman king size filter ama sivyo umeandikiwa? Halafu kando kidogo imeandikwa kidogo 'Ciggarette smoking is harmful to your health' hata watu wengine huwa hawaoni hiyo kwa sababu ni ndogo. Kwa hivyo, tumesema wenye kutumia bidhaa lazima wahifadhiwe, hizo zisiwadhuru wala zisitangazwe kwa njia ambayo inamhadaa yule mwenye kutumia unafahamu hivyo? kina mama ukijipaka mafuta aina fulani uso wako utakuwaje? Mweupe itakuwa hakuna pimples na nini maskini kina mama wengine wanakwenda ananunua cream fulani akija akijipaka unamuona madoa doa kama chui ama sivyo? Mwingine anataka nywele iwe ndefu sana anaambiwa kuna mafuta aina fulani ukijipaka nywele zako zitakuwa hivi na hivi mzee atakupenda sana, masikini ya Mungu anakwenda kujipaka nywele zinamwagika anabaki kipara ama hamjaona mambo kama haya yanatokea bwana? Tunasema yule consumer mwenye kutumia bidhaa kama ile lazima ahifadhiwe.

Fair administration: Mambo ya utawala lazima uwe ni utawala ambao unaangalia kila mtu. Kutii amri ambayo ni kinyume cha sheria, wazee waliniambia zamani mtu alipokuwa anafanya kazi katika jeshi, mkubwa wako akikuambia shoot piga risasi hata kama ni mama yako unaambiwa ufanye nini kwanza, piga risasi halafu baadaye unauliza afande kwa nini nimepiga risasi ama sivyo amri ya zamani hiyo? Kwa sababu mkubwa amesema imekuwa ni amri, iwe ni sawa ama si sawa unatekeleza kwanza halafu unauliza baadaye. Mkubwa amesema, sasa chini ya sheria mpya tumesema, ikiwa mkubwa amesema ndio ni mkubwa lakini amesema kinyume na sheria anavunja sheria huna jukumu la kufuata amri ambao ni kinyume na sheria na kwanza katika sheria ya Kiislamu unaambiwa, *'Laa atwaa atta li makhlukin fi maasiyatin khaliq'*, ama sivyo? Huwezi kumtii mwanadamu katika kumuasi Mwenyezi Mungu, huwezi kumtii mkubwa wako katika kuvunja sheria ndivyo tulivyoambiwa hapa.

Ni haki yako kama mwanadamu, usipelekwe tu kama kondoo, fanya fanya wakati mwingine unauliza lakini afande hapa ni sawa kweli, si ninaona sheria mahali fulani inasema hivi na hivi, una haki hiyo na huwezi kuadhibiwa. Lakini msiende kugombana na wakubwa zenu bwana mtafutwa kazi eh jihadhari.

Kufikia mahakama hapa kwanza mtu akitaka kwenda kortini ukiwa hapa Bura korti iliyo karibu iko wapi? Wapi?

**Audience:** Hola.

**Com. Lethome:** Hola kilometer ngapi kutoka hapa?

**Audience:** Hamsini.

**Com. Lethome:** Hamsini, ni kila mtu ambaye anafika kortini huko?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Wallahi mimi ninajuwa kuna baadhi ya wenu mmekaa hapa wakati mwingine umedhulumiwa ama kuna haki fulani unataka kufuata ukifikiria hiyo habari ya kwenda kortini na gharama na siku ambazo itapotea, unasema potelea mbali ama sivyo? Najuwa kuna watu hapa wamekaa, wameachilia tu wamesema ah itachelewa sana, itatupiliwa mbali, nitapoteza, sina pesa za kufika huko, sina pesa za wakili si ndiyo? imekuwa korti ziko mbali sana na wananchi na hata ikiwa karibu korti zimejengwa kwa njia ya kikoloni sana, sisemi yaani kuhusu ile mjengo lakini utaratibu utaratibu unaotumiwa katika korti hata juzi nilikuwa ninatoa mfano ninasema, utamuona mzee kama huyu bwana hapa saa hizi ukimpa hii microphone azungumzie watu hapa, atazungumza vizuri bila wasi wasi, mpeleke kortini akawekwe kizimbani pale ndiyo utaona. Unaona mzee ashaanza kutetemeka au hamjaona hivyo? Anashindwa hata kuzungumza maneno aliyokuwa nayo kichwani yanapotea yote, kwa nini? Kwa nini?

**Audience:** Wasi wasi.

**Com. Lethome:** Wasi wasi ushamuingia pale sijui nitahukumiwa, nitafungwa, nifanya makosa kwa hivyo, kwanza ukimwambia mtu bwana nataka uje uwe shahidi katika kesi yangu, watu wengi hukubali? Kortini mimi aah hapana usiniletee mimi taabu, tunataka korti iwe ni korti ambayo wananchi wanapenda na wanaweza kupata haki zao kwa urahisi na ziwe karibu na watu. Na mambo ya kucheleweshwa kesi pia muda mrefu, hiyo ni kunyume na haki za binaadamu, utakuta mtu kesi pengina shamba tu au ya mali yake tu. Miezi sita miezi saba au pengine mtu umekwenda umeshtakiwa unatuhumiwa kuwa wewe ulifanya kosa fulani ukienda kortini unatakiwa useme ndio au la. Ukisema ndio utahukumiwa, ukisema la unafanywaje?

**Audience:** Unarudishwa rumande.

**Com. Lethome:** Rudisha rumande huyo mpaka mwezi ujao ama sivyo? Utakuta masikini watu wengi hajafanya jambo lakini kwa kuogopa kwenda huko rumande kwa sababu ni jahanam hiyo nyingine, unasema ndio afande nilipatikana na msokoto wa bangi ama sivyo? Unahukumiwa, nidhamu tunayofuata si ndio mzee, kuna mzee amekubali kabisa. Kwa hivyo tunataka pia mahakama zetu zinazofanya kazi ziweze kuangalia maslaha ya yule mwanadamu. Watu wenye kushikwa wana haki za kibinadamu ama hawana haki?

**Audience:** Wana haki.

**Com. Lethome:** Leo hii hapa polisi kwa mfano wakikushika wewe unafanya makosa kwanza utafungwa kamba mikono yote

miwili nyuma hata pengine ni hatia ndogo tu uliyofanya, utashikwa hapa surwali unatembea mguu iko juu juu hivyo ama sivyo? Unapigwa hapa vibaya ukienda kufika pale police station ushavunjwa vunjwa hata meno ama sivyo?

**Audience:** Ndivyo.

**Com. Lethome:** Na wengine tunasimama tu, unaona yule mbona anampiga, ah ni polisi ni askari amemshika. Sasa akishamshika ndio ana haki ya kumpiga vile, haya unaingia hiyo cell, unaambiwa zungumza sasa sema, sheria inasema hapa una haki ya kunyamaza unaweza kusema sizungumzi mpaka nipelekwe kortini ndiyo nitazungumza.

**Speaker:** Na ukiwawa?

**Com. Lethome:** Huku kwetu chini ya sheria hii ndio utauawa, lakini chini ya sheria mpya mapendekezo tunayopendekeza ni kuwa mtu anaposhikwa pengine ametuhumiwa sheria inasema, a person is innocent until proved guilty, mtuhumiwa hana makosa mpaka yathibitishwe yale makosa wapi, kortini. Huku kwetu huwa ni kinyume, ukishikwa tu wewe ni mkosaji mpaka ithibitishwe kuwa wewe huna makosa ama sivyo? Ndiyo utaona mtu anakaa rumandi mwiezi sita ama zaidi. Anapigwa huku na mateso mengi, anapelekwa kortini amepatikana hana hatia, miezi sita ya maisha yake ama mwaka ushapotea hata zaidi ya mwaka. Ashapigwa hakuna mtu ambaye atakayemlipa kipigo alichopigwa, vunjwa vunjwa meno, mikono alikuwa anaweza kufanya kazi akitoka kule hata kazi hawezi kufanya, vijana wamefinywa finywa si ndiyo unafinywa ukipelekwa huko mpaka uzungumze useme. Haya yote tumesema ni kinyume cha haki ya binadamu au torture ile watu wanaambiwa ili uweze kusema kwa sababu, unaambiwa hebu sema mliiba ama hamkuiba? Unasema afande hatukuiba, unaambiwa wewe ngoja utazungumza na ni kweli utazungumza, utafinywa mpaka mwanaume mtu mzima unalia unaita mama ama sivyo?

**Audience:** Ndio

**Com. Lethome:** Mpaka makosa ambao haukufanya unasema uliyafanya. Kwa hivyo, haya yote tunasema yapigwe marufuku, kila mahali tulipokwenda watu wamelalamika sana kuhusu unyanyasaji wanaofanyiwa hasa wakishikwa. Hatusema mtu asishikwe, mtu ashikwe akienda kinyume na sheria, lakini asivunjiwe haki zake za binadamu kwa mfano, Sheikh wewe ukishashikwa, ndiyo maana imekuwa wewe si Muislamu tena, ukiwa cell hauna haki ya kuswali Sheikh, una haki ya kuswali ama hauna haki ya kuswali? Cell ilivyo hivi sasa unaweza kuswali huko kwenye cell?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Huwezi, kwa hivyo inatakiwa hata kama uko cell una haki zako zote za kibinadamu, zile haki zako ziweze kuangaliwa na ukidhulumiwa kule ndani uwe na mahali unaweza kuenda kulalamika. Afande nimedhulumiwa, ukiwa mgonjwa watu wangapi wanakufa kwenye cell si ni wengi sana? Jela wanakufa kwa sababu hawaangaliwi tumesema ni kinyume na haki za kibinadamu.

Kesi pia zisiwe ni zenye kucheleweshwa na wale ambao hawawezi kujimudu kupata uakilishi wa mawakili, serikali iweze kuwasimamia pia kwa sababu, pesa hizo zinazotumiwa na serikali, serikali inatoa wapi pesa? Kwetu sisi, sisi ndio tunawalipa

kodi, unapoingia dukani kununua kilo ya sukari unalipa kodi kuna pesa za serikali. Unapotia gari yako petroli, unaponunua kikoi, unaponunua shati, kuna pesa ambazo unalipa serikali kwa hivyo, tunasema mtu ambaye hajiwezi hajimudu katika mambo ya kesi aweze kusimamiwa.

Haki za wafungwa waliyofungwa pia iweze kuangalia, wawekwe katika mazingara ambayo ni ya kibinadamu, sijaingia huko na Mwenyezi Mungu asikubali, sitaki kuingia, lakini nasikia wanavyolala huko sikuzuri sana ama kuna mtu anayejuwa huko ndani kuko vipi? Lakini sote tunasikia mavazi wanayoyavaa si mavasi mazuri, nasikia wanalala kwenye simiti, wanafanyishwa kazi kama wanyama, ni binadamu. Tumesema pia mtu akifungwa chini ya sheria mpya imependekezwa kuwa mtu kama huyo ana haki ya kudhuriwa na watu wake, kama ni mwanaume ambaye alikuwa ameoa ana haki ya kudhuriwa na mkewe jela, kuweko utaratibu fulani waweze kukutana. Kama ni mama ambaye ameolewa, kuweko utaratibu aweze kukutana na mumewe na watoto wake na familia na kiongozi wake wa kidini kama ni Sheikh wake anataka kuja kusikia mawaidha ya kidini apewe mawaidha kwa sababu tumesema jela si mahali pa adhabu, jela ni mahali pa kubadilishwa mtu tabia. Na ndiyo sababu, katika chini ya sheria mpya, tumeondoa neno Prison jela limeondolewa, neno ambalo tumetumia hapa na ndilo linalotumiwa katika nchi nyingi ni, correctional services, mahali pa kubadilisha tabia.

Leo hii mtu anashikwa pengine alikuwa ni mwizi wa kuku, akiwekwa huko ndani akitoka utasikia ameiba mbuzi amerudi ndani, akikaa kaa utasikia amekuwa mwizi wa ngombe siku hizi huyu. Inakuwa ni kama kule huenda anaenda kufundisha kuwa mwizi zaidi amekuwa hard core. Hapa pawe ni mahali pa watu kurekebishwa tabia zao, correctional services na mtu akitoka jela pia ile stigma, mnaanza kusema yule bwana, unamuona yule ametoka juzi prison yule kuna mtu ambaye anataka kushirikiana na mtu ametoka prison kweli? Ah yule bwana usishirikiane naye ametoka x-prison yule, ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Imekuwa na stigma pia, na yeye kwa sababu anaitwa x-prison anaamua sasa psychologically wacha niwaonyeshe mimi ni x-prison. Kwa hivyo tumesema hiyo iondolewe sasa iwe ni correctional services, tutasema yule ametoka katika kituo cha kubadilisha tabia, tunatarajia amebadilishwa tabia, ndio maana pia askari jela mafunzo yao pia yabadilishwe wapate mafunzo ya kutosha kuweza kuwabadilisha wale wanaofungwa kule tabia zao.

Sasa hizo ndiyo baadhi ya haki ambazo tumesema mwanadamu anapewa kwa sababu ni mwanadamu chini ya sheria, ni nyingi lakini mtajisomea zingine wakati hauruhusu niangalie kila haki. Lakini kuna kitu ambacho tunapozungumzia habari ya hizi haki zote, lazima tuwakumbushe na tumekiandika hapa katika sheria, hakuna haki ambayo haina mipaka. Hakuna haki isiyokuwa na nini? Mipaka. Hata haki alizotupa Mwenyezi Mungu zina mipaka yake ama hazina mipaka?

**Audience:** Zinazo

**Com. Lethome:** Kwa mfano Mwenyezi Mungu ametukubalia uhuru sisi binadamu '*kullu washrabu'* ama sivvyo? Lakini ametuwekea mpaka akatuambia *'wala tushrifu'*. Kuleni na munywe lakini msifanye israfu, hiyo ni mpaka ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa umepewa haki zako zote hapa, una haki ya kuishi, haki ya kumiliki mali, haki ya kutembea kila mahali, haki ya kuabudu unavyotaka lakini umeambiwa usipite mipaka. Kila haki ina mipaka ukipita tu ile mipaka haki yako itachukuliwa na sheria, kwa mfano, haki ya kumiliki mali lakini usimiliki mali ya haramu, ukimiliki mali ya haramu serikali itakuchukulia hatua.

Haki ya kwenda kila mahali unapotaka, lakini usiende ukafanya uhalifu ukienda kufanya uhalifu utashikwa. Una uhuru wewe mtu yeyote asiingilie uhuru wako, uhuru wako utaingiliwa ukivunja sheria, kila haki ina mipaka. Tumia haki yako ya dini lakini usiwe wewe sasa unanizuia na mimi kufuata dini yangu au unazuia mpaka mtu aliyelala mgonjwa asiweze kutulia kupumzika la. Haki yako isivuke mpaka, kwa mfano Sheikh ukiwa Msikitini unasoma Qur'an halafu akaingia mtu anataka kuswali sunna pale, sheria inakuambia nini?

**Audience:** Punguza sauti yako.

**Com. Lethome:** Upunguze sauti yako ama sivyo kijana? Haki yako ya kusoma Qur'an msikitini ya kutafuta dhawabu isimuahiribie yule naye haki yake kutafuta dhawabu kwa kusali kwa *kushuu*, si tunaambiwa tuswali kwa *kushuu*. Sasa angalia hata mambo ya dini pia ina mipaka yake na ndiyo unaambiwa katika Qur'ani '*watilka huddudhu Llah'* na hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu, *fala ta'atadduha*, usikeuka mipaka ya Mwenyezi Mungu, ama hatukuambiwa hivyo katika Qur'ani?

**Audience:** Tumeambiwa.

**Com. Lethome:** Pia katika sheria ya nchi pia kuna mipaka. Tumia haki yako zote hizi ulizopewa kama mwanadamu lakini usivuke mipaka ndiyo unaona kuna sheria za nchi. Mimi nina haki ya kuendesha gari barabarani ama sivyo? Sasa nina haki niendeshe gari yangu katikati ya barabara wengine wasipite? Ama mimi nisema tunaambiwa keep left mimi nina haki nitaendeshea right itawezekana? Nitapata accident ama mimi niseme na mimi nitatumia haki yangu mimi nitaendesha across hivi, gari yangu ninaishimamisha hivi si barabara inaenda hivi, mimi ninaendesha hivi itawezekana? Lazima kuwe na nidhamu kwa hivyo haki zina mipaka.

Jambo lingine, utekelezaji wa hizi haki zitakuwa hazina faida ikiwa hauwezi kulazimishwa wewe kupewa haki yako kwa mfano, tumesema ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa kila mmoja anapata maji, chakula na makazi na elimu ya watoto ina maana kuwa hiyo haki haina faida yeyote ikiwa hatuwezi kulazimisha serikali kufanya hivyo na ndiyo maana hapa tumesema kuna njia mbili za kulazimisha serikali, au mtu yeyote ambaye ana jukumu la kuhakikisha kuwa unapata haki yako kama raia, kwanza ni korti unaweza kwenda kortini kuilazimisha serikali au kumlazimisha mtu yeyote akupe haki zako za kimsingi.

Pili kuna tume ambayo tumeiunda hapa tumeiita Human rights and administration Justice commission. Kuna commission ambaye tume ya kusimamia haki za binadamu na pia uadilifu katika idara, katika serikali. Tumeiunda tume hiyo ama

tumependekeza tume hiyo iwe katika katiba ili iweze kusimamia maswala ya haki, unaweza kulazimisha hizo haki zake kupitia kwa tume kama hiyo. Nitatulia kidogo hapa kwa sasa nawapa dakika tano hivi kama kuna mtu ana swali kuhusu haya niliyo yazungumzia hadi sasa, uliza swali lako, nitalijibu kama kuna sehemu ambayo huku fahamu na mimi nipumue kidogo halafu tuendelee na sehemu zingine kuhusu mambo ya uakilishi na mambo ya Bunge. Mambo ya kupiga kura, uakilishi wa Bunge, halafu tutaingia katika mambo ya Executive, Rais, Prime Minister na nani? Na kisha mambo ya kortini, swali lolote?

**Abubakar:** Mimi ninaitwa Abubakar na ninataka kuulizia hapa katiba imesema kutakuweko na elimu ya lazima ya msingi, hii katiba itahakikisha vipi hiyo elimu itafikia watoto wote? Especially katika sehemu hii yetu unaweza kuona ambao wanaenda shule ni chini ya asili mia moja kwa hivyo tungetaka kujuwa kama hii katiba mpya imezungumzia tu au kuna vipengele fulani inaotumia ili kuhakikisha ya kwamba hayo yaliyozungumziwa kuwa inaweza kufanywa? Sijui kama ninaweza kendelea kuuliza maswali mengine ama?

**Com. Lethome**: Haya sawa hilo la kwanza.

**Abubakar**: Swali lingine kulingana na mpangilio ya Katiba ya Kenya nimeona ya kwamba constitution of Kenya imetokea kabla pengine customary law na sheria ya dini ya Kiislamu iko number ya tatu katika hiyo mpangilio, kwa hivyo inamaanisha ya kwamba kama constitution ya Kenya ndiyo the supreme law in the land. Ina maanisha ya kwamba hii sheria ya Kiislamu imekuwa superceded na customary law, yaani vile ninavyosema ina maanisha kwamba mila za waafrika au customs za kiafrika iko na maana zaidi kuliko dini ya Kiislamu?

Swali lingine ambalo ninauliza ni kwamba, katika basic rights ile mahitaji ya mwanadamu wa kawaida kuna habari ya maji, katika sehemu hii yetu, hivi sasa isipokuwa pengine ni hii mvua, watu hawanyi maji kabisa wacha habari ya kuzungumza pengine watu na wanyama wanapigania maji kama ilivyotokea huko Takaba, hapa hata hiyo maji ya kupigania pamoja na wanyama hakuna. Ninataka kujuwa hii katiba imezungumzia kwamba watu watapewa hiyo maji safi lakini kisije tu kama ni maandiko yaliyoandikwa kwamba hayo maji safi yatakuweko, lakini huku kwetu tunataka kuhakikishiwa hii katiba mpya itafanyeji ili kuhakikisha kwamba hayo maji safi itapitakanwa?

Swali lingine ni kuhusiana na consumer rights, haki ya wateja au haki ya wale wateja ambao wanatumia bidhaa, tunataka kujuwa katika sehemu kama hii inasema katika hiyo kifungo ya sheria ilikuwa inasema, mtu anaweza kuwakilisha malalamiko lake kwa High Court, lakini hapa korti ambayo iko karibu na sisi iko kilometer hamsini, mimi pengine nimenunua kitu ya shillingi mbili ambayo nilipoitumia hiyo kitu, ili expire wakati wake, nitafanyaje ili kwenda huko? Hiyo itakuwa ni ghali kuliko hata hiyo kitu niliyotumia kwa hivyo, hiyo consumer rights hapo katika hii consumer rights au haki ya wateja, ninaona hii sheria hailingamani na ukweli ambao unatendeka katika nchi hii yetu.

Nafikiri zingine bado hujazungumzia kwa hivyo nitasimama hapa isipokuwa kuna kitu nataka kueleza, katika profile ya Bura ambayo tuliona mlisema kwamba katika eneo hii wa Pokomo ndiyo wengi, hii eneo hii sidhani kama kuna Mpokomo anaishi

hapa isipokuwa pengine awe ni mfanyikazi. Na kitu kingine ambayo imetokea ni kwamba kuna NGO ambayo walifanya civic education katika sehemu hii, na hiyo civic education inaonyesha katika Bura profile imefanywa na NGO ya Wajir, na tofauti ya Bura Constituency na Wajir ni kubwa hata ki mikoa kwa hivyo tunashindwa ni vipi hawa watu wanaendelea kusema kwamba, katika Bura constituency economic activity kubwa ni fishing au ukulima ile ya kulima yaani crop farming. Kwa hivyo, tunashangaa kwamba hata kama nyinyi wenyewe mlipotoka Garissa mpaka kupita hapa ama popote mlipotoka katika hii wilaya, huwezi kuona economic activity ya hii area ni ufugaji, livestock farming kwa hivyo, tunashangaa kama Commisioners au nyinyi mnaweza kuandika report ambazo inaonekana na macho ambazo haziridhishi, itakuaje kwamba maoni yetu inaweza kupokelewa vyema? Asanteni kwa sasa.

**Com. Lethome:** Nafikiri ngoja nimjibu huyu bwana halafu tutakujibu wewe. Kwa sasa bwana Abubakar nashukuru kwa haya maswali yako yote na hili la mwisho kuhusu profile na information ambayo si sawa, we have noted that, it will be corrected sio lengo letu kabisa kuja kutoa information ambayo si sawa. Sio lengo lengo kabisa na it has been noted na ndiyo sababu tumekuja tuweze kusikia yale ambayo pengine mnaona tumekwenda kinyume na vile ambavyo ni sawa. Kwa hivyo, tunashukuru sana kwa hayo ambayo ulituambia na tutahakikisha kuwa profile ya Bura itakuwa ni ya kisawa sawa, inaeleza Bura vile kulivyo.

Kuhusu maswali ambayo uliyauliza, swali lako la kwanza ni kuhusu constitution kuwa ndiyo the supreme law halafu utaratibu uliyowekwa ni kuwa African customary law imetangulizwa mbele ya Islamic sheria. Kwanza ningependa kukueleza ikiwa katika nchi kama hii ambayo sio nchi ya Kiislamu, hata kuna kipengele hapa ambapo kinasema kuwa, hakuna state religion, hakuna dini ya kitaifa kinyume na vile kwa mfano, ukienda nchi kama Saudi Arabia, utaambiwa the state religion ni Islam, nchi ya taifa ni Uislamu ama ukienda mahali kama Vatican utakuta dini ya kitaifa inayotambulikana kitaifa ni kirasmi ni dini ya Kikatoliki. Hapa Kenya tunasema hakuna state religion, hakuna dini ya taifa lakini hata hivyo tumeambiwa kuna sources, asili ya sheria, sheria zitakazotumika katika nchi ya Kenya, tumeambiwa ni zifuatazo:

Ya kwanza ni katiba, katiba ya nchi ndiyo itakuwa source ya kwanza au asili ya kwanza ya sheria. Halafu Act of Parliament, sheria ambazo zinabuniwa na Bunge, halafu African customary law, mila za kiafrika halafu Islamic and Hindu personal law, sheria za Kiislamu na za Hindi kuhusu masala ya familia. '*Al akhwali shaqshiya'* wale ambao wanajuwa kuhusu mambo yale ya ndoa, mambo ya uridhi na mambo ya nikah na mengine yanayohusiana na familia.

Kisha baada ya hapo sheria zinginezo, lakini hapa huwezi kusema kuwa kuna sheria ambayo hapa iko juu ya katiba, katika nchi kama Kenya ambayo haitawaliwi na sheria ya Kiislamu, Katiba ndiyo sheria ya juu. Zilizofuata zote hapo hakuna ambayo unaweza kusema hii iko juu ya nyingine, it is only the constitution that is the supreme law in the land. All the others must follow the constitution, kwa hivyo hazikufuata in order hiyo, hakuna order yeyote ambayo imefuatwa hapa. Order ni ile ya katiba peke yake, katiba ndiyo ya msingi na ndiyo hapa zimetajwa tu kuonyesha kuwa katiba inatambuwa hizi sheria.

Katiba inatambuwa kuwa kuna mila za kiafrika, kuna sheria za Kiislamu na sheria za Bunge lakini hakuna kusema kuwa kuna sheria hapa ambayo zingine zote ziko chini yake isipokuwa katiba peke yake. Kwa hivyo the order followed here does not mean that the all the ones that follow are subordinate to the ones that are above them, tumefahamikiana bwana Abubakar?
**Abubakar:** Kabisa, kabisa.

**Com. Lethome:** Na ndiyo sababu hii kwa mfano, leo Bunge ikipitisha sheria, si hapa Bunge tumesema ni number two, Bunge imepitisha sheria hapa ambayo imevunja korti za kadhi Kenya, tutakubaliana nayo?
**Audience:** Hatuwezi.

**Com. Lethome:** Hatuwezi kukubaliana naye kwa sababu hapa watakuwa wametuvunjia haki zetu ambayo tumepewa na katiba ambayo ndiyo sheria kuu au tuseme mila ya kiafrika inasema, mimi ninapokwenda kuoa kama Masaai lazima nipeleke mtungi wa pombe ya busaa, sasa hapa nitafuata sheria yangu ya dini ama nitafuata sheria ya mila?
**Audience:** Ya dini.

**Com. Lethome:** Nitafuata sheria ya dini hapa. Kwa hivyo, utaratibu uliopangwa hapa sio wa kuonyesha sheria ambayo ni lazima ifuatwe na ile ambayo iko chini yake isipokuwa katiba peke yake.

Kuhusu basic rights, mambo ya maji ni kweli ndugu yangu Abubakar ukiangalia hata katika hii katiba ambayo tunaibadilisha hivi sasa, kuna haki nyingi ambazo tumepewa lakini mpaka sasa hazijapatikana. Unakuta ni wino tu ulioandikwa kwenye karatasi, sheria imeandikwa imewekwa haikutekelezwa ama sivyo?
**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Na hakuna mahali unaweza kuenda kulalamika, ukichunguza pengine katika development plan ya huu mji wa Bura kuna plan ya mabarabara ama sivyo? Unambiwa hapa panafaa kuwa na barabara, ukijenga hapa uweke barabara, kunafaa kuwa na uwanja fulani, hapa kunafaa kuwe na kitu fulani, hivyo vitu vipi mpaka sasa? Hakuna, havikutekelezwa ni kwa sababu sheria hii haikutoa wakati wa kusema, ikifikia wakati fulani jambo hili liwe limetekelezwa sasa tunapendekeza mabadiliko tunasema, haki hizi za msingi ziwe kila mmoja apate hizi haki za msingi. Mnajuwa sisi kwa mfano, kama commission, tukishamaliza kazi ya tume hii, ikishapitishwa na Bunge basi, tushamaliza kazi yetu. Ifuatwe isifuatwe itakuwa sio jukumu letu, sasa ndiyo tukasema katiba yenyewe lazima iweke vipengele vya kulazimisha yale yaliyopendekezwa yafuatwe ikifikia muda fulani na ndiyo ukisoma utaona kuwa baada kila sehemu tumesema, ikifikia mwaka mmoja, au ikifikia miaka miwili jambo hili liwe limefanyika na huku mwisho tukasema mwananchi ana haki ya kuenda kortini ama kuenda katika tume kulalamika ikiwa kuna jambo ambalo limetajwa katika katiba kama haki yake na hakupata.

Kwa hivyo tumetoa muda wa kutekelezwa na mimi ninawaambia mengi hapa yatategemea sisi msimamo wetu kuhusu sheria, ikiwa itakuzwa zitabaki tu pale tu kwenye makaratasi, hakuna kazi itafanyika. Itakuwa ni sheria nzuri lakini haifwatwi, kama vile

Qur'an nzuri maneno ya Mwenyezi Mungu lakini hayafuatwi kama vile ndiyo hivo. Lakini hapa tumetoa na tumetoa mpaka na adhabu ama hatua ya kuchukuliwa anayepewa mamlaka ya kutekelezwa akose kutekeleza kuna hatua imewekwa hapa ya kuchukuliwa. Kwa hivyo, hiyo tu ndiyo mechanism ambayo tumeweza kuweka ya kuhakikisha yale yaliyo katika Katiba yanafuatwa, lakini mengi yatategemea viongozi tutakao wachaguwa ni viongozi wa aina gani na wale tutakawapa mamlaka ya kutekeleza katiba hii ni watu aina gani? Kwa sababu ni mimi na wewe na viongozi tutakao wachaguwa ambao watatekeleza hii katiba hakuna mtu atakaye toka nje aje afanye hii kazi ni sisi wenyewe. Kwa hivyo Bunge tumeipa muda wa mwaka moja au miwili kutekeleza haya yote yaliyo hapa.

Mambo ya consumer rights ni kweli kama walivyosema, mimi nikiwa pengine nimekwenda kununua soda shilingi ishiri halafu nimekuta kuwa ina kitu cha kunidhuru mimi, siwezi kupoteza shilingi zingine mia mbili na kuenda Hola kutafuta korti. Lakini ninakumbuka tulipozungumzia habari ya haki za korti, mwananchi kupitia korti nafikiri nilitaja nikasema kuwa, nilipouliza korti iliyo karibu iko wapi, mliniambia ni Hila. Nikasema chini ya sheria mpya, ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa korti ziko karibu na watu ama sikusema hivyo?

**Audience:** Ulisema hivyo.

**Com. Lethome:** Nilisema hivyo, kwa hivyo chini ya sheria mpya hiyo mambo ya korti kuwa mbali ama huduma zingine zozote za muhimu kuwa mbali na wananchi nataka Bunge lihakikishe kuwa huduma kama hizo zimeletwa karibu kwa sababu, haki nyingi tunazipoteza kwa sababu ya kufikiria gharama za kufikia huduma hiyo na ndiyo maana nikawaambia ninajuwa kuna watu hapa, wana haki zao za kisheria lakini wamesema akifikiria habari ya kufika kortini Hola na wakati atakaopoteza na gharama, anasema potelea mbali ama sivyo? Tulitaja hizo.

Nafikiri hili lingine kuhusu profile nimezungumzia juu yake tuchukulie hatua gani, nafikiri maswali yako yalikuwa ni hayo tu Abubakar? Kuna mwenzako huko ana swali?

**Ali Wario**: Asante ndungu yangu. Kwanza tukiwa wakenya.

**Com. Lethome**: Jina lako?

**Ali Wario:** Jina langu ni Ali Wario tukiwa wakenya hapa tulipo tuna wasi wasi, moja ya hiyo wasi wasi ni kwamba shilingi bilioni mbili pesa ya umma zilitumika kupata katiba tulionayo sasa ingawa ni draft hii si katiba, nataka tume itupe dhibitisho kwamba hii itakuja kupitishwa kwa sababu hivi tuna wasi wasi nasikia Moi hataki, nani hataki, sisi mwananchi tunataka hii kitu na tunapotaka iwapo leo fursa iko na Moi, kesho asubuhi aseme hii ni haramu, tutafanya vipi? Moja ni hii.

Pili ndungu licha ya mimi kupenda hii kazi na kuwapongeza kwa juhudi yenu, pia nina shaka moja, life style of the people living in this area mtindo wa maisha ya watu wanaoishi sehemu hii katiba ni muhimu itambuwe. Angalia hii ukurasa vile ilivyo kubwa katika hii document yote hii kubwa haikuguzwa mfugaji na mifugo hakuna, as big as it is, neno kwa neno. Hii ni sikitiko kubwa

kwa sababu miaka arobaini iliyopita sisi tumegandamizwa, tumenyanyaswa na kuteswa, leo tunafikiri katiba hii itakuja kututetea na katiba hii there is no one word pastoralist in it, there is no livestock in it. Tegemeo letu sisi ni nini kama wewe hujatuwekea mfugaji hapa, wewe hukutuwekea mifugo hapa, unatuambia katika District list umeweka wizara zote ile unayotaka kuzitaja lakini mifugo hukutaja, ati Kenyans milioni saba wanategemea mifugo seven million Kenyans depend entirely on livestock and livestock produce.

What is the way forward katiba hii inakwenda mfugaji hakukuzwa, mwelekeo wetu, tamaa yetu katika katiba mpya ni nini? Policy planners wengi wametu-fail umesikia watu kuuwana Tana River kwa nini wameuwana? Kwa sababu katiba tulizo nazo ni chongo ni bubu, ni kiziwi haizungumzi juu ya umiliki ya ardhi ya mfugaji. Katiba inazungumza mkulima, mfugaji hana chake katika katiba tulizo nazo, iwapo wewe leo hutoweka wazi inatakikana upambanue kwamba ana haki ya kumiliki hiki na maisha yake ni haya. Leo ndungu yangu Abubakar ni vizuri ameona na akaiguzia draft, inatuambia majority ni wakulima si ukweli. Nataka mkosowe halafu ndungu yangu katika ile haki ya elimu mimi nimetoa memorandum yangu wakati Commissioners walikuja kuchukuwa maoni, mtindo ya elimu ambayo tuko nayo sasa is meant for people with permanent settlement. Wale watu watakao lazimika kukaa mjini, mfugaji elimu hii haimfai tunataka mtindo ya elimu sababu inasemekana kila mtoto apewe elimu ni sawa, apewe elimu, mtindo ile ya elimu itakayopewa ikubaliane na my lifestyle.

Nikienda mwisho kabisa, mwisho nikienda kugusia ndungu yangu sisi tuko katika hatari kubwa, leo tunataka kuzungumzia mambo ya katiba ambayo tunaipa nguvu zaidi, kuna na Mwenyezi Mungu pia neno moja imetuumiza sana sisi wakenya, kortini unamwita fulani lord halafu unasujudu, sasa ndungu yangu wewe Muislamu kafikirie, mimi nikuite wewe lord halafu nikusujudie wewe uislamu wangu upo?

**Audience:** Hakuna.

**Ali Wario:** Kwa hivyo tumetoa pendekezo hapa, tumesema ikiwa lazima mtu aitwe maulana waite wale wanaotaka kuwaita isiwe makosa juu ya Waislamu, mimi nisilazimishwe kusujudia Jaji, hii isiwe lazima katika sheria, iwe our independent thing. Mimi nitamuita mheshimiwa na hiyo ni heshima tosha, si lazima nimuite maulana, si lazima nimsujudie. Hii ni sikitiko kubwa halafu ninatoa pendekezo tafadhali ninamaliza, kwamba hii tume ya katiba au Bunge leo na hata siku zinazo kuja, isitunge sheria itakayovunja hukuma ya Qur'an kwa sababu ni hatari kubwa. Sababu outrightly unajuwa hatutakubaliana Mwenyezi Mungu keshatoa hukumu yake, ananiambia haki ya mwanamke ni nini katika uridhi, ya mwanaume ni nini, leo wewe ukikaa kortini uniambie enda ukampatie 50% haiwezekani, kwa hivyo, hukumu isitolewe hukumu ambaye itaenda kudhalilisha Qur'an kwa mujibu wa wale wana dini ya Kiislamu asante, haya mengine ukifika ndiyo tuko pamoja.

**Com. Lethome:** Haya inshaallah, asante sana bwana Ali kwa hayo mapendekezo yako na pia baadhi ya maoni ambayo umeongeza. Nafikiri sababu ya sisi kuja hapa nakutaka wananchi washiriki katika kuchambuwa mswada huu ni kama haya anayoyazungumzia bwana Ali. Nikuweza kujaza mapengo ambayo yako katika mswada huu na pengine kupunguza mengine ambapo tumepita mipaka ili tuweze kupata katiba mpya ambayo itakuwa imechukuwa maoni ya wananchi wote na pia

malalamishi ya wananchi, kwa hivyo, haya yote aliyozungumzia bwana Ali Wario ni mambo muhimu na yamenaswa na chombo chetu na ni mambo ambayo yatazingatiwa huko.

Kuhusu wasi wasi wake, ni wasi wasi ambao hata mimi niliyokaa hapa ninao kwa sababu, kusema kweli gharama nyingi zimetumika katika kazi hii, muda mrefu imetumika matumaini ya wakenya sasa ni kuwa yako juu sana wanatarajia kuwa na katiba mpya. Lakini sasa hayo aliyoyauliza bwana Ali ili tuweze kuondoa wasi wasi huo ni yako kwingine, hayako mikononi mwetu kama tume yako kwingine mikononi mwa wengine ambao chini ya sheria iliyoko hivi sasa ndiyo walio na uwezo sasa wa either kukubalia hii kazi ikamilike ama isikamilike ndungu yangu.

Sheria iliyobuni tume hii na ambayo iliweka mpangilio utaratibu wa kufanya hii kazi imesema hivi, baada ya sisi kukamilishi kazi hii tunayoifanya hivi sasa, kuzunguka na kuchukwua maoni zaidi ya wananchi na kuchambuwa mswada huu, kuwe na kongamano la kitaifa kuhusu katiba, National Constitutional Conference ambako wakenya zaidi ya mia sita karibu na thelathini watakutana kwa muda wa mwezi moja kutoka kila sehemu ya nchi, waweze kuchambua na kujadiliana yale watakayokubaliana nayo katika kongamano hilo ndiyo itakuwa sheria mpya ya nchi hii. Bunge itakuwa kazi yake ni kupitisha tu, sasa baina ya wakati huu na wakati huu wa kongamano lolote linaweza kutokea.

Chini ya katiba hii Rais wa nchi ana haki ya kuvunja wakati wowote atakao kulivunja Bunge, hata hivi tunazungumza na wewe pengine saa nane Bunge litavunjwa na atakaye livunja atakuwa anatumia sheria iliyoko hapa. Hii katiba imempa mtu mmoja binadamu mmoja haki ya kufanya hivyo, atakuwa anaitumia haki hiyo, Bunge likivunjwa kabla ya tarehe ishirini na nane siku ya kongamano, Kongamano halitafanyika kwa sababu karibu nusu ya wale wanaokuja katika hilo kongamani ni Wabunge, bila Bunge hakuna Wabunge, ina maana lazima tungoje mpaka uchaguzi ufanyike Bunge lingine liundwe mwaka ujao ili tuweze kufanya kongamano hili.

Kwa hivyo hilo sasa wasi wasi huo alionao Ali na mwingine mimi pia nina wasi wasi huo isipokuwa tu sasa ni kumuomba Mwenyezi Mungu kisha wale ambao wamepewa mamlaka haya ya kuvunja na kutovunja Bunge, wasikize kilio cha wananchi waweze kusubiri mpaka tufanye kazi hii. Hilo haliko mikononi mwetu na ndiyo unaona hivi sasa sisi tunaendelea kufanya kazi zetu hata tumepelekwa kortini tusimamishwe nafikiri mmesikia, hatuku simama amri ya kortini hatukuitii kwa sababu tulisema ni lazima tu endelee na kazi tumepewa mamlaka na Bunge na kwa niaba ya wananchi wa Kenya tuendelee na kazi na ndiyo tunaendelea mpaka hivi sasa.

Kuna order za kortini hivi sasa hata nyinyi hivi mlivyo hivi sasa ni kinyume cha sheria kulingana na akili zao walio kwenda kortini kwa sababu walisema, hakuna kujadiliana kuhusu mambo ya katiba, wakatoa order lakini tuliipuuza ile amri ya kortini kwa sababu, hata katika hii katiba tumesema hakuna ruhusa kutii amri ambaye ni kunyume na sheria. Tulipuuza kwa msingi huo, kwa hivyo wasi wasi huo tunao sote na ni wasi wasi ambao inatakiwa kila mwananchi aweze kuwa nao hivi sasa na muweze kuzungumza kama ni viongozi wenu Wabunge, mna Mbunge pia na yule Mbunge anaweza kumfikia Rais, amueleze kuwa

wananchi wa sehemu yangu wanasema bwana Bunge lisivunjwa mpaka kazi hii iweze kukamilika, hilo ndilo ninaloweza kusema kuhusu wasi wasi yako.

Kuhusu mambo ya livestock na pastoralist, watu ambao hufanya kazi ya kufuga mifugo na watu wenye kuhama hama. Ni kweli kama ulivyosema hii katiba imewapuuza na sheria nyingi ya nchi zimewapuuza hata ninapozungumzia habari ya matumizi ya ardhi, utakuta ardhi inayotumiwa na wafugaji mara nyingine huitwa idle land, kama mimi ninakotoka masaini utakuta wa masaai wanaambiwa ardhi yao nyingi ni idle land haitumiki. Na wanasahau kuwa kila sehemu ya ardhi ya mfugaji inatumika kwa sababu ya malisho na ardhi katika sehemu kama hizi ni tofauti na ardhi katika sehemu ya mkoa wa kati ambako acre moja unaweza kulisha mifugo yako watano mwaka mzima, hapa utahitaji pengine acre hamsini kuweza kulisha mifugo watano kwa mwaka mmoja ama sivyo? Kwa sababu ardhi ni tofauti na ndiyo maana ndungu yangu Ali ningependa uangalie katika sehemu za land mambo ya land, tumetambuwa kitu kinachoitwa communal land owndership, ardhi inayomilikiwa na watu kwa jumla, kwa sababu ya mambo ya malisho na ninajuwa pengine haikutoka wazi wazi na ungependa itoke wazi wazi lakini ningependa tu uangalie chapter 11 katika Land Policy framework, tumejaribu kutaja sana kuhusu mambo ya wale wanaomiliki ardhi kwa sababu ya malisho yao. Lakini pia maoni yako kusema kuwa unataka itoke wazi wazi tumeichukulia na itazingatiwa.

Kuhusu pia watu kupuuzwa watu wa hasa kutoka sehemu kama hizi, ukiangalia Chapter 3 Article 14 if you have the papers Ali, una ile karatasi hebu tuangalie pamoja, Article 14 angalia Sub-Article 11.

**Ali Wario**: Iko page ngapi?

**Com. Lethome:** Sasa page yako na yangu itakuwa ni tofauti lakini ngoja, National goals and values, iko page four. Ukiangalia page four Sub-Article 11 chini ya 14 kuna 1,2,3, mpaka kumi na moja.

**Ali Wario:** Page five.

**Com. Lethome:** Page five number kumi na moja tumesema hapa, the Republic shall ensure the fullest participation of women, the disabled and the marginalized communities and sectors of the societies in political, social and economic life of the country. Marginalized, sasa pastaralists wameingia chini ya marginalized. Jambo lingine ndungu yangu Ali ningependa kusema ni kuwa, katiba haiwezi kuzungumzia kwa tafsiri juu ya kila jambo, sasa ni juu ya Bunge kuhakikisha kuwa inachukuwa muongozo kama huu kutoka hapa, muongozo kuhusu matumizi ya ardhi kutoka katika sehemu inayozungumzia juu ya ardhi na kubuni sheria itakayozungumzia sasa kila kitu kinacho husu kwa mfano mkulima wakulima shamba wa mimea, mkulima wa mifugo na mkulima wa aina nyingine yeyote. Kwa hivyo zile tafsiri zitakuwa katika Act of Parliament, ni kama vile mambo ya elimu kama vile ulivyouliza mambo ya elimu, hapa tuemsema kila mtoto ana haki ya elimu ya msingi ambao ni free and compulsory. Ya lazima na iwe ni bure sasa tafsiri za kusema kwa sababu tumesema kila Mkenya maana yake, mfugaji wa hama hama ameingia ndani yake kwa sababu ni Mkenya.

Ni jukumu sasa la Bunge ipitishe education Act, sheria ya elimu ambayo itahakikisha kila mmoja kulingana na lifestyle yake na

mtindo wa maisha yake ameipata hiyo elimu. Kwa hviyo, katiba hapa haiwezi hapa kuandika kuhusu mambo ya mobile schools, skuli za kuhama hama, itakuwa sasa ni kutokana na muongozo wa katiba, Bunge libuni sheria itakayo hakikisha yule mwenye kuhama hama anapata masomo, yule mwingine ambaye anataka kusoma intergrated masomo ya dini na mengine yasiyo kuwa ya dini, ihakikishe kuwa imeingia huko. Kwa hivyo, kazi kubwa hapa ni muongozo itoke kwenye katiba, Bunge lipitishe sheria itakayo simamia sehemu hiyo ili kuhakikisha kila mmoja anapata haki yake, lakini hayo ni maoni mazuri uliyosema na haya mengine yote kuhusu Bunge kupitisha sheria ambyao ni kunyume na sheria Kiislamu, hayo yote tumeyanukuu na yatakuwa ni mwongozo katika utaratibu uliyobaki kwa kazi hii.

Ningependa kuendelea sasa na sehemu zingine kwa sababu, bado tuna sehemu nyingi sana na ningependa tugusie at least kila sehemu kabla ya jioni kufika.

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Lethome:** Hatujaingia kwenye ardhi tafadhali.

**Interjection:**

**Com. Lethome:** Ni kwa sababu Ali aligusia lakini itakuja mambo ya ardhi tafadhali. Naona mambo ya ardhi tungoje kuna chapter special on land, there is a special chapter on land

**Interjection:** Nilikuwa ninataka kuongezea pahali bwana Ali aliongea

**Com. Lethome:** Ngoja.

**Kassim Dakane Kunow:** Kassim Dakane Kunow, nilikuwa ninataka kuongezea hapo bwana Ali vile alisema nafikiri ile swali alikuuliza ni kuhusu maisha ya hii watu pastaralist na hata vile umetujibu watu bado hawaja fahamu.

**Com. Lethome:** Wewe sema sija fahamu.

**Kassim Dakane Kunow:** Sija fahamu na pahali nilikuwa ninataka unifahamishe, yeye amesema maisha yangu kama hii katiba ilipitishwa na vile imepitishwa hivi sasa ikielekea na siku husishwa mimi nikiwa mfugaji, kulingana na nchi zingine unaona mfugaji anahifadhiwa sana kulingana na ile hifadhi zake. Kwa sababu, kuna nchi zingine unakuta ile mnyama kama ngombe inahifadhiwa kabisa kama vile sasa crops imewekwa upande wa agriculture lakini mfugaji ametengwa kabisa.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo kwa ufupi tunaita marginalized imekuwa marginalized si ndiyo?

**Kassim Dakane Kunow:** Ndio kabisa, sasa hapo ndiyo nilikuwa ninataka kujuwa maisha yake inaelekea wapi katika hii katiba ya Kenya?

**Com. Lethome:** Sasa ndungu yangu ninafikiri ni wewe ndiyo huku fahamu usiseme wengine hawakufahamu, wengine

walifahamu. Nilimueleza bwana Ali kuwa kuna kifungo kinachosema kuwa, serikali itahakikisha makundi ama jamii ambazo zimetengwa marginalized groups na pastaralists wanaingina chini ya marginalized group, zitahakikishiwa kuwa zimeshiriki kikamilifu katika maisha ya kijamii social life, political life and economic life, mambo ya uchumi na tunapozungumzia habari ya uchumi ya pastaralist tunazungumzia habari ya mifugo yake. Kisha nikamusomea sehemu ambayo inazungumzia hapo na nikamuambie angalia Article 14 Sub-Article 11, umesikia nikimuambie hivyo? Nikamuambie angalia ukurasa number tano na tukaangalia pamoja tukakuta kuna hilo marginalized communities wale ambao wametengwa unaona, na nikamuambia katiba haiwezi kuandika kila kitu kuhusu communities moja moja. Kuna kitu ambacho tunaita Act of Parliament, sheria inayopitishwa na Bunge, katiba inatoa muongozo, general principle, details una fahamu maana ya details? Hizo huja kwenye Act of Parliament.

Kwa mfano mambo ya elimu katiba inasema kila mmoja kila mtoto Kenya apate elimu ya bure ya msingi inaishia hapo. Lakini inasema Bunge lihakikishe kufikia miaka miwili ijayo limebuni sheria ya kuhakikisha jambo hilo limepatikana, kuhusu mambo ya pastaralist na other marginalized group, Bunge lipitishe sheria kuhakikisha kuwa malalamishi yao yamechukuliwa kwa hivyo ndiyo nimekuwambia jambo alilolizungumzia Ali na wewe ni muhimu lakini mahala pake ni Bunge sasa ipitishe sheria kutokana na muongozo wa katiba ili mfugaji asibaki nyuma wala asisahaulike. Umefahamu ndungu yangu?

**Com. Lethome:** Ninaingia sehemu nyingine sasa ya uakilishi. Nilipoanza kuzungumza asubuhi, nilizungumzia habari ya mamlaka yote kuwa yanatokana na raia ama sivyo tulivyosema? Tukasema mamlaka yanayotumiwa na Bunge, legislative authority imetokana na mwananchi wa Kenya, yeye ndiye mwenye kupiga kura kumpeleka Mbunge kule.

Executive authority, ili inayotumiwa raisi na baraza la mawaziri katika kutekeleza majukumu yao imetokana na mwananchi pia.

Judicial authority, mamlaka yanayotumiwa na mahakama pia yametokana na mwananchi, lakini ili mwananchi aweze kushiriki, hawezi kushiri kila mmoja kwa mfano, sisi wote ni millioni thelathini haiwezekani sote kwenda Bunge ama inawezekana?
**Audience:** La.

**Com. Lethome:** Itakuwa ni Bunge moja kubwa sana itakuwa Kenya mzima ni Bunge. Kuna wawakilishi wetu wanao kwenda kule na ndiyo sababu tunapiga kura. Kwa hivyo sehemu sheria ya kupiga kura pia ni muhimu sana, na ndiyo sasa tunataka tuangalie mapendekezo yaliyoko katika mambo ya kupiga kura.

Kwanza tumependekeza hapa chini ya sehemu hiyo kuwa, ni haki ya kila mwananchi kupiga kura nafikiri ninapozungumza hivi utasikia wengi wanalalamika wanasema, mimi mwaka uliopita mwaka wa tisini na saba nilitaka kupiga kura lakini sikuweza kupiga kura, sababu ni nini, sikupata kitambulisho cha kupiga kura, kwa nini hukupata sina kitambulisho cha nchi. Kwa nini huna kitambulisho cha nchi, nimekwenda kutaka kupewa lakini utaratibu wa kutoa kitambulisho ni mgumu sana ama sivyo?
**Audience:** Ndivyo.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo hapa tunasema ni jukumu la serikali kuhakikisha kila mmoja anapata hiyo haki ya kupiga kura lakini katiba imesema ni haki yako kama mwananchi kuweza kupiga kura ili utoe mamlaka yako umpe yule mwenye kukuwakilisha, anapoyatumia haya mamlaka ajue anatumia mamlaka uliyompa yeye kama raia.

Kwa hivyo ukiangalia kifungo number sabini na nane, Article 78 inasema, mtu yeyote ambaye amefikisha umri wa miaka kumi na minane basi ana haki ya kupiga kura na mtu kama huyo awe ni mwananchi wa Kenya, kuna masharti yaliyopangwa pale. Ndungu yangu kuna nini?

**Interjection:** Maswali moja tafadhali baba.

**Com. Lethome:** Haya tafadhali baba uliza basi haraka twende.

**Interjection:** Ninauliza swali nzuri sana.

**Com. Lethome:** Sawa mpe mpe.

**Michael Atego:** Mimi swali langu halitajukuwa hatua.

**Com. Lethome:** Jina lako tafadhali?

**Michael Atego:** Mimi ninaitwa Michael Atego Asego. Swali langu ni kuhusu hivi, mimi nimefika umri wa miaka kumi na tano sawa, nimeenda pale mahali inapewa vitambulisho nimepeana document yangu yote, haya kitambulisho ninaongojea kura iko karibu na hiyo kitambulisho nitaongojea nipewe baada ya kura, then inasemekana nijaze ingine tena.

**Com. Lethome:** Ni nani anakuambia ujaze ingine tena?

**Michael Atego:** Hiyo ni vitu mimi nimeona.

**Com. Lethome:** Ndiyo ni nani amekuambia?

**Michael Atego:** Ni nani, sasa ukiweka mtu pale mimi ninaenda kuuliza yeye ni nani?

**Com. Lethome:** Basi ni sawa.

**Michael Atego:** Siendi kuuliza yeye ni nani yeye ananijazia form na ninapigwa picha pale, hiyo picha mimi ninangojea itoke kule ninaambiwa bado iko kwa computer itakuja tu ngojea, mimi ninaendelea kuongojea. Hiyo ndiyo kitu mna umiza nayo wananchi halafu mkikuja mnadanganya sisi hapa, oh, oh Nairobi, tengenezeni siasa mzuri, mtafute kura mzuri kwa njia ile inafaa msaidie wananchi.

**Com. Lethome:** Asante japo hatutafuti kura sisi bwana, sisi hatukuja kutafuta kura bwana. Haya basi tuendeleeni amepata uhuru wake freedom of expression. Tunasema pia ukiangalia kipengele number themanini na moja Article 81 kuhusu tume ya

uchaguzi, Electoral Commission na majukumu ambayo tumeipa. Kuna baadhi ya majakumu ambayo tumeipa tume ya uchaguzi, Electoral Commission of Kenya yako hapi, miongoni mwao ni kuhakikisha kuwa utaratibu wa kupiga kura una fahamika, simple and precise kusiwe na utaratibu ambao ni mzito kufahamika na kufuatwa. Kuhusu masanduku ya kura, hivi sasa rangi ya masanduku ya kura huwa ni rangi gani?

**Audience:** Nyeusi.

**Com. Lethome:** Ukiangalia katika vyombo vya habari nchi nyingi sana nafikiri sisi ndiyo tumebaki nyuma, masunduku huwa ni transparent yanaonekana kilicho ndani hapa ninajuwa kawaida ikienda kwenye polling station huinamishwa hivi ama sivyo, unaambiwa iko kitu ndani kwenye debe? Hakuna lakini kilicho huko ndani kama kuna kitu kimenasa kwa bundi unaweza kuona? Hakuna, sasa ndiyo nilisema kulingana na mtindo unaofuatwa na nchi nyingi ili kuwe na uwazi masanduku pia yawe transparent.

Ya pili kuwa, ihakikishe kuwa kura mara nyingi malalamishi mengi kuhusu mambo ya kura ni kuhusu kuhesabiwa kura ndiyo hupotea kura nyingi ama sivyo? Mwaka tisini na saba mlipigia kura wapi nyinyi watu wa hapa Bura, mlipigia wapi? Kituo cha kupigia kura kilikuwa wapi?

**Audience:** Hapa.

**Com. Lethome:** Hapa hotelini hii?

**Audience:** Shuleni.

**Com. Lethome:** Pale shuleni na zilihesabiwa wapi?

**Audience:** Hola.

**Com. Lethome:** Hapo, kwa hivyo hapo hapo skulini na zikahesabiwa hapo.

**Audience:** Kuna zingine zinatoka Mbalambala.

**Com. Lethome:** Kuna zingine zinatoka Mbalambala zinaletwa hapa?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Kutoka Mbalambala mpaka hapa ni kilometer ngapi?

**Audience:** Mbali.

**Com. Lethome:** Mbali, tuseme mia moja ama zaidi ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Yanayotokea hapa kati kati kura zinaposafirishwa kuna mtu anayeijuwa?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Sasa watu wengi wamelalamika wakasema kuwa kura nyingi huwa zinapotea zinaposafirishwa kwa hivyo, chini ya sheria mpya kura zihesabiwe mahali inapopigiwa. Ikiwa pigiwa Mbalambala zihesabiwe huko huko, Hola huko huko, hapa Bura zihesabiwe huku huku, zisiwe zinasafirishwa kabla ya kuhesabiwa. Hilo ni jukumu ambalo limepewa tume ya uchaguzi.

Kisha baada ya hapo tunaangalia tume ya uchaguzi yenyewe, mara nyingi siku hizi utasikia tume ya uchaguzi inalaumiwa kwa kupendelea. Mara nyingi huwa inalaumiwa kuwa inapendelea chama kipi? Kinachotawala ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Inaambiwa unapendelea hivi kwa sababu ndiyo kiko serikalini, kwa hivyo chini ya sheria mpya tunataka tume ambayo iko uhuru ambayo haionekani kuwa inalemea upande wowote. Kwa hivyo uchaguzi wake na hasa uchaguzi wa mwenyekiti uwe pia unapitia katika Bunge, kwa hivyo hata Rais akiwa na haki ya kuteuwa, ateuwe tu lakini huo uteuzi wake lazima upitishwe na Bunge kwa sababu Bunge linawakilisha watu wote, kila mmoja. Chini ya katiba mpya tunasema tunapendekeza wasiwe chini ya wananae at least mtu mmoja mmoja kutoka kila mkoa kuweze kupatikana mtu mmoja mmoja kutoka kila mkoa na wasiwe zaidi ya kumi kwa hivyo, baina ya nane na kumi. Na mwenyekiti atakuwa ni mwenye kuteuliwa na Rais lakini awe ni mwenye kupitishwa ama uteuzi huo uthibitishwe Bunge lenyewe.

Mwenyekiti awe ni mtu ambaye masomo yake na ujuzi wake unamwezesha kuwa Jaji wa mahakama kuu kwa sababu hutokea matatizo mengi ya kisheria, awe ni mtu ambaye anafahamu matatizo kama hayo ya kisheria. Kazi za tume ya uchaguzi, hivi sasa kazi za tume ya uchaguzi ni zipi? Nafikiri tunazijuwa moja:

Registration, kuandikisha wapiga kura ama sivyo? Haya nyingine?

**Audience:** Kupanga uchaguzi.

**Com. Lethome:** Kupanga uchaguzi na kusimamia uchaguzi ama sivyo? Haya kazi nyingine?

**Audience:** Kutangaza matokeo.

**Com. Lethome:** Kutangaza matokeo ya uchaguzi, sasa chini ya katiba mpya tumependekeza kutokana na maoni ya wananchi, hayo na zaidi hayo hasa kuhusu mambo ya uandikishaji wa wapiga kura. Dadika hii kwa mfano, ikiwa wewe hukujiandikisha kupiga kura na unataka kujiandikisha sasa hivi kabla uchaguzi unaweza?

**Audience:** Huwezi.

**Com. Lethome:** Utaambiwa tumefunga uandikishaji ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Uandikishaji una muda maalum, hufunguliwa kisha ukafungwa na utakuta kuwa inawaharimishia watu wengi haki ya kupiga kura kwa sababu, wakati ambapo unataka kujisajidili muda umekwisha imefungwa, mpaka ungoje tena mpaka watakapo fungua. Chini ya katiba mpya tunasema kuwe na continuous voter registration, iwe ni ya kuendelea mpaka siku ya uchaguzi, mpaka wakati wa uchaguzi watu wawe wanaendelea kujiandikisha.

Mambo ya kuweka mipaka ya sehemu za uakilishaji Bungeni au wakilishaji katika mabaraza, wahakikishe kuwa pia kuna uchaguzi wa wadilifu wa haki. Kitu kipya tumesema pia tume iwe ni yenye kusimamia vyama vya kisiasa, hivi sasa utakuta vyama vyote vya kisiasa hakuna msimamizi wa kuhakikisha kuwa vyama vya kisiasa vina nidhamu fulani ambavyo vinafuatwa na vinaweza kuchuliwa hatua vikikeuka na ndiyo sababu leo hii kwa mfano, mimi nikija na chama changu hapa nataka kuandaa mkutano wa chama changu hapa na eneo hili wafuasi wengi sio wa chama hichi changu pengine nitapigwa kwa mawe hapa ama sivyo? Ama nitatukanwa ama itatokea vurugu lolote ama utakuta vyama vingine vya kisiasa mpaka vina majeshi yao utasikia sijui kuna taliban, kuna mungiki, kuna bagdad boys, pengine utasikia kuna jeshi la mzee kwa sababu hakuna nidhamu imekuwa kazi ya vyama vingi vya kisiasa ni matusi kutukanana tu. kwa hivyo, tumesema tume ya uchaguzi iwe ndiyo yenye kusimamia vyama kama hivyo.

Tatizo lingine leo hii tukitangaza campaign imeanza vyama vyote vitakuwa sawa katika kufanya campaign yao? Wengine wataweza hata kupata helicopter ya kufanya campaign ama sivyo? Na wengine hata gari moja la kufanya campaign hakuna itabidii wafuate wafuasi wao nani ana landrover yake atusaidie ama sivyo? Yaani vyama vyote haviko sawa kifedha kiuchimi. Ndiyo tumesema hapa kutakuwa na political party's fund, kutakuwa na hazina ya vyama vya kisiasa ili kuhakikisha kuwa vyama vyote ambavyo vimetimiza masharti yatakayowekwa zinaweza kusaidiwa katika shughuli zake, sasa hapa mtu anaweza kusema ikiwa akutakuwa na pesa vyama vya kisiasa vitapewa mimi na ndungu yangu na mke wangu tutatengeneza chama chetu cha kisiasa ili tupewe pesa ama sivyo wandungu yangu? Hii ni njia rahisi mteremko wa kupata pesa kutoka kwa serikali, lakini tunaambiwa hapa hakuna chama ambacho kitapewa pesa hizo kisipotimiza masharti na baadhi ya hayo masharti ni kuwa kila chama lazima kiwe na kile tunaita national character. Kiwe na sura ya kitaifa kisiwe na sura ya sehemu moja nchi bila nyingine au sura ya kikabila au sura ya dini fulani na leo hii ukijaribu kuangalia kila chama tulicho nacho utaweza kukihusisha na kabila fulani tuanzeni, DP ni ya wakina nani?

**Audience:** Kikuyu.

**Com. Lethome:** Unaona moja kwa moja tunajuwa tu, NDP ilikuwa ya kina nani?

**Audience:** Wajaluo.

**Com. Lethome:** Ford Kenya ni ya kina nani?

**Audience:** Luhya.

**Com. Lethome:** Ford Asili ni ya kina nani?

**Audience:** Wakikuyu.

**Com. Lethome:** Saba saba Asili ni ya kina nani?

**Audience:** Wakikuyu.

**Com. Lethome:** Shirikisho party ni ya kina nani?

**Audience:** Coast.

**Com. Lethome:** Coast ama sivyo? Na si Coast yote Wadigo kule chini, sio Coast nyinyi si ndiyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Haya tuingie nyingine SDP ni ya kina nani?

**Audience:** Wakamba.

**Com. Lethome:** KANU ni ya kina nani?

**Audience:** Afadhali hiyo.

**Com. Lethome:** Afadhali kidogo afadhali ama sivyo? Kwa hivyo ndiyo tunasema hapa chini ya sheria mpya, vyama vingi vilivyosajiliwa vitaanguka kwa sababu, vina sifa vya kikabila au sifa ya sehemu moja ya nchi. Kwa hivyo havitapata hiyo funding, havita pata kupewa hazina hiyo, hazina itakuwa ni ya chama ambacho kina sifa ya nchi nzima, national character. Pesa katika hazina zitapatikana kutoka katika budget, mizania ile inayosomwa kila mwaka itakuwa 0.3% ya ile budget ya nchi itakuwa ni ya political parties fund. Kuna kitu kingine ambacho tunaita voter education, wananchi wengi huwa hawajui haki zao za kupiga kura ana ile card lakini hajui kima chake mwingine atakuambia hii naishika tu ngoja, si huu ni mwaka wa uchaguzi, hii bila kupewa shillingi elfu moja na yule hii yangu hapatii tunaiuza ile. Unasahau kuwa haina thamani na ni kujitukana wewe unapompa mtu kwa sababu amekununulia kilo moja ya sukari, huwa unajitukana mwenyewe, hiyo ni haki ambayo hakuna mtu anaweza kuinunua ile haki yako. Hebu fikiria unapoipiga hiyo kura yako, unampa mtu haki ya kuenda Bunge miaka mitano na kwenda kukuamulia wewe maisha yako kwa hivyo tunasema ni juu ya tume ya uchaguzi kuwaelemisha wananchi kuwapa kitu kinachoitwa voter education, kusimamia mambo ya uchaguzi na pengine kukiwa na malalamishi yeyote kuhusu mambo ya uchaguzi itakuwa ni kazi ya tume hiyo kusimamia.

Tuingie katika vyama vya kisiasa, tulipokuwa tunazungumzia habari ya haki za kimsingi tulizungumzia juu ya haki za kisiasa tukasema ni haki ya kila mwananchi kujiunga na chama cha kisiasa anachotaka. Lakini vyama hivi vya kisiasa lazima viwe na

nidhamu kwa hivyo kuanzia kifungu number themanini na saba tumeweza kuzungumzia juu ya vyama vya kisiasa vinatakiwa viwe na nidhamu ya aina gani. Muhimu ambalo nataka tusome pamoja ni kuhusu kazi zinazofanywa na vyama vya kisiasa, ngoja niwaulize swali moja hapa muone vile ambavyo huwa hatujui tunafuata tu.

Vyama vya kisiasa kazi yao ni nini kwa mfano, wewe chama chako tuseme ni KANU si ndiyo? Kazi ya KANU kama chama cha kisiasa ni nini? Ama DP, ama Ford Kenya, Ford Asili, kazi yake ni nini? Mbona yaani nyinyi si wafuasi wa vyama vya kisiasa?

**Audience:** Kulinda haki yako vipi.

**Com. Lethome:** Kulinda haki yako vipi? Serikali ndiyo inalinda haki yako sio chama cha kisiasa. Mwingine atasema mimi chama changu ni KANU kazi yake imesekana wazi wazi ni kupinga upinzani ama sivyo? Hakuna kazi nyingine na ndiyo unaona tuna fujo nyingi sana kuhusu mambo ya vyama vya kisiasa. Leo hii mimi nikipanga hapa mkutano ukitaka kujuwa ule mkutano ni wa upinzani ama ni wa chama kinachotawala, sikiza tu yale matusi yatakayo kuwa hapo. Mambo ya kutukanana na kuchocheana na kutoa ahadi za uwongo, ni mkinichagua mkichagua chama hiki tutawapa hiki na hiki na hiki, mwingine naye anakuja anakuambia changu ukikichagua hivi na hivi na hivi. Kwa sababu katiba iliyoko haijapangia vyama hivi function zao ama kazi maalum za kufanya ambazo zitalete maendeleo kwa hivyo tumesema kazi zake zimepangwa, miongoni za kazi za vyama vya kisiasa ni mambo ya kulete maendeleo katika nchi na pia kuweza kuwaelemisha wananchi juu ya haki zao, civic education na ku-mobilize kupata ile rai ya umma au ya wakenya kuhusu jambo lolote linalowahusu. Kwa mfano, hivi sasa maswala ya katiba Bunge livunjwe lisivunjwe, maslaha ya wakenya yako wapi tuende katika uchaguzi chini ya katiba ya zamani ama ya hii mpya? Haya ni maswala ambayo yanahitaji msimamo wa wananchi, ni juu ya vyama vya kisiasa kuweza kuwahimiza kuwahamasisha watu waweze kuwa na msimamo kuhusu jambo kama hilo.

Na kwa vile vitakuwa vyama vya kisiasa vikipewa msaada fulani wa kifedha kila mwaka kila chama lazima kifanye kile kinachoitwa returns, kuonyesha kwa muda wa mwaka mmoja uliyopita hicho chama kimefanya nini activities. Ya pili, msaada kilichopata kimetumia vipi? Hivi leo ukichunguza hakuna returns ambazo zinafanywa na political parties, utakuta viongozi wa vyama wanazungumza habari ya democrasia, ukichunguza chama chenyewe ndani yake hakuna democracia, chama kina milikiwa na mtu mmoja ama wawili. Utakuta chama hakijafanya uchaguzi pengine tangu kisajiliwe mpaka leo hakijafanya uchaguzi wa mashinani na kinaendelea tu inasema democracy na ndani ya chama hakuna democracy. Ndiyo maana tumeweka uchaguzi chini ya tume ya uchaguzi na tumeweka nidhamu ambayo ni lazima ifuatwe na vyama vya kisiasa.

Kisha tumesema mtu ikiwa amechaguliwa kwa tikiti ya chama fulani kuenda kuwakilisha wananchi wa sehemu fulani Bungeni, kisha akifika huko aamue kukihama hicho chama basi sheria imesema arudi kwa wananchi wakampigie kura tena, atafute uakilishi mara ya pili kwa sababu imani ya watu walipompigia kura kama alisimama na chama ilikuwa pengine ni katika chama alicho simama nacho. Akitaka kubadilisha lazima arudi kwa wananchi tena.

Chini ya vyama vya kisiasa pia tumesema tunatambuwa kuwa kuna watu ambao wangependa kusimama bila ya kuwa na chama chochote wametambuliwa independent candidates pia wako hapo. Ukiangalia sehemu ya tisini na saba, Article 97 ndiyo imezungumzia juu ya vyama vya kisiasa na vitakavyo simamiwa na tume ya uchaguzi. Kipengele number tisini na nane kinazungumzia juu ya nidhamu katika vyama vya kisiasa.

Jambo lingine muhimu sana lazima tulizingatie hapa, leo hii mimi nikiwa ni waziri na mimi ninasimamia pengine cha fulani, mimi ni katibu Mkuu wa chama fulani, itakuwa wakati ninaposhughulikia chama changu ninatumia rasilmali za nchi kama waziri ama kwa mfano, ikiwa mimi ni Raisi wa nchi na ni mwenyekiti wa chama cha kisiasa, inakuwa ni vigumu kwa wananchi kutofautisha baina ya mali ya chama na mali ninayotumia ya nchi kama Rais sijui kama mnanifahamu hapa? Kwa mfano, mimi niwe ni chairman wa DP na mimi ndiyo President wa nchi ninapokwenda kuhutubia mkutano wa DP, nitakuwa ninaweka gari lile langu la kiraisi kando kwanza natumia la DP ama nitatumia hilo hilo la Rais. Hali ilivyo utakuta anatumia lile lile la Rais, bodyguard anayotumia ni yule yule anayemlinda akiwa Rais inakuwa watu hawajui mimi ninapozungumza kama chairman wa DP, ninazungumza kama President wa nchi au kama wa chama. Ninapoendesha siasa za chama, watu wakati mwingine wanaweza kufikiria kuwa ni siasa za nchi kumbe ni siasa za chama.

Kwa hivyo, ndiyo tumesema hapa chini ya kifungu number kumi na moja, mtu yeyote akichaguliwa kuwa Rais au apewe mamlaka yeyote katika serikali kuanzia Deputy Secretary hadi juu basi asiwe na cheo chochote katika chama cha kisiasa, sababu ni nini? Kulinda mali ya nchi yasitumiwe kuendesha siasa za chama, mimi nikiwa Permanent Secretary nisitumie cheo changu kuendesha siasa za chama changu kwa sababu kuna mwingine ambaye ana chama chake na yeye si Permanent Secretary, hatapata nafasi kama ile yangu ya kuitumia kuendesha siasa ya chama. Kwa hivyo, katiba hii mpya ikipitishwa hatutopata Rais ambaye ni mwenyekiti wa chama au katibu wa chama au organizing secretary wa chama. Ukishachaguliwa tu katika cheo katika nchi unawahudumia wananchi wote cheo cha chama cha kisiasa unawacha kando, sijui kama mumenifahamu hapo?

**Audience:** Tumefahamu.

**Com. Lethome:** Na tumesema hapa ni haramu ama ni kunyume cha sheria mtu yeyote kutumia mali ya umma kuendesha siasa ya chama kwa mfano, mimi nina gari hapa GK ni mali ya nani? Ya serikali mali ya umma hii kwa vile mimi ni Commissioner nimepewa hiyo gari siasa zimeanza naitumia kwenda kufanya campaign ya chama changu. Ni kunyume cha sheria na inatakiwa nishtakiwe mara moja kwa sababu nyote mwajuwa vile mali ya umma imetumiwa vibaya kwa sababu ya siasa ama hamjui?

**Audience:** Kweli.

**Com. Lethome:** Utakuta mpaka wafanyikazi wa serikali wametumiwa katika kuendesha mambo ya siasa, tumesema chini ya katiba mpya yakomeshwe haya yaishe.

**Audience:** Hata ndege inatumika.

**Com. Lethome:** Hata ndege inatumika, hii ndege kidogo kidogo.

Tunaingia katika Bunge sasa Chapter seven sasa hatutaki kuwavunjia Waislamu haki yao ya kwenda kuswali salatul thuhur, athuhuri mnaswali saa ngapi?
**Audience:** Saa saba na robo.

**Com. Lethome:** Haya bado dakika kumi kwa hivyo tunavunja kikao sasa, tunatoa muda wa saa moja peke yake tafadhalini saa nane kamili turudini hapa tuendelee na kikao sawa bwana, haya twendeni tukaswali hiyo ni haki ya kimsingi.

Tunaze sasa poleni tumechelewa kidogo sasa tutaendelea, asubuhi tumezungumzia habari ya kupiga kura na tukaeleza vile ni haki ya kila mwananchi kuweza kupiga kura kwa sababu wale ambao tunawapeleka Bunge wanatumia uwezo huo ambao sisi raia tunawapa ili waweze kuendesha shughuli katika Bunge. Sasa tungependa tuangalie Bunge lenyewe tunapendekeza nini katika Bunge na tunajuwa kwanza kazi ya Bunge, kazi ya Bunge ni kutengeneza sheria za nchi na uongozi wote unatokana na Bunge. Na wale wako huko tumewapa mamlaka hayo wafanye kwa maslaha yetu, kwa hivyo utaona sisi tumependekeza hapa baadhi ya mambo ambayo yatafanywa na Bunge kwa niaba yetu lakini kutakuwa na mabadiliko kidogo nafikiri mumesikia watu wengi wakisema chini ya sheria mpya badala ya kuwa na Bunge moja tutakuwa na Bunge mbili.

Moja tutaita National Council baraza la kitaifa, ya pili tutaita National Assembly kama ile ambayo tuko nayo hivi sasa. Hii ya kwanza ambayo tunaita National Council wazee wa zamani watakumbuka tulivyopata uhuru mwaka wa sitini na tatu, tulikuwa na kitu kinaitwa senate sasa hatutakuwa na senate tutakuwa na National Council baraza la kitaifa na itakuwa na wawakilishi kutoka kila wilaya, District. Kwa mfano, hivi sasa Kenya tuko na District ngapi? Nani anajuwa tuko na District ngapi Kenya?
**Audience:** Sabini.

**Com. Lethome:** Sabini, District zote za Kenya ni sabini kila District itafanya uchaguzi wa mtu mmoja kwenda kuwakilisha District kwa mfano Tana River District, kutatoka mto mmoja kwenda katika hilo Bunge ambalo tumeliita National Council kuweza kuwakilisha maslahi ya watu wa District mzima. Kwa hivyo tutakuwa na wanachama wangapi katika hiyo Bunge?
**Audience:** Sabini.

**Com. Lethome:** Mmoja kutoka kila sehemu ama kila wilaya. Baada ya hapo kuna kitu kinaitwa affirmative action, affirmative action maana yake ni kujaribu kuwaleta wale ambao wako nyuma kuwaleta mbele wawe sawa na wengine. Na kama nilivyotanguliwa kusema asubuhi, imeonekana kuwa kina mama ni watu ambao wamebaki nyuma sana, wanawake kwa hivyo, wanapewa viti thelathini katika hilo Bunge ambalo tumeliita National Council. Kwa hivyo, sabini ukiongeza thelathini inakuwa ngapi? Mia moja, na hiyo thelathini hatutaki wachaguliwe wanawake wa kutoka sehemu moja peke yake au baadhi ya mikoa na mikoa mengine ibaki nyuma, tukifanya hivyo itakuwa tunadhulumu baadhi ya mikoa.

Kwa hivyo utaratibu uliyowekwa na sheria ni kuwa vile viti thelathini vya wanawake tutavigawanyia mikoa saba, mikoa yote ya Kenya ni mingapi?
**Audience:** Nane.

**Com. Lethome:** Nane, ondoa Nairobi unabaki na ngapi saba, ukigawiya mikoa saba kila mkoa viti vine, vitakuwa ishirini na nane, viwili vilivyobaki Nairobi vyote vimekuwa thelathini. Huo ndiyo utaratibu utakaowekwa kwa sababu Nairobi iko karibu na Bunge na inawakilishwa kwa njia nyingi, kwa hivyo hiyo ni sehemu ya kwanza ya Bunge.

Sehemu ya pili ya Bunge ni ile ya kawaida ya Wabunge tunawaowachaguwa kuwakilisha sehemu zetu za uakilishaji Bungeni, constituencies kwa hivyo tutakuwa na viti mia mbili na kumi vile vya kawaida na kwa sababu ya jamii ambazo huwa zinabaki nyuma au pengine haziwakilishwi vizuri katika uchaguzi, kutakuwa na viti vya Wabunge wateule, nominated members tisaini ambavyo vitagawanywa kulingana na kuangalia sehemu ambazo hazikuwakilishwa vizuri au sehemu ambayo ina watu wengi na inawakilishwa na mtu mmoja. Hivyo viti tisaini vitagawanywa kwa njia ambayo itahakikisha kuwa kuna usawa, kwa hivyo Bunge litakuwa na Wabunge mia nne na lile lingine mia moja kwa hivyo wote yaani National Assembly na National Council zikiwekwa pamoja zitakuwa ni Parliament ndiyo Bunge. Watu wengine wanasema ni kwa nini tuwe na Bunge mbili, sababu ni kuwa kuna kitu katika lugha ya Kiingereza tunaita checks and balances. Checks and balances ni kuwa kwa mfano mimi leo nikifanya kitu najuwa kuna mkubwa wangu ananiangalia ataniuliza kwa nini umefanya hivi na yeye pia akifanya kimakosa ataulizwa na aliyemkubwa kuliko yeye sasa Bunge tulipatia mamlaka lazima pia tuliweke chombo kingine cha kuweza kuirekebisha hiyo Bunge ikifanya makosa. Ndiyo maana tukaweka hiki chombo ambacho tumekiita National Council ili Bunge likifanya jambo iwe kuna chombo kingine ambacho kinaangalia Bunge linafanya sawa ama si sawa.

Kitu kingine ni kuwa itakuwa wananchi wanawakilishwa zaidi, kwa sababu tutakuwa na Mbunge wa kawaida ambaye anawakilisha constituency na mwingine anayewakilisha District, kwa hivyo itakuwa maslaha ya wananchi yanachukuliwa zaidi. Bunge pia tumelipa mamlaka zaidi kwa mfano, chini ya hii sheria ambao tunaitumia hivi sasa mamlaka mengi yako na Rais hayako na Bunge kama vile kuvunjwa Bunge, kuamua uchaguzi utafanywa lini, hakuna mtu anayejuwa kwa mfano Bunge litavunjwa siku gani, kuna mtu anajuwa? Hata MP wenu hajui Bunge litavunjwa lini anayejuwa ni Rais peke yake, tumetoa mamlaka hayo na tukapendekeza kuwa Bunge lisivunjwe na mtu yeyote, lijivunje lenyewe, muda wako ukiisha lijivunje lenyewe na Bunge pia liwe na calender yake, time table inajulikana ikifika tarehe fulani, mwezi fulani mwaka wa tano Bunge linavunjwa, ikifika tarehe fulani mwezi wa pili mwaka ujao baada ya Bunge kuvunjwa, Bunge jipya linakaa kikao chake cha kwanza yaani calender ambao inajulikana. Kwa mfano nikiuliza mtu hapa uchaguzi wa mwaka tisini na saba ulifanyika tarehe ngapi ama siku gani? Ishiri na tisa mwezi wa December ama sivyo? Na uchaguzi wa mwaka huu utafanyika tarehe ngapi?
**Audience:** Ishirini na nane.

**Com. Lethome:** Ishirini na nane nani anajuwa hakuna matu anayejuwa, na Bunge mpya itakaa kikao cha kwanza lini? Hakuna mtu anayejuwa ndiyo maana tumeweka ukisoma hapo utaona kuwa tumeweka mpangilio hivi kwamba Bunge itakuwa na

calender yake tarehe yake inajulikana ya kuvunjwa Bunge au Bunge kujivunja lenyewe na Bunge jipya kukaa kikao chake cha kwanza.

Majukumu ya Bunge, Bunge limepewa nguvu zaidi hapa kwa sababu nidhamu tutakayofuata hapa ni nidhamu ya Bunge, nithamu ambaye inaitwa kwa kizungu Parliamentary system. Nithamu ambayo inapatia Bunge mamlaka zaidi kuliko chombo kingine chochote, utaona hivi sasa kuna kitu tunaita constitutional offices, wale wanaoshikilia mamlaka katika ofisi za kikatiba kwa mfano, tuna Balozi tuna kama Commissioner wa polisi, Mkuu wa sheria, Governor banki kuu ya Kenya na ma Jaji wale ambao wanateuliwa na Rais na mawaziri. Sheria imempa Rais mamlaka hivi kwamba yeye ndiye anayewateuwa na yeye ndiye mwenye kuwafuta na ndiyo utakuta hata saa saba za mchana kwenye taarifa ya habari unaweza kusikia waziri amefutwa kazi ama hamjasikia hivo? Taarifa ya saa saba unasikia waziri amefutwa kazi au mtu mwingine ameteuliwa.

Rais anapofanya hivyo huwa hajavunja sheria huwa anatumia mamlaka ambayo amepewa na sheria hii, sasa tumetoa mamlaka hayo kutoka kwa mikono ya Raisi yamewekwa katika Bunge. Raisi ana haki ya kuteuwa lakini uteuzi wake hautekelezwi mpaka Bunge ipitishe, kwa hivyo anasema mimi nataka huyu lakini huyu hatakuwa waziri au ambasaddor yaani Balozi mpaka Bunge ipitishe mumefahamu hiyo. Hivo hivo uteuzi wa ma Jaji, uteuzi wa Attorney General, Mkuu wa Sheria, uteuzi wa Prime Minister, Ministers na hata Governor wa banki kuu ya Kenya itakuwa hivyo. Mkuu wa polisi pia itakuwa hivyo, kwa hivyo ukisoma sehemu hiyo utaona kuwa kuna mamlaka mengi sana ambayo tumepatia Bunge. Na kila mama wasibaki nyuma, kuna kipengele ambacho kinasema lazima thuluthi moja ya wale watakao kuwa Bungeni wawe ni wanawake sasa itawezekanaje hivo, tumelipa Bunge muda wa miaka mitatu kutengeneza sheria ambayo itahakikisha kuwa katika uakilishi wa Bunge yaani ukigawanya mara tatu thuluthi moja itakuwa ni wanawake.

Uchaguzi wa watu wa Bunge namna utakavyofanyika umeelezwa na Bunge litakuwa na muda wa miaka mitano kama kawaida isipokuwa tu lile Bunge la kwanza ambalo tumeliita National Council litakuwa na muda wa miaka minne. Kwa hivyo uchaguzi utakuwa unafanywa baada ya miaka minne, uchaguzi wa Bunge lile la kawaida itakuwa vile vile tunavyofanya hivi sasa miaka mitano. Kuna sehemu inayozungumzia juu ya Mbunge anayechaguliwa kisha hatekelezi kazi yake, mamlaka tumesema iko kwa raia na raia wanaweza kumrudisha angalia kifungu number mia moja na kumi na mbili, Article 112 imeeleza utaratibu wa kuweza kumtoa Mbunge, wananchi wanawezaje kumtoa Mbunge. Najuwa hii inaweza kutumiwa vibaya kwa sababu ikiwa kwa mfano mimi na huyu bwana tunapigania kiti cha uBunge cha Bura, akinishinda tu mimi nitatafuta namna ya kumtoa ama sivyo, nitakuwa ninaanza sasa fitina kuchochea huyu hafai mpaka atolewe, hilo tumeliwaza na tukalifikiria tuwaweka masharti ya kuweza kumtoa Mbunge kama huyo.

Kwanza sababu za kumtoa Mbunge ni kuwa pengine kama akili yake si timamu au afya yake haimruhusu kufanya kazi, hiyo ni sababu moja. Sababu nyingine ni kuwa ameivunjia ama amekivunjia heshima cheo chake kama Mbunge kwa sababu kuna baadhi ya mambo hautarajii Mbunge kuyafanya. Akikivunjia kile cheo chake heshima ni sababu nyingine, sababu nyingine ni kuwa anakosekana kwa muda mrefu sana anakaa bila kuja kuwatembelea watu wake na inatokea sana ama sivyo, utamuona

mara moja pengine baada ya mwaka ama baada ya miaka mitano akija kuomba kura tena ama sivyo?
**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Ndiyo tumesema wale ambao wana tabia kama hiyo, sasa wakome wawe kila mara wanawatembelea watu wao wanawashauri na kuweza kujua matatizo yao ili waweze kuyawakilisha Bungeni. Hizo ndiyo baadhi ya sababu ambazo zinaweza kumfanya Mbunge atolewe, utaratibu wenyewe unasema hivi, ikiwa wewe unataka kumtoa ama Mbunge atolewe utaandika malalamishi utaomba kwa maandishi kumpelekea Speaker wa Bunge kuwa huyu fulani hafai kuwa Mbunge wetu tena, sababu kadha wa kadha kama nilivyotaja lakini ili kuepusha mtu asiwe ana mchimba mwenzake bila ya sababu sharti ya kwanza ambayo imewekwa ni kuwa, lazima upate signature ya asili mia thelathini ya wale waliyopiga kura wote katika ile eneo, 30% of the registered voters of the constituency. Upate signature ya asili mia thelathini ya wale wote waliojiandikisha kama wapiga kura katika ile constituency yako, ukishapata hivyo unapeleka pamoja na malalamishi yako kwa Speaker wa Bunge.

Speaker wa Bunge naye hachukuwi hatua mpaka atume kundi likafanye uchunguzi kutoka kwenye Electoral Commission, tume ya uchaguzi ikaganye uchunguzi kisha imletee taarifa Speaker wa Bunge kuwa ni kweli huyu bwana alivyotuhumiwa ni sawa, akili yake si timamu, ana maradhi ambayo hayamruhusu kufanya kazi, amevunjia ofisi yake ama cheo chake heshima au hawazuru watu wake. Basi wakiridhika na hiyo reporti watapeleka kwa Speaker tena, Speaker akiridhika ndiyo anaweza kutangaza kuwa kiti cha Bura hivi sasa kiko wazi kipiganiwe, mumefahamu utaratibu uliyoko kupatikane asili mia thelathini ya wapiga kura katika sehemu wa wakilishaji Bungeni, waweke sahihi ndiyo iweze kukubalika. Na sababu zenyewe zisiwe ni sababu tu za uzushi ziwe ni za ukweli kwa hivyo hayo ndiyo baadhi ya mabadiliko ambayo yamependekezwa katika Bunge chini ya sheria mpya.

Mengine ni kama yale yanavyotokea katika Bunge hivi sasa isipokuwa pia tumesikiza malalamishi ya wananchi kuhusu mishahara ya Bunge, wananchi wamelalamika wanasema kuwa walijiongezea mishahara mikubwa sijui kama nyinyi mnalalamika ama mnaridhika na hilo jambo? Ukiwa mfanyikazi nani anayekuwekea mshahara ni wewe mwenyewe ama mwajiri wako?
**Audience:** Mwajiri.

**Com. Lethome:** Mwajiri, sasa mwajiri wa Wabunge ni nani?
**Audience:** Sisi.

**Com. Lethome:** Sasa mlishauriwa walipojiongeza mishahara?
**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Na wewe binadamu ukiambiwa saa hizi bwana unataka kiasi gani cha pesa utajiwekea nyingi ama kidogo?
**Audience:** Nyingi.

**Com. Lethome:** Tabia ya mwanadamu wasomali wanasema mwanadamu ni *hunguri* si ndiyo ama *hunguri weine* ukitaka, ni tabia ya mwanadamu sasa kumuambia mtu wewe jiwekee unachotaka atajiwekea kikubwa, kwa hivyo usilalamike tuliwapa hiyo nafasi tumeiondoa. Kutakuwa na tume ambayo itaitwa Salaries and Remuneration Commission, ndiyo itaweka mishahara ya Wabunge mpaka ya Raisi, Waziri Mkuu, Mawaziri, ma Jaji na wengine watakaoshilikia vyeo vikuu katika nchi. Kusiwachiwe mtu mmoja ama watu kujiwekea mishahara yao wenyewe, italeta watu kutoaminiana na pia chuki kuna namna ya Raisi anavyoweka sahihi sheria zikipitishwa na Bunge. Pia tumezungumzia juu yake na tumependekeza kuwa sheria yote ikipelekwa Raisi sharti aipitishe kwa muda wa siku saba kwa mahakama kuu kupata ushauri au sivyo airudishe kwa Speaker wa Bunge aiweze kuiandika hile sheria upya ikiwa pengine kuna jambo ambalo anaona hakukubaliana nalo.

Tatizo lingine ambalo tunalo katika Bunge letu hivi sasa ni tatizo la kitu kinachoitwa quorum. Quorum ni idadi ya chini inayokubalika kisheria ili Bunge liweze kufanya kazi yake kwanza Wabunge wote wa Kenya wangapi hivi sasa? Mia mbili ishirini na wawili kwa sababu tuna mia mbili na kumi waliochaguliwa na kumi na wawili wanaoteuliwa, wajumbe maalum. Unaambiwa wakiwa thelathini tu hiyo ni quorum, yaani Wabunge thelathini wakiweza kusikizana wanaweza kuenda Bunge na wakapitisha jambo lolote, hiyo idadi inaonekana ni ndogo sana kwa hivyo mapendekezo ni kuwa quorum ya Bunge iwe ni 30% asili mia thelathini ya Wabunge wote walioko.

Lugha inayotumika katika Bunge iwe ni lugha ya Kiswahili, Kingereza na sign language kwa sababu ya wale ambao hawawezi kufuata lugha hizo mbili kwa sababu ya ulemavu fulani. Kutakuwa na kamati za Bunge kama vile tulivyo hivi sasa na kazi zake zimepangwa Bunge inayosemekana litakuwa Nairobi, makao yake yatakuwa ni Nairobi na kama nilivyowaambia mamlaka ya kulivunja Bunge tumeondoa mikononi mwa Rais tumepeleka wapi? Tumeipa Bunge lenyewe lijivunje kulingana na utaratibu wake yaani muda wake ukiisha ndiyo ukiangalia kipengele number mia moja arobaini na mbili Article 142 imeeleza Bunge muda wake utakwisha lini na Bunge jipya muda wake utaanza lini. Kwa mfano, ukiangalia Article 142 Sub-Article 5 inakuambia kuwa both houses of Parliament shall stand prorogued on 30th November in every year and the next session shall commence on the 1st Tuesday of February in the next year. Ikifika tarehe thelathini mwezi wa kumi na moja katika ule mwaka wa uchaguzi, Bunge linajivunja lenyewe. Ikifika jumanne ya kwanza mwezi wa pili katika mwaka unaofuata, kikao kipya cha Bunge kinaanza. Kwa hivyo itakuwa ni jambo ambalo linajulikana, hivi sasa tunaambiwa uchaguzi utafanyika, kuna mtu anayejuwa ni lini? Hakuna na hayo ni mamlaka ambayo Rais amepewa.

Jambo lingine ningependa kuwaguzia ukiangalia katika katiba hii kipengele number ishirini na tano kinasema kuwa, yeyote anayeshikilia mamlaka kama vile Commissioner wa polisi, Jaji, Balozi, Mkuu wa sheria, mkubwa wa banki kuu ya Kenya Governer wa Central Bank of Kenya, sheria inasema hapa, “they hold office at the pleasure of the President”. Wanashikilia yale mamlaka kwa mapenzi ya Rais kwa hivyo, anapomfuta yeyote katika hawa huwa anatumia sehemu kama hiyo na unaona kuwa watumishi kama hao wanafanya kazi wakitaka kumridhisha mtu mmoja badala ya kuangalia wananchi. Ndiyo mamlaka hayo yametolewa yamepelekwa Bunge.

Tuingie katika Executive hivi sasa katika wale ambao tunawapa mamlaka ya kutawala nchi kuanzia Rais, mawaziri na wengineo. Tuna watu tulivyopendekeza haya mapendekezo katika katiba mpya walilalamika na kusema kuwa tumemvua mamlaka yote Rais amekuwa ceremonial. Ceremonial maana yake ni mtu tu amewekwa hana mamlaka yeyote, hana nguvu zozote na haiwezekani wala haingii akilini tuwe na Rais, kiongozi ambaye hana mamlaka yeyote la. Bali tu yamepunguzwa na yakawekewa mizani yasikueki ile mizani, kwa mfano hapa utaona ukiangalia kipengele number mia moja hamsini, Article 150 kuna baadhi ya mamlaka aliyopewa Rais, yeye ndiyo kiongozi wa taifa, Head of State, Commander in Chief of the Defence Forces, Chairperson of the National Security Council and the Chairperson of the Defence Council. Ni mwenyekiti wa haya mambo yote. Is a symbol of unity of the nation, yeye ndiyo ishara ya umoja wa nchi and has responsibility to promote and enhance the unity of the nation. Anajukumu la kuhakikisha kuwa kuna umoja katika nchi. Saveguard the sovereignty of the Republic, kuhakikisha uhuru wa taifa la Kenya pia upo, promote and respect the diversity of the people, awe ni mwenye kuheshimu tofauti za watu wa Kenya. Tulipotangulia tuliona kuwa sisi ni tofauti tofauti lakini sote tuko katika nchi ya Kenya.

Kwa hivyo utaona kuwa ana mamlaka lakini mamlaka yake kama sehemu hiyo inavyosema pale mwisho (c), lazima ayatumie mamlaka hayo kulingana na katiba asikeuke katiba, kazi zake zimetajwa katika Article 151 sehemu ya mia moja hamsini na moja, zimeelezwa na pia imeonyeshwa vile ni lazima kila wakati kabla hajafanya jambo lolote aweze kushauriana na baraza la mawaziri yaani Cabinet kabla hajafanya shughuli yeyote.

Kipengele cha mia moja hamsini na mbili kinaeleza majukumu yake kuhusiana na sheria zinazopitishwa na Bunge. Muhimu ni kuangalia kipengele na mia moja hamsini na tatu, 153 uamuzi wowote ambao unatolewa na Rais sharti uwe kwa maandishi na uwe na sahihi yake sio kusema tu mzee alisema, tunataka kama ni uamuzi ametoa iwe kuna mahali unaweza kuonyesha kwa maandishi alisema na yameandikwa na ameweka sahihi yake. Hivi sasa utasikia mtu anasema mzee alisema, ndio alisema kuna mahali imeandikwa na ameweka sahihi yake? Sasa tungependa kuwe na utaratibu kama huo ili kuondoa wasi wasi na watu kutishwa tishwa saa zote kuwa fulani amesema wala hakusema. Ili uwe Raisi una takiwa uwe ni mtu wa aina gani:-

- Uwe ni Mkenya wa kuzaliwa sio Mkenya wa kuja Mkenya kwa kuzaliwa,
- Uwe na umri kati ya miaka thelathini na mitano na sabini, hivi sasa unaweza kuwa Rais hata ukifikia miaka mia moja, kwa hivyo miaka sabini ni wakenya wamependekeza hilo,
- Awe ni mtu mwenye mwenendo mzuri na
- Awe na shahada kutoka katika chuo kikuu kinachotambulika, graduate,
- Awe ni mtu ambaye ameteuliwa na chama chochote cha kisiasa kilichosajiliwa au anaweza pia kuwa ni mtu independent candidate lakini ili kuzuia watu wasiwe wanakimbilia tu mimi ninataka kupigania kiti cha Rais, mimi kesho asubuhi ninaamka kuna mtu asiyetaka ukubwa? Hakuna kila mtu anapenda ukubwa sema kama kuna nafasi kama hii, mimi nitapigania Urais. Ikiwa wewe utakuwa ni independent candidate basi unaambiwa lazima uungwe mkono na watu wasiopungua elfu moja na sio watu wako tu kwa mfano, kama wewe ni Muorma kutoka hapa iwe ni wa Orma tu wamekuunga mkono watu elfu moja la, au watu wa Mkoa wa Pwani peke yao la, Raisi anapotawala anatawala sehemu

moja? Anatawala sehemu moja?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Anatawala Kenya nzima kwa hivyo tunataka Rais ambaye ni popular ambaye anaungwa mkono Kenya nzima kwa hivyo unaambiwa ikiwa wewe ni independent candidate unataka kupigania Uraisi upate kuungwa mkono na watu elfu moja kwa uchache na kupatikane at least kwa uchache watu mia moja kutoka kila mkoa wa Kenya. Kuna mikoa mingapi Kenya? Minane kwa hivyo upate watu mia nane wasiotoka katika mkoa wako halafu waliyobaki watoke katika mkoa wako na kwa jumla wasipunguwe ngapi? Elfu moja ndiyo sasa unaweza kusema Ibrahim Lethome ni Presidential candidate ama Mr. Ali amekuwa Presidential candidate la sivyo huwezi kupigania.

Na kuna masharti hapo ya kuonyesha mtu ambaye hafai kuwa Rais chini yake iko hapo. Uchaguzi wa Rais utaratibu wake umewekwa hapo chini ya kifungo number mia moja hamsini na saba. Muhimu hapa kuona tu nikuwa hivi sasa Rais tunaambiwa ni yupi anyaeshinda ama Raisi anayechaguliwa lazima aungwe mkono na asili mia ishirini na tano ya wapiga kura kutoka mikoa mingapi? Mitano sasa huo utaratibu umebadilishwa, lazima apate kura asilimia hamsini ya kura zote zilizopigwa katika Kenya nzima kwanza hiyo, 50% of all the votes cast kwa hivyo, Kenya nzima kama wamepiga kura elfu hamsini, Raisi anatakawa apate kura ngapi kwa uchace? Elfu ishirini na tano. Hiyo kando sharti ya pili apate kwa uchache asili mia ishirini ya kura zilizopigwa kutoka mikoa minne nusu ya mikoa yote ya Kenya, we want a popular President Rais watu wasiseme huyu ni wa upande fulani na sio wa upande fulani mtu ambaye anaaungwa sehemu kubwa, ikipita itakuwa hivyo.

Raisi anaweza kupigania kiti cha uraisi mara mbili miaka mitano mara mbili yaani miaka kumi. Na akishachaguliwa kuwa Raisi kama tulivyosema kiti kile chake cha kisiasa aachane nacho kwa sababu tanataka Rais ambaye atatawala nchi nzima na asitumie mamlaka yake kuendesha siasa zake za chama chake. Kuna sehemu ya kuonyesha kuwa Rais anaweza kuondolewa through kile tunachoita impeachment kifungu number mia moja sitini na tatu, anaweza kutolewa namna gani kwa sababu tumesema lazima mamlaka yake yatumiwe kulingana na sheria.

Ofisi ya makamau wa Rais, hivi sasa nani anayemteuwa makamu wa Rais, nani anayemchaguwa?

**Audience:** Rais.

**Com. Lethome:** Nani anayemtoa?

**Audience:** Rais.

**Com. Lethome:** Nani makamu wa Rais Kenya hivi sasa?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Nani huyo amesema Saitoti, hakuna hatuna makamu wa Rais hivi sasa na ni kwa sababu ameteuliwa na mtu

ambaye ana mamlaka ya kumteuwa na kumtoa. Nchi zingine utakuta kuwa makamu wa Rais pia hupigiwa kura. Kuna mtu ambaye husimama tunamuita running mate wa President ana simama kupigania kiti cha umakamu wa Rais, anachaguliwa kama makamu wa Rais kwa hivyo mtu kama yule atafanya kazi zake bila uhoga anajuwa wananchi ndiyo waliyemchaguwa katika kiti hicho. Kwa hivyo, tumependekeza makamu wa rais awe ni mtu mwenye kuchaguliwa na qualification zake ziwe kama zile za Rais kwa sababu panapotokea pengo katika kiti cha urais, yeye ndiyo atakaye shikilia pale.

Na Kazi zake zimepangwa chini ya kifungo number mia moja sitini na saba na mishahara yao imepangwa chini ya kifungo mia moja sitini na tisa.

Tuingie katika kitu ambacho ni kipya Kenya ambacho kimependekezwa na wananchi. Ofisi ya Waziri Mkuu, Prime Minister, tunajuwa hivi sasa tunapozungumzia habari ya Executive, tuna Rais, Baraza la mawaziri na Baraza hili la mawaziri alilolichaguwa ni Raisi na hawa mawaziri wote ni Wabunge sasa mapendekezo yetu ni kuwa na haya mapendekezo nitarudia, ni kutokana na maoni ya watu ni kuwa kuwe na Prime Minister, waziri Mkuu ambaye atakuwa ndiye kiongozi wa shughuli za serikali. Rais, yeye ni Mkuu wa nchi yetu anasimamia nchi nzima, umoja wa kitaifa ana majukumu yake.

Prime Minister ndiye atashughulika na mambo ya serikali na mambo ya kisiasa, kwa hivyo the President will be above party politics atakuwa kule juu sana asivunjiwe heshima katika kujiingiza katika mambo ya serikali. Huyo atateuliwa kutoka katika Bunge na atateuliwa kutoka kwa atakuwa ni yule kiongozi wa chama kitakachokuwa na wafuasi wengi katika Bunge, ikiwa anaungwa mkono ama watu wana imani naye katika Bunge, la sivyo anaweza kuchaguliwa hata asiyekuwa kiongozi wa majority party katika Bunge ili awe Prime Minister.

Atakuwa na wasaidizi wawili, two deputy Prime Ministers ambao pia watateuliwa kutoka katika Bunge. Kisha kutakuwa na mawaziri wasiozidi kumi na watano na mawaziri hawatokuwa Wabunge, najuwa hapa mtu atasema ala, watatoka wapi hawa? Watatoka nje ya Bunge, watu watatuma maombi ikiwa wanaonekana wamesikia kiwango kinachotakikana watateuliwa kama Wabunge na kuna sababu mbili.

1. Hivi sasa utakuta anayechaguliwa kuwa waziri ni mjumbe aliyechaguwa kuwakilisha sehemu fulani ama sivyo? Lakini anapochaguliwa kuwa waziri anatakiwa kuhudumia katika hiyo ofisi yake ya waziri, sehemu yake ya uakilishi Bungeni au Kenya mzima?

**Audience:** Kenya nzima.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo utakuta hapa kuna watu wanaumia, ima wanaumia au wanafaidika zaidi. Akiamua kutumia mamlaka yake ya ofisi ya waziri kuwasaidia watu wake, watakuwa wanasaidika kuliko watu wale wengine wasiokuwa na waziri. Akiamua kuwapuuza kwa sababu ya shughuli zake za uwaziri, itakuwa hawana mwakilishi katika Bunge.

Sababu nyingine ni kuwa, tunataka kuchaguwa mawaziri ambao wanaitwa kwa kizungu technocrats, mtu ambaye amesomea

kazi ama somo linalohusiana na wizara yake. Kwa mfano waziri wa afya, awe ni mtu ambaye amesomea na ana ujuzi katika mambo ya matibabu, kuna wakati katika nchi hii tulikuwa na waziri wa afya ambaye alikuwa jemedari mstaafi, amri Mkuu wa jeshi la Kenya akafanywa waziri wa afya sijui alikuwa akizungumza lugha gani na madaktari katika wizara yake.

Tunataka waziri wa fedha awe ni msomi katika mambo ya uchumi, ndiyo mambo yetu hapa Kenya hayaendi sawa sawa ni kwa sababu mtu anachaguliwa kwa sababu ya uhusiano wake na nani? Na ndiyo kila mmoja inabidi lazima apige makofi hata Rais akifanya makosa lazima apige makofi na aonyeshe uso wa kutabasamu mbele ya Rais ili kukitokea nafasi apewe yeye. Kwa hivyo tumesema tunataka mawaziri ambao ni technocrats professionals ambao wamesomea kazi zinazohusiana na wizara yao.

Kwa hivyo watakuwa kumi na watano na hatutakuwa na Assistant Minsiters, tutakuwa na Deputy Minsiters. Kila wizara itakuwa na msaidizi mmoja lakini hataitwa Assistant kama vile sasa, ataitwa deputy, atakuwa na majukumu yake pia na ofisi yake. Jana kuna mtu aliniambia kuna wakati Shikuku alisema, hivi sasa Assistant Minister ni kama popo mnamjua popo?
**Audience:** Eeh.

**Com. Lethome:** Popo si ndege wala si mnyama yuko kati kati, haijulikani yeye ni Mbunge ama ni waziri yuko kati kati. Waziri ana bendera yeye hana bendera lakini anaitwa yeye ni assistant minister waziri msaidizi. Tumependekeza awe ni deputy minister na wasiwe wengi wawe pia ni kumi na watano, hivi sasa utakuta waziri mmoja wasaidizi wangapi?
**Audience:** Wengi.

**Com. Lethome:** Wawili ama watatu. Kipengele number mia moja sabini na nane kinazungumzia namna ambavyo tunataka Wabunge na viongozi kama vile mawaziri, kuna mwenendo fulani ambao tunatarajia kutoka kwao kwa hivyo kuna kitu ambacho tumekiita, leadership code. Leadership code ni muongozo kwa viongozi kuna baadhi ya mambo ambao hatutarajii viongozi wafanye kwa hivyo tumewawekea sheria fulani na lazima wazifuate hizo sheria.

Kama nilivyowaambia mshahara pia ya Prime Minister, Deputy Prime Minister, Ministers, na Deputy Prime Ministers, kipengele ama kifungo number mia moja sabini na tisa vile vile itatokana na commission ama tume tuliyoiita salaries and remuneration commission. Tume ya kuangalia juu ya mishahara na marupu rupu mengine.

Mambo ya Permanent Secretaries, kifungu number mia moja thamanini na moja na ofisi zingine za jamhuri ya Kenya zimetajwa katika kifungu number mia moja themanini na tatu.

Tuingie katika sehemu nyingine ya Judiciary lakini natoa muda wa dakika tano tu kama kuna swali lolote kuhusiana na hayo niliyoyataja bado tuna sehemu kubwa sana, kuna judiciary ambayo hatujataja na mambo ya ardhi na mambo mengine ambayo ni muhimu kuyazungumzia. Dakika tano peke yake ninamuona Bwana Ali mkono uko juu tafadhal.

**Ali:** Asante Bwana Commissioner, yangu pengine ni ukumbusho kwa yale ambayo ulituambia haswa hii inaenda kwa parties na haswa kwa vyama sababu ndiyo wanafanya mambo ya uteuzi. Maudhui ya kwanza ya kukuwa na nomination ni kuwakilisha wale watu ambao hawana uwezo wa kuchaguliwa, maudhui hii imetafsiriwa vibaya sasa imekuwa ni chombo cha kufanyia campaign. Vile mimi nimepata serikali sasa, nitampa nominated MP kutoka region ile ninataka kuomba kura, kwa hivyo mimi ninataka, nomination iende kwa watu ambao hawawezi kujichaguwa iwe ni kabila chache, iwe ni mtu ana ulemavu fulani, nomination clearly katika Katiba iwe defined, iende kwa watoweza kujichaguwa.

Pili, hii role ya Deputy Ministers ni vile Shikuku alivyosema ni kweli, rafiki yangu mmoja ananiambia ile cover, ile cabinet meeting wakati wanapokwenda ministers, assistant minister haoni ngozi ya ile file inakaa namna gani ya waziri yake. Hii ni kama matusi, kwa hivyo iwe a clear thing defined in the constitution, assistant minister awe na role maalum ya kutekeleza katika serikali hii asante.

**Com. Lethome:** Asante sana Bwana Ali maoni yako tumeyapokea na ni mazuri kabisa, hakuna haja ya kumchaguwa mtu anakula pesa za serikali, pesa za wananchi na hakuna kazi maalum aliyopewa ama aliyowekewa ni jina tu Assistant Minister na pia mambo ya uteuzi ni kama alivyosema Bwana Ali, mambo ya nominated members iwe inaangaliwa watu wale ambao hawakuwakilishwa vizuri katika uchaguzi, kweli na ni chombo ambayo kinatumiwa vibaya sana.

**Kassim Dakale:** Mimi yangu nataka unifahamishe ulisema mawaziri watatuma application ndiyo wachaguliwe. Na kutuma ile application vile watachaguliwa, lazima wawe wasomi na kuna sehemu zingine wale watu wenye kusoma hawako na wana haki kuwa na waziri. Sasa watu kama mambo yao itakuwa namna gani?

**Com. Lethome:** Hebu pendekeza unataka namna gani**?**

**Kassim Dakale:** Sasa hapo pendekezo yangu ni ya kuwa waziri..(End of tape 3 side A).

**Com. Lethome:** Asante swali mazuri asante. Abubakar?

**Abubakar:** Asante sana. Mimi ninatoa maoni kuhusiana na National Council. Kwa National Council tunaona kwamba tuna wajumbe sabini ambao wanatakikana kuchaguliwa kulingana na wilaya lakini kulingana na mimi vile ninaonelea ni kwamba, kuna uhasama miongoni mwa makabila kwa hivyo, iwapo hawa hawa makabila kwa mfano, katika wilaya hii ya Tana River kuna makabila ambao kutoka uhuru ianze hawajawahii kumpeleka mtu wao Parliament. Iwapo basi tutatumia hiyo mbinu ya District nzima kuchaguwa mtu mmoja basi wale wale kabila ambao wanamazoea kumpeleka mtu wao Bunge ndiyo wataweza kumpeleka mtu wao tena katika National Council. Hii itazidisha uhasama tukiangalia mfano wa Rwanda vile inavyotokea ya ukabila na hivi majuzi Tana River pia ilikuwa imekumbwa na utatizo wa ukabila.

Kwa hivyo kwa maoni yangu ingekuwa hii National Council katika Affirmative action ambayo imepewa wanawake, hiyo affirmative action ingepewa makabila ndogo ndogo, minority tribes kuliko maanake wanawake hawataleta uhasama katika jamii au hawatachangia katika kupigana kwa watu. Ingekuwa hiyo jukumu unaangalia katika yale yote uliyotuambia katika hii kikao

ya sasa, kwamba wanawake wamepewa umuhimu zaidi, hiyo umuhimu zaidi ingepewa makabila madogo ili nao waweze kutambulika katika taifa, asanteni.

**Com. Lethome:** Asante Abubakar, asante kwa hayo maoni na yamepokelewa. Ningependa sasa swali la mwisho halafu tuendelee kidogo tuingie katika Judiciary.

**Johnson Mburu:** Bwana Commissioner naona hapa nikama tunalemekea kidogo maana..
**Com. Lethome**: Jina?

**Johnson Mburu:** Jina ninaitwa Johnson Mburu. Ninaona tunapopeleka Bunge ama Bunge linapoteuwa wale kumi na wawili unakuta katika uteuzi wao hakuna hata crippled hata mmoja yuko katika Bunge, kwa hivyo ningeona ya kwamba nao wapewe kwa vile wana haki ya kuishi na wana haki ya kupata elimu kama vile tulipofunzwa asubuhi na wana haki ya ki afya, pia nao wateuliwe.

Jambo lingine utakuta kama sector ya jua kali hata Bunge inapokaribia kupitisha budget yake, jua kali sector huwa inadharauliwa ambayo sasa ndiyo inachukuwa jukumu tuseme mtoto akitoka shule baada ya kumaliza shule pengine anaingia katika sector hii ambazo nayo ningeonelea pengine serikali itoe mtazamo wa kuichochea zaidi ndiyo iweze kuvuta watoto wengi wale wanajikalia manyumbani ovyo ambao wanaharibika katika nyanja ambazo hazihisi kama vile tuligusia pengine machokora. Pengine machokora wanaharibika kwa ajili ya kwamba environment ile wametoka ni nzuri lakini kulingamana na ubanisi wa sheria za kiserikali haziwatilii maanani.

Pia jambo lingine ninaona linatubana zaidi ni kama vile jukumu linalopea PS, maana PS ni kama macho ya waziri na anapokuwa pale anaweza kuwa na pendekezo la kuvutia Ministry yake iwe na pato fulani kama vile tax, tuseme kama hii ya hospitalini unaona vile inatukabili ama PSV. Unakuta mwananchi wa kawaida yule lay man hajafunzwa kwamba hii tax itakuwa na faida na wewe na itakuwa na faida kwa serikali maana tunahitaji muendeleo wa kimaendeleo ili tuwe katika muungano mmoja.

Unakuta yule mtu anayoadhirika hapa zaidi ni mwananchi kwa hivyo ningeomba, pengine serikali itoe mtazamo zaidi na iweze kufafanua imfundishe mwananchi kabla kupitisha tax yeyote ili iweze kumadhiri.

Jambo lingine ninapolitoa mtazamo ni kama lile unaona unakuta uchocheza pengine wa kabila, unahusika ama Commissioner ikitoa pengine uchunguzi fulani utakuta wale wale ambao ni wanasiasa ndiyo wachochezi wakuu ambao pengine huwa wanafunikwa na serikali maana huwa ni kama chombo kinatumika cha kuyumbishwa yumbishwa kugonganisha wananchi ambayo hii imetuletea hasara kubwa kupoteza wananchi ambao hawana hatia yeyote. Kwa hivyo ningeona ya kwamba ikiwa ni Mbunge kama mimi ambaye nimetenda kosa lile, nichukuliwe jukumu la kisheria na nipelekwe kwa wananchi wangu wajuwe ya kwamba, ni mimi nilileta lile tengamano ya kuwakosanisha na serikali. Kwa hivyo ningechangia pia tunapotoa mtazamo kama

vile tumezungumzia pengine mtu amepelekwa mahakamani lakini kabla hajatoka mahakamani amepelekwa rumande. Mtu huyu pengine ni mtoto wa miaka kumi na tano na pale ndani ya cell hakuna mtu anayemshughulikia kutoa mtazamo pengine anapata madhara fulani pale ndani ama mama anawekwa pale ndani na wale ma askari walioko pale hakuna hata mama aliyekaribu. Kwa hivyo ningeomba iwe kama sheria police station zote ama courts, kuwe na watu wa kutetea kina mama na watoto maana hawa ndiyo jamii ambayo inaonekana kama ni thaifu na serikali inatoa mtazamo kwa wakati huu kuweza kuwaleta karibu na njia za kimaendeleo maana utakuta pengine vile kama wafungwa wanalalamika kwamba ubakaji katika prison. Nikumaanisha hata ubakaji unaweza kuwa pale katika yale mazingara ambayo ni duni na wewe uko pale hauna uhuru na yule anayekuja kutazama hana ushauri anaweza kuruhusiwa kutoa kwa kabila lako.

Kwa hivyo tunaona kama sisi ambao si wasomi tunabanika zaidi tunapoenda kuona mfungwa pale ama ndani ya cell maana inabidi uongee lugha ambayo inaeleweka na mimi sijasoma pengine Kiswahili. Kwa hivyo kuwe na mtafsiri pale katika station ambaye anaweza kutumia lugha pengine ni Somali anazungumza na huyu kuweza kutafsiri ili yule mfungwa aweze kuwa na uhuru wa kuishi yale maeneo kwa wakati ule. Pia ningetoa mtazamo ya kwamba.

**Com. Lethome:** Malizia tafadhali?
**Johnson Mburu:** Sorry.

**Com. Lethome**: Toa nakuambia toa lakini kwa ufupi tafadhali.
**Johnson Mburu:** Ninapoangalia wakati Rais tumemteuwa ni mkabidhi wa uongozi, naona anabaniza ma District mengine ama province zingine hana zile jukumu la kutembelea na kuchukuwa maoni katika mazingara tofauti tofauti si kama vile Tanzania utakuta Rais yuko na uhuru hata anachukuwa maoni katika mashule, anakaa na mazingara ya machokora kujibu mashtaka kuwafanya uhuru. Kwa hivyo ningeomba sheria itumike ya kwamba, Rais atakapoteuliwa awe na haki ya kugawa ama kutembelea District kisawa sio apendelee upande mmoja ama province moja kama vile ilivyo sasa. Utakuta kama sisi watu wa Tana River tumesahaulika sana miaka mingi hata kumuona Rais inakuwa wale wameinukia hawajamuona Rais lakini wanasikia yupo. Kwa hivyo awe na uhuru wa kutembelea wananchi wake, District ama tabaka yeyote wakati wowote ni asante Bwana Commissioner.

**Com. Lethome:** Asante Bwana Johnson. Sasa tuingieni katika chombo kingine ambacho ni muhimu sana, tumeangalia chombo ambacho tumekiita Legislature ambayo ni Bunge, kazi yake ni kubuni sheria na kuweka siasa ya serikali. Tuna Executive ambao ni wasimamaizi wa kuendesha shughuli za idara ya serikali sasa chombo kingine ambacho tulichonacho ni chombo ambacho hutumia sheria kuhakikisha kuwa kila mmoja anapata haki yake ndiyo tunakiita Judiciary. Judiciary ndiyo koti za nchi ambazo inasimamiwa na wanasheria, imeanzia katika kifungo cha mia moja themanini na nne.

Hivi sasa tunajuwa ukiangalia koti zetu iliyo juu zaidi tunaita Court of Appeal, mahakama ya rufani kwa Kiswahili. Chini yake tuna mahakama kuu, High Court halafu chini yake tuna zile tunaziita surbordinate court za magistrate. Nafikiri hata Hola ni

Magistrates court ama sivyo? Naam, tumeona kuwa hizi mahakama hazitoshi kutekeleza majukumu, utakuta kesi zimerundikana muda mrefu, kesi pengine hazifanywi inavyotakikana kwa hivyo tumewasikiza wananchi na tukaweza kuangalia nchi zingine zinavyofanya kazi na tumependekeza yafuatayo:-

- Juu kabisa kuwe na korti inaitwa Supreme Court, mahakama kuu. Ilikuwako pale mwanzo.
- Halafu chini yake tutakuwa na Court of Appeal, mahakama ya rufani,
- Halafu chini yake High Court,
- Baada ya High Court tutakuwa na hizi mahakama za magistrate, ikiwemo mahakama ambayo inahusiana na sheria za Kiislamu ambayo inaitwa Kadhis' court.
- Kisha tutakuwa na mahakama zingine ambazo tunaita tribunal ambazo zitakuwa zikifanya kazi kulingana na vile sheria ya Bunge itakavyotaka zifanye kazi.
- Kisha tunajuwa kuna mahakama za kitamaduni, wa Orma kwa mfano kimila mna mahakama zenu ama hakuna, kuna korti za kimila? Usikatae kijana bwana wazee saa hizi wananiambia iko, hakuna kabila ambalo halina bwana. Kwa mfano ki-Orma zamani mtu akiiba ngombe wa mtu mwingine hakuna vile wazee walivyokuwa wakikaa wanakata shauri?

**Audience**: Hata waleo iko.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo hasa maswala yanayohusiana na mambo ya kifamilia na mengine yanaweza yakahukumiwa ikiwa kutakuwa na mahakama za kimila kama hizo. Kama Wameru wana yao inaitwa *Nchuri ncheke*, na Wakamba wana yao pia, waluhya juzi nimetoka Bungoma wameniambia wana yao na mimi ninajuwa hasa wa Orma yao ni very organized. Inasemekana kwanza wa Orma ama wale wote wanazungumza lugha ya ki-borana yao ni more organized katika East Africa yote hakuna ambayo ni organized kuliko yao lakini itakuwa na mamlaka kulingana na vile sheria itakavyoamua sio katika kila jambo.

Kisha kuna kitu ambacho husumbua watu wengi sana, independence of the judiciary. Uhuru wa mahakama, uhuru wa korti ama uhuru wa yule Jaji ambaye anakusikiza kesi yako.Utakuta sehemu nyingi wananchi wanalalamika na kusema kuwa korti huwa zinapendelea upande mmoja kwa mfano hii leo, mzee wewe ukiwa na kesi na waziri muende kortini unaona uamuzi utalalia upande gani, utampendelea nani? Mara nyingi utakuta yule ambaye anacheo katika serikali ama sivyo au mtu mwenye mamlaka utakuta mahakama zetu hazina uhuru au hata ikiamua kesi kwa uadilifu utakuta watu wakilalamika tu ah amempendelea yule kwa nini, yule si ni rafiki ya waziri fulani na waziri yule si yuko karibu sana na President na President si ndiyo mwenye kuchaguwa ma Jaji ama sivyo watu wanavyosema?

Kwa hivyo tunasema korti ziwe na uhuru zaidi kifungu number mia moja themanini na sita na ndiyo sababu tukasema pale mwanzo uteuzi umetolewa mikononi mwa Rais umepelekwa Bunge. Kwa sababu Bunge ndilo linalowakilisha wananchi wote. Kwa hivyo, kutakuwa na chombo ambacho tunakiita Judicial Service Commission ambayo itakuwa na jukumu la kuteuwa ma Jaji na pia tumetoa muelekeo kuhusu Jaji akishachaguliwa atakaa pale kwa muda gani, au akiondoka yule Jaji Mkuu, ni nani atakayeteuliwa kuchukuwa mahala pake?

Hivi sasa tunajuwa kuwa alipotoka Chesoni, alichaguliwa Chief Justice yupi? Anaitwa nani Chief Justice?

**Audience**: Bernard Chunga.

**Com. Lethome:** Bernard Chunga. Alikuwa Jaji wa mahakama gani kabla hajachaguliwa? Utakuta yeye alikuwa yeye ni Prosecutor, alikuwa ni director wa prosecutions. Ameteuliwa akawekwa pale, watu hawakutarajia kulikuwa hakuna utaratibu wa kuonyesha ni nani anayefaa kuchaguliwa kuwa Jaji Mkuu. Kumetolewa utaratibu wa kuonyesha kuwa akiondoka Jaji Mkuu chief Justice, basi anayeteuliwa kuchukuwa mahala pake lazima awe the senior most Jaji katika hiyo korti. Yule ambaye ni wa kiwango cha juu kabisa ndiye anayeteuliwa kuchukuwa mahali pa huyo aliyoondoka ili kusitokee uhasama na kuweze kuwa na uhuru zaidi katika hizi korti.

Kisha kila korti itakuwa ikifanya kazi gani, imepangwa hapa na ningependa moja kwa moja tukaangalie juu ya mahakama ya Kadhi, kadhis court; ama umri wa ma Jaji kabla sijaenda katika Kadhis court kuna umri wa ma Jaji. Huu ndiyo umesababisha ma Jaji kwenda kortini kutushtaki na kuzuia tusiendelee na kazi, moja katika mambo yaliyowakera sana ni umri. Civil servants wana retire wakiwa na umri gani hivi sasa?

**Audience:** 55 years.

**Com. Lethome:** Fifty-five years, ma Jaji miaka sabini na minne. Tukapendekeza baada ya kuwasikiza wananchi umri wao wa kustafu pia urudishwe chini ufikie miaka sitini na mitano ndiyo malalamishi ambayo mumeyasikia. Kwa hivyo, tumependekeza hapa umri wa Jaji wa kustafu uwe miaka sitini na mitano, akifikisha miaka sitini ana khiari ya kustafu anaweza kustaafu kwa khiari yake lakini akifikisha sitini na mitano analazimishwa kustaafu kisheria anaweza kuongezewa pengine mieze kadha kumaliza kesi alizokuwa nazo katika mahakama yake. Kwa hivyo, hilo ndilo pendekezo ambalo limewekwa na tunapozungumzia habari ya ma Jaji pia inahusu Magistrates na ma Kadhi pia.

Kifungu number mia moja tisaini na tisa kinazungumzia juu ya ma kadhi. Najuwa hii sehemu ikiwa na Waislamu wengine wangependa kujuwa sana kuhusu maswala ya ma kadhi. Hivi sasa nchi nzima kuna ma kadhi na Chief Kadhi mmoja peke yake, ukianza kazi ukiwa kadhi, utakufa ukiwa kadhi tu wewe hakuna kupandishwa cheo ama sivyo? Na ukiingia mahakama ya kadhi mimi ni wakili huenda mahakama za kadhi, utamkuta amepewa chuma kimoja pengine hakikupangiwa kuwa korti, kilipangiwa kuwa store amepewa pale, amepewa kiti chake hapa na karani wake yuko hapo na typewriter ya zamani, wale waliona kesi wameketi hapo na wanaongoja kesi zao kusikizwa wako nje huko kwenye verandah wamewekewa ubao huko ama sivyo? Ama hamjaona hivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Utamkuta Chief kadhi ambaye ndiye kadhi Mkuu, hakimu Mkuu katika sheria ya Kiislamu hapewi heshima inayostahiki kupewa kwa hivyo, tumesema chini ya Katiba mpya lazima wapewe heshima wanayostahili kupewa ma kadhi na

watakuwa katika viwango vitatu.

- Kiwango cha kwanza ni katika District, kutakuwa na mtu ambaye tunamwita Kadhi katika District.
- Kiwango cha pili ni katika mkoa kutakuwa na Senior Kadhi kwa hivyo katika kila mkoa kutakuwa na kadhi ambaye ataitwa Senior Kadhi.
- Katika kila wilaya kadhi ambaye ataitwa District kadhi.
- Kisha kutakuwa na Chief Kadhi ambaye atakuwa ni kiongozi wao wote.

Kiwango cha District Kadhi kitakuwa ni sawa na wale ambao tunawaita Resident Magistrate.
Kisha kiwango cha Chief Kadhi kitakuwa ni sawa na hakimu wa mahakama kuu yaani High Court.
Senior Kadhi atakuwa ni kama Chief Magistrate, ikiwa Chief Magistrate anabebwa na Mercedez na bodyguard kwa nini Chief Kadhi asibebwe nayo. Ni Kadhi pia na anafanya kazi katika idara ya mahakama apewe yale yote wanayopewa ma Jaji wengine.
District Kadhi atakuwa na kiwango sawa na District Magistrate.

Appeal hivi sasa rufani, ukienda katika mahakama ya kadhi na hukuridhika na uamuzi wake ni binadamu yule ama sivyo? Si *maasum* kama vile tunavyosema, yeye anafanya makosa, ikiwa hukuridhika na uamuzi wake hivi sasa chini ya sheria hii appeal yako unapeleka High Court na unapopeleka High court sheria inayotumika pale unaambiwa sio ya Kiislamu infact wengine wenye dharau zao hukuambia Islamic Law is irrelevant at this level. Kuwa sheria ya Kiislamu hapa haifanyi kazi, hilo tumeliondoa baada ya kuwasikiza wananchi na ikawa appeal ikitoka kwa District Kadhi inakwenda moja kwa moja hadi kwa Senior Kadhi katika mkoa. Kwa mfano, Tana River kutakuwa na District kadhi, ikiwa hukuridhika naye katika makao makuu ya mkoa kutakuwa na Provincial Kadhi utapelekea appeal kwake Mombasa, ukiwa hukuridhika na uamuzi wake pia ni mwanadamu pia unapeleka appeal sasa kwa Chief Kadhi atakayekaa chini na ma kadhi wengine wawili.

Ikiwa hukuridhika pia na uamuzi wao ndiyo unaambiwa sasa nenda Court of Appeal, mahakama ya rufani ambako yataangaliwa maswala ya kikatiba na maswala mengine ya kisheria. Kwa hivyo kumetolewa utaratibu huo, kazi walizopewa kama kadhi ni kama vile ilivyokuwa hapo mwanzo kuhusu mambo ya familia, mambo ya ndoa, talaka na uridhi na mambo mengine yanahusiana na hayo na wakaongezewa kuwa ikiwa pengine Waislamu wawili wanadaiyana pesa, wana kesi unahusiana na mambo ya pesa au mu'amala mwingine wowote basi wana khiari pia ya kupeleka wakahukumiwe kulingana na sheria ya Kiislamu. Angalia chini ya kifungu number mia mbili haya yote utayaona.

Uteuzi wa ma kadhi, ma kadhi watachaguliwa na chombo tulichokiita Judicial Service Commission, isipokuwa Chief Kadhi anapochaguliwa lazima wahusishwe Waislamu kuchaguliwa Chief Kadhi. Na ma kadhi wanapoteuliwa kazi zao, ona Ramadhani hivi sasa inakaribia ama sivyo? Katika mizozo ambao tutasikia, utasikia Chief Kadhi ametajwa kuhusu mambo ya kuandama mwezi ama sivyo? Siku ya Idd pia ikifika utakuta, nchi zingine utakuta Kadhi huwa haingilii maswala kama hayo,

hiyo ni kazi ya mtu tunayomuita mufti kunakuwa na *mufti* ndiye mzungumzaji kwa jina la Waislamu ama anayehusika na mambo ya dini.

Kadhi anahusika na mambo ya kortini peke yake, chini ya sheria mpya Waislamu wenyewe wajitafutie *mufti* wakuzungumza maswala ya kidini kabisa, huyu itakuwa kazi yake ni kortini kujaribu kuamua kesi za Kiislamu. Sijui kama mumefahamu kuwa kadhi asiingilie mambo kama hayo, mambo ya Ramadhani mwezi umeandama, haukuandama la, yeye ajihuzishe na mambo ya kesi kortini. Asiwe yeye ndiye mzungumzaji rasmi kwa niaba ya Waislamu. Kuna maswala ya *waqf* mkoa wa pwani tunajuwa kuna mali nyingi sana ambazo zinaitwa *waqf* property, mali ya *waqf* ambayo ilitolewa na watu ili iweze kusaidia miradi ya Kiislamu. Inavyosimamiwa hivi sasa hairidhishi na chini ya sheria mpya imekuwa ma kadhi ndiyo watakao angalia ikiwa kuna mzozo wowote ambao unahusiana na maswala ya *waqf*.

Kuna hiki chombo ambacho nimekirudia mara nyingi sana nimekiita Judicial Service Commission. Chini ya sheria hii, Judicial Service Commission ambayo ina haki ya kuteuwa ma Jaji au kuteuwa wale wanaofanya kazi katika idara ya mahakama, inaongozwa na Chief Justice. Chief Justice huchaguliwa na nani? Nani humchaguwa Chief Justice?
**Audience**: Rais

**Com. Lethome:** Rais, kisha kuna ma Jaji wawili wa mahakama kuu ambao pia huchaguliwa na President. Kisha kuna Mkuu wa sheria huchaguliwa na nani? Na President. Kisha kuna Chairma wa Public Service Commission ambaye huchaguliwa na nani? Ndiyo unaona independence ya Judiciary imeingia doa, chini ya Katiba mpya tumependekeza Tume hii ambayo inaitwa Judicial Service iweze kuwa na watu wafuatao:-

- Mwenyekiti wake ambaye atakuwa amechaguliwa atakuwa ni Jaji wa Supreme Court ambaye atateuliwa na Rais kisha apitishwe na Bunge,
- Kisha kutakuwa na mwanamke wa Kiislamu ndani yake ambaye atachaguliwa na chama cha Kiislamu chochote kinachotambulikana Kenya,
- Kutakuwa na Mkuu wa sheria ndani yake,
- Jaji mmoja kutoka mahakama kuu,
- Kisha kutakuwa na Jaji kutoka katika mahakama ya rufani,
- Jaji kutoka High Court,
- Chief Kadhi atakuweko,
- Magistrates wawili,
- Mawakili wawili, mmoja akiwa mwanamke mwingine mwanaume. Magistrates pia mmoja mwanamke mwingine mwanaume,
- Walimu wawili wa sheria, mmoja mwanaume mwingine mwanamke,
- Kisha kutakuwa na mwakilishi wa baraza la elimu ya kisheria na

- Mwenyekiti wa Public Service Commission atakuwako na
- Watu wengine watatu.

Sababu ya kuwaweka hawa watu wote ni kuweka balance, kuwe na mtu anayewakilisha university, mtu anayewakilisha High Court, mtu anayewakilisha Waislamu na jambo lingine ambalo nimesahau kutaja hapa imependekezwa japo haikutajwa hapa iko katika report yetu ni kuwa, katika kila korti ya kadhi kutakuwa na mwanamke hatakuwa ni kadhi kwa sababu sheria ya Kiislamu haimruhusu mwanamke kuwa kadhi wala hatakuwa ni msaidizi wa kadhi yaani assistant kadhi bali atakuwa anawasaidia wanawake wa Kiislamu wanapokwenda kortini ikiwa wana mambo wanataka kuzungumza lakini kwa sababu ya zile adabu za Kiislamu, hawezi kuzungumza na mwanaume kuhusu mambo anayoyataka na ni lazima ayazungumze ili apate haki yake. Ama hamkubali kuwa kuna baadhi ya mambo ambayo mwanamke hawezi kuzungumza na mwanaume?

**Audience:** Iko.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo atawekwa mwanamke kukaa pale sio assistant kadhi, kuna wengine wanasema tunamuita assistant kadhi, no, tumesema assistant to the Kadhi. Atakayekuwa anayemsaidia kadhi kusikiza kesi kuhusu wanawake wa Kiislamu.

Kifungu number mia mbili na tano inazungumzia juu ya kazi zitakazofanywa na tume hii ambayo tumeiita Judicial Service Commission.

Sasa kuna kitu ambacho nitazungumzia ambacho ni kipya pia wale ambao wana draft angalieni Chapter Ten, devolution of power. Devolution of power, muhimu sana na ni jipya hili na hapa lazima tufahamu hii kwa sababu tusipofahamu, itakuwa ni sehemu kubwa sana ya katiba mpya ambayo tutakuwa hatujaifahamu.

Neno devolution maana yake ni usambazaji wa mamlaka kwa mfano, mimi niwe ni chief. Nina mamlaka ya chief, ninaweza kuyasambaza mamlaka yangu niyapunguze niwape watu wengine ili waweze kuendesha kazi ile ile ambayo mimi ningeendesha lakini wawe karibu sana na wananchi. Badala ya kuwa mamlaka yote yako Nairobi mahali pamoja, tumeyasambaza mamlaka yawe karibu na wananchi chini ya devolution of power, usambazaji wa mamlaka.

Hivi sasa tunajuwa kuwa utawala wote uko mahali pamoja, kuna mtu ataniambia hapana utawala uko kila mahalai kwa sababu kuna ofisi ya Assistant chief hapa. Nje ya ofisi ya assistant chief kumeandikwa nini? Office of who?

**Audience:** Office of the President.

**Com. Lethome:** Na yule Assistant chief amewekwa pale na nani? Mlimchaguwa?

**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome:** Hakuchaguliwa na mtu yeyote na je ikiwa hamkuridhika na kazi yake mnaweza kumtoa?

**Audience**: Hapana.

**Com. Lethome:** Hamwezi kumtoa kwa sababu hamukumweka hamna haki ya kumtoa na ukiangalia matatizo mengi tuliyonayo hivi sasa na baada ya kutembea Kenya nzima kuwasikiza wananchi ni kuwa, governance is very far from the people, utawala uko mbali sana na wananchi. Mambo yote yamewekwa mahali pamoja ndiyo sasa tunataka mamlaka yawe karibu sana na mwananchi awe na uwezo wa kusema anataka kutawaliwa vipi na ndiyo maana utaona ikiweza kupita katiba hii, tutakuwa hatuna idara ambayo inaitwa hivi sasa Provincial Administration itaondoka, hakuna PC, hakuna DC, DO, chief, assistant chief, kuna assistant chief hapa? Itakuwa mamlaka hayo yamekwisha kwa sababu, mamlaka yamepelekwa kwa watu wenyewe lakini watajitawala vipi. Sehemu ambayo hivi sasa tunaita sub-Location itaitwa village na itatawaliwa na baraza ambalo litaitwa village Council.

Village Council itakuwa imechaguliwa na wananchi wenyewe wasizidi watu kumi na wasiwe chini ya watu sita. Kazi yao ni kuangalia nidhamu katika sub-Location. Tunaingia katika sehemu ambayo inatawaliwa na chief hivi sasa inaitwaje? Location kwanza hii sub-Location yenu inaitwaje?

**Audience:** Merti.

**Com. Lethome:** Merti, tuseme katika hiyo sub-Location ya Merti ndiyo tumeita village, Merti itatawaliwa na village Council ya Merti sio sub-chief. Tuingie katika Location mnaitaje Location?

**Audience:** Bura.

**Com. Lethome**: Bura Location. Bura Location iko na sub-Location ngapi?

**Audience:** Mbili.

**Com. Lethome**: Mbili ipi nyingine?

**Audience:** Tagdera.

**Com. Lethome:** Ni Tagdera, sasa unaambiwa tunakuja sasa katika kiwango cha Location kutakuwa na baraza lingine hapa ambalo litaitwa Location Council na itakuwa na wawakilishi wawili kutoka katika kila sub-Location, ile village. Kwa hivyo, Council ile ya tumeiita ya kwanza ni Bura?

**Audience:** Merti.

**Com. Lethome**: Merti na ile nyingine ambayo tumeiita?

**Audience:** Bura.

**Com. Lethome**: Itatuma watu wawili wawili waje katika Location, wataunda Council yao ambayo itaitwa Location Council. Na wale wawili watakaotoka katika sub-Location moja lazima awe ni mwanamke, kisha badala ya chief tutakuwa na mtu ambaye anayeitwa Location Administrator. Huyu ndiyo atakayekuwa anasimamia utawala katika Location, atateuliwa na nani? Hatoteuliwa na mtu, atapigiwa kura na watu wote katika Location kwa hivyo, mtamchaguwa mumpendaye na mumtowe msiyempenda.

Kwa hivyo atakuwa sasa naye anatafuta kura kwa wananchi, afanye kazi kulingana na mapenzi ya wananchi. Tunatoka hapo tunaingia katika District ya Tana River, hivi sasa District ya Tana River iko chini ya idara ya nani? DC, District Commissioner, kutoka wapi yeye?

**Audience:** Hola.

**Com. Lethome**: Aliletwa na nani?

**Audience:** Serikali.

**Com. Lethome**: Yeah, hamkumchaguwa wala hamna haki ya kumuondoa. Baada ya kuwasikiza wananchi tumependekeza yafuatayo:-

- Katika wilaya kutakuwa na baraza ambalo tutaliita District Council na hiyo District Council itakuwa na watu ambao watachaguliwa kupigiwa kura katika ile wilaya na isiwe na watu chini ya ishirini wala wasizidi thelathini. Wao ndiyo watakao shughulikia idara katika District, ofisi ambayo itakuwa ni ya msimamizi wa District ataitwa District Administrator. Atakuwa yeye ndiye msimamizi ya ile District na sio DC.
- Atakuwa pia amechaguliwa na wapiga kura wote katika ile eneo, kwa hivyo, watu wa Tana River District mnataka mtu ambaye atatawala sehemu hii mtachaguwa mtu mnayemtaka nyote mtampigia kura.
- Halafu pia atakuwa na wafanyikazi ambao wataweza kumsaidia pale tunawaita Chief officers ambao watakuwa wamechaguliwa ama wameteuliwa na ile District Council.

DC anaweza kuondolewa na nani leo hii?

**Audience:** Rais.

**Com. Lethome**: Rais peke yake ndiye anaweza kumuondoa, ndiye aliyemteuwa anamuakilisha pale Rais hata mpige kelele sijui huyu anatunyanyasa hafanyi kazi vizuri, unaambiwa nenda unakotaka ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome**: Sasa tumesema Administrator huyu wa District can be dismissed by the votes of an absolute majority of members of the District Council that is supported in a referendum by a majority of those voting in the referendum. Kwa ufupi,

wananchi katika wilaya wanaweza kukaa chini na wakapitisha kura ya maoni ya kusema kuwa huyu hatufai kama mtawala wetu katika wilaya yetu naam District. Hiyo ni District sasa tuje katika province. Provincial headquarters yenu iko wapi?

**Audience:** Mombasa.

**Com. Lethome**: Nani anayewakilisha watu wa Tana River Mombasa katika ofisi ya Provincial Commissioner?

**Audience:** Hakuna.

**Com. Lethome**: Nani? Huyu kijana ananiambia yuko, nani? PC ndiyo anawakilisha. PC ameteuliwa na nani pale?

**Audience:** Na Rais.

**Com. Lethome**: Na Rais, kwa hivyo katika mkoa tumesema kutakuwa na Provincial Council, baraza la mkoa. Baraza hili la mkoa litakuwa linawawakilishi wawili wawili kutoka katika kila wilaya. Coast Province tunajuwa ina Tana River, Kilifi, Lamu, Kwale, Kaloleni, sijui wapi, huko kote, Voi, Taita Taveta, kila moja itatoa watu wawili wawili. Hao watakwenda katika baraza la mkoa ili kuweza kuwakilisha malalamishi au matakwa ya watu ya wilaya ile ambayo ilimtoa yule mtu. Kwa hivyo, wawili wawili kutoka katika kila wilaya watakwenda kuwakilisha wa wilaya yao katika Provincial Council.

Kisha kutakuwa na Executive Committee, kamati tekelezi ya mkoa ambayo itakuwa ni wale District administrators, wale ambao wanasimamia kila wilaya kwa mfano, kama Coast Province ina wilaya tano basi kila Mkuu wa wilaya atakuwa ni mwanakamati wa Executive Committee yaani hakuna jambo ambalo linaweza kutekelezwa katika mkoa bila wao kuhusishwa pia. Kwa sababu watakuwa katika executive committee ya mkoa.

Nani atakayemchaguwa huyu mtawala wa mkoa? Atachaguliwa na Provincial Council, ile baraza la watu wawili wawili kutoka kila wilaya ndiyo watakaokaa chini kisha watamchaguwa mmoja wao awe ndiye muakilishi wao katika mkoa. Utaona kuwa mapendekezo haya yakipita yalivyo hivi sasa, vyombo viwili vitakwenda. Kwanza Provincial Administration, ya pili county Council mabaraza ya miji, kwa sababu kazi wanazozifanya hivi sasa wakati mwingine utakuta zina mgongano kwa hivyo, badala ya kuwa na idara mbili kutakuwa na idara moja peke yake. Kwa hivyo, viti vya Councillors pia vitakuwa hakuna.

Sababu ya kuweka pendekezo hili kwanza tulijiepusha na lile jambo ambalo watu wengi sana walikuwa wanalizungumzia na lilikuwa linatisha pengine kugawanaya Wakenya, majimbo. Kuna watu wengi sana walikuwa wakisema tunataka kujitawala, tunataka kila jimbo lijitawale, rasilmali zilizo katika jimbo fulani ni za hilo jimbo peke yake. Tukaweka idara ambayo inawahusisha wananchi, idara ambayo imewaletea watu utawala karibu lakini pia haikutenga Wakenya kuwa watu watengane. Kwa sababu ukisoma baadaye utaangalia kazi zitakazofanywa na provincial government, hiyo serikali yetu ya mkoa itafanya nini? Ile ya District itafanya nini? Na kuna uhusiano gani baina ya serikali ya wilaya na serikali kuu hasa katika mambo ya rasilmali. Rasimali zigawanywe vipi kwa mfano, sehemu hii ni sehemu ya mifugo, rasilmali kubwa au mapato makubwa yatakuwa ni kutokana na mifugo, jee mapato hayo yatatumiwa vipi, pale pale katika ule mkoa na pia katika kuleta maendeleo

katika nchi.

Kuna baadhi ya rasilmali ambazo hakuna mtu anaweza kudai kuwa hizi rasilmali ni za sehemu hii peke yake kwa mfano, tuna bandari ya Kilindini (end of tape 3 side B). Pia isiwapuuze wale ambao wako pale watu wa Mkoa wa Pwani, wafaidike na sehemu zingine za nchi zifaidike. Ukisoma utaona kuanzia kama sehemu ya mia mbili ishirini na sita imeeleza namna ya kugawanya rasilmali baina ya sehemu hizi tofauti tofauti kama vile wilaya na pia serikali ya kitaifa.

Sehemu ya mia mbili ishirini na saba inazungumzia juu ya inter-governmental relations. Serikali hii ya kijiji, hii ya location na ya district na ya mkoa, na ya nchi, zitakuwa zikihusiana vipi, zitafanya kazi vipi. Kuhusu kazi zitakazofanywa na mabaraza haya yote, nyuma kuna schedule ambayo tunaita Seventh schedule nyuma kabisa, mwisho kabisa. Seventh schedule, number two inakueleza ni kazi gani zitakazofanywa na haya mabaraza District government list, utaona kazi nyingi zinazofanywa na County Council zitakuwa zinafanywa na District government na pia kazi nyingi zinazofanywa na Provincial Administration, ofisi ya Mkuu wa wilaya itakuwa ikifanywa na District government ambaye itakuwa ni serikali iliyowekwa na watu.

Kwa ufupi ni kama kuwa kuna Bunge ndogo katika location, Bunge ndogo katika district, Bunge ndogo katika province. Na Mabunge haya yote yanahusiana pia na Bunge katika taifa.

Maswala ya ardhi Bwana Ali ardhi inaanzia kuanzia kifungu cha mia mbili thelathini na mbili, kuhusu siasa ya ardhi ambayo itahakikisha kuwa kuna usawa na uadilifu katika kugawanya rasilmali hii ambayo ni muhimu sana kuliko pengine rasilmali zote. Ardhi, vita vingi utakuta watu wanapigana ni kwa sababu ya kupigania rasilmali hii ambayo ni ya ardhi. Kuhusu umilikaji wa ardhi imewekwa katika kifungu cha mia mbili thelathini na tatu na aina ya ardhi imewekwa katika kifungu cha mia mbili thelathini na nne na utakuta kuna mahali ambapo tumetambuwa ama kuna mapendekezo kuhusu ardhi ambayo inaitwa communal land ambako ardhi inamilikiwa na jamii fulani.

Kwa mfano jamii ya wafugaji, mtu asiyejuwa mwenendo ya maisha au tabia ya maisha ya mfugaji atakuja hapa akisafiri kutoka pengine Garissa mpaka hapa, ataona ardhi imekaa tupu haina kazi ama sivyo? Wanaweza kuita idle land lakini mfugaji anajuwa hiyo sio idle land ni sehemu ya kufugia mifugo. Na pia ukienda sehemu za Kiambu ama Central Province mtu anagawiwa ardhi acre mbili, inatosha kufuga ngombe wake pale wa maziwa, mbuzi, kuku na kulima pale, lile shamba lake linatosha. Huku kwetu kwa mfano, ukigawia kila Muorma hapa umgawiye acre kumi, inamtosha? Kila Muorma umpe acre kumi inamtosha?
**Audience:** Hapana.

**Com. Lethome**: Kwa hivyo utakuta kuna umiliki wa ardhi ambao tunaita communal land ownership ambao tunasema jamii ya Ki-orma inamiliki ardhi fulani. Kuna title deed ambayo inapewa wasimamizi wa kabila hilo au jamii hiyo ili waweze kusimamia ile ardhi yao. Kwa hivyo, ukiangalia kifungu number 235, inazungumza juu ya maswala haya ya ardhi, tenure of lands na kulindwa ardhi kwa sababu ni sehemu muhimu sana ya rasilmali yetu. Hivi sasa tunajuwa ardhi yote iko katika wizara ya ardhi,

kuna mtu ambaye tunamuita Commissioner of Land, ni mtu mmoja huyu ambaye anasimamia ardhi zote Kenya lakini sasa hapa tumependekeza badala ya kuwa na mtu mmoja lakini kuwe na Tume ambayo itaitwa National Land Commission. Tume ya kitaifa ambayo inasimamia mambo ya ardhi, kazi zake itakuwa ni kama vile zimepangwa hapa chini ya kifungu mia mbili thelathini na saba, itakuwa inasimamia maswala yote yanayo husiana na ardhi katika nchi.

Tuna kifungu kingine ambacho kinazungumzia habari ya mazingara hivi sasa tunakuta watu wengi wanaumia kwa sababu mazingara yetu hayazingatii vizazi vijavyo. Utakuta kwa mfano Nairobi unajuwa kuna mto anaitwa Nairobi River, mshauona huo mto? Unakaaje? Maji yake unaweza hata kutaka kuoshea, hauwezi kutaka hata kuosha nayo chochote kwa sababu mazingara yamechafuliwa au unakuta sehemu zingine kunaweza kufunguliwa kiwanda hapa ambacho kinaweza kuwa kinatoa pengine harufu fulani itawadhuru watu wote hapa. Kwa mfano, hapa kukiwekwa kiwanda cha saruji, cement factory hapa baada ya miezi miwili utakuta karibu kila mtu hapa ana asthma kwa sababu ya vumbi ya lile cement au kuwekwe kiwanda ambacho kinatoa chemicals ambazo zinawadhuru watu na mifugo kwa hivyo hapa tumesema lazima mazingara yaweze kuhifadhiwa au kwa mfano nimekwenda mji unaita Dadaad. Utakuta watu wa Dadaab pale wanalalamika wanasema serikali imeweka makao ya wakimbizi pale katika ardhi yao.

Utakuta malalamishi makubwa ya watu wa pale Dadaab ni kuwa mazingara yameharibika wale watu wamekuja ni wakimbizi wamekuja na mifugo yao, wanamatumizi ya miti, wamekata kila mti pale kumekuwa ni jangwa. Inakuwa mazingara yamechafuliwa.

Pia kutabuniwa chini ya kifungu mia mbili arobaini, kutabuniwa tume ambayo itaitwa National Environment Management Commission. Tume ya kusimamia mazingara ya kitaifa na pia kuweza kuchukuwa hatuwa ikiwa mazingara yataweza kuchafuliwa. Maswala ya fedha, matumizi ya pesa za serikali yamewekwa kuanzia kifungu cha mia mbili arobaini na tatu. Namna ya kutumia fedha za serikali na budget iwe inapangwa vipi. Haki za serikali kuweza kukopa pesa pia imezungumzia juu yake. Central Bank of Kenya itakuwa inafanya kazi vipi, yule Governor wa Central Bank atachaguliwa vipi, kisha kuna huyu mtu ambaye hivi sasa anaitwa Controller and Auditor General. Mtu anayesimamia matumizi ya pesa za serikali, hivi sasa ni ofisi moja tumeigawanya ziwe mbili.

Moja anaitwa the Controller of Budgets angalia Artile 253 Controller of Budges. Huyo atateuliwa na Rais hisha uteuzi wake utapitishwa na Bunge na atakuwa ni mtu ambaye ana ujuzi wa kusimamia matumizi ya fedha ndiye atakayekuwa Controller of Budgets.

Kifungu mia mbili hamsini na nne kutakuwa na mwingine tunamwiita Auditor General, ni Mhasibu Mkuu. Kuangalia jee pesa za serikali zimetumiwa sawa sawa kulingana na mipangilio ya serikali au la. Kutakuwa na baraza pia ambalo litaitwa Economic and Social Council chini ya kifungu mia mbili hamsini na saba, hili baraza litakuwa linasimamia maswala yanayohusiana na matumizi ya fedha.

Mambo mengine ni kama vile Prison, tumesema Prison itabadilishwa na itaitwa Correctional Services na unaweza kuangalia sehemu ambayo inahusiana na maswala hayo. Kuhusu mambo ya polisi ambayo tutaita Kenya Police Service iko chini ya kifungu number mia mbili sitini na nne, 264. Commissioner wa Polisi hivi sasa anachaguliwa na nani?

**Audience**: Rais.

**Com. Lethome**: Na kufutwa anafutwa na nani?

**Audience:** Rais.

**Com.Lethome**: Na yeye. Ukiangalia 266 tumempa nguvu zaidi. Tumesema commissioner atakuwa anachaguliwa na Rais lakini lazima uteuzi wake upitie Bunge na atakuwa anachaguliwa kwa amuda wa miaka kumi. Kwa hivyo kabla miaka kumi haijaisha labda afanye makosa hawezi kutolewa na mtu yeyote tunampa kidogo nafasi ya kuweza kufanya kazi bila ya kuogopa kuwa anaweza kuondolewa.

Kifungu mia mbili sitini na saba ndiyo kinazungumzia habari ya Kenya Correctional Services. Maswala ya Prison, Prison iwe ni mahali pa kubadilisha tabia za watu sio mahali pa kuadhibu watu kama ilivyo hivi sasa. Kisha kifungu mia mbili sabini na moja kinazungumzia habari ya ulinzi, defence. Article 271 mtaangalia habari ya ulinzi na tutakuwa na baraza ambalo tutaliita National Security Council, baraza la usalama wa taifa. Atakuweko Rais, makamu wa Rais, Prime Minister, kutakuwa na waziri wa ulinzi, kutakuwa na Mkuu wa majeshi, Army Commander, Navy Commander, Airforce Commander, Commissioner wa polisi atakuwepo, Director of Correctional Services, huyu ndiyo Mkuu wa magereza hivi sasa tunayemwita Mkuu wa magereza, Director of National Security Intelligence. Kuna ile idara ambayo tunaita hivi sasa National Intelligence Services wale watu ambao katika vikao hata katika kikao kama hiki nafikiri kuna mmoja ama wawili kuja kuangalia mambo yanaendeleaje. Wao Mkuu wao pia atakuwa katika National Security Council, kisha kutakuwa na wenye kiti wa kamati ambayo inahusika na ulinzi katika Bunge, Mkuu wa sheria.

Kazi za baraza hili la usalama zimepangwa hapa chini ya kifungu number mia mbili sabini na tatu ili kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata usalama wa kutosha.

Ukiangalia Chapter 16, kuna kitu kinaitwa Leadership and Intergrity, kuna watu ambao kwa sababu ya vyeo vyao lazima wawe na tabia aina fulani ambao tunatarajia kutoka kwao. Kama vile Rais, Prime Minister na makamu wake wawili na mawaziri na makamu wao, wawakilishi wote katika Bunge, wawakilishi katika ma baraza tuliyoyataja hivi sasa kuanzia village Council, location Council, district Council, provincial Council. Hao wote kuna sheria fulani ambazo ni lazima wazifuate. Sheria zenyewe zimewekwa ukiangalia huko nyuma utaona kuna code of conduct ya hawa watu.

Kisha kutakuwa na baadhi ya tume ambazo zitabuniwa na Katiba hii, kwa mfano, kuna hiyo commission moja ambayo ni

muhimu sana ukiangalia chini ya kifungu mia mbili themanini na nane, Article 288 Commission yenyewe itaitwa the Commission on Human Rights and Administrative Justice. Hapa ndipo mwananchi anapoweza kuenda kulalamika ikiwa haki zake za kimsingi zile tulizosoma chini ya sura ya tano, Chapter five, fundamental rights zimevunjwa basi anaweza kupelekea tume hii malalamishi.

Kuna tatizo lingine sijui hapa kama mnalo, kuna watu ambao tangu tulipopata uhuru wamedhulumiwa sana. Wengine watu wao wameuawa, mali zao zimepotea na mpaka sasa haijajulikana haki iko wapi. Ni jukumu la hii tume chini ya Katiba mpya kuweza kuangalia haki za watu zilizo thulumiwa waweze kurudishiwa haki zao na ukiangalia chini ya hicho kifungu 288 sub-article 3, VII, inasema 'the Commission shall take step to secure appropriate redress where human rights have been violated'. Tume hii itakuwa na jukumu la kuchukuwa hatuwa zinazofaa za kisheria mahali ambapo haki za kibinadamu zimefunjwa ama zimekeukwa. Kwa hivyo kuna tume nyingi ambazo zitabuniwa chini ya Katiba mpya.

Kuna sehemu ambayo ni muhimu kabisa lazima tuiangalie, hivi sasa tunaiita hii Katiba a people driven constitution. Katiba ya wananchi wa Kenya, tunaipeleka Bungeni, tuna hakika gani kuwa Bunge halitakaa chini lipitishe mabadiliko kama vile hii ilivyobadilishwa. Hii Katiba tulipewa mwaka tisaini na tatu, unaambiwa baada ya mwaka mmoja tu karibu nusu ya vifungu vyake vilikuwa vimebadilishwa na Bunge, kufikia sasa imebadilishwa mara thelathini na nane, 38 years in thirty nine years. Sisi tangu tupate uhuru miaka thelathini na tisa, imebadilishwa mara thelathini na nani. Bunge lina haki ya kupitisha kuna kifungu hapa tunasema, thuluthi mbili, two-thirds ya Bunge wanaweza kupitisha mabadiliko yeyote katika Katiba sasa tunajisumbuwa tumezungunka kuchukuwa maoni ya watu, pesa nyingi za serikali zimepotea, pesa za umma zenu nyinyi zimepotea kulipa Commissioners na nini, kutengeneza katiba mpya halafu baada ya muda mfupi Wabunge waweze kuibadilisha wanavyotaka.

Tumeweka ni kitu gani kinacho hifadhi katiba hii isiwe ni yenye kubadilishwa ovyo ovyo. Angalia kifungu number mia mbili tisaini na nne, Article 294 imetoa mamlaka kiasi fulani kwa Bunge kuweza kubadilisha baadhi ya sehemu ya Katiba hii lakini kuna sehemu ambazo ni za msingi sana haina haki za kubadilisha sharti Bunge lipate maoni ya wananchi wenyewe. Kwa mfano, katiba hii ukiangalia nyuma huku mwisho kabisa, utaona kuna hesabu zimewekwa kuhusu mipaka ya Kenya, the territory of Kenya. Ushaona huko nyuma kabisa, ukiangalia huko nyuma ikiwa ni mpaka ya Kenya na Somalia uko mahali fulani imepitia mahali fulani, imewekwa nukta nukta. Mipaka yetu yote imetajwa katika katiba mpya, hii katiba ya zamani haikutaja territory ya Kenya iko wapi, mpaka wa Kenya uko wapi.

Unaonaje jee Bunge likikaa chini lianze kupitisha sheria ya kusema tumebadilisha mpaka wa Kenya, mpaka wa Kenya na Somalia ni Tana River hapa. Hakuna mtu atakuwa na uwezo wa kusema la, kwa sababu ni Bunge tumelipa uwezo wa kubadilisha. Kwa hivyo, tunasema Bunge lina uwezo wa kubadilisha katiba kwa kupata thuluthi mbili wanaounga mkono katika Bunge lakini, kuna baadhi ya vipengele ambavyo ni muhimu sana, hawawezi kubadilisha mpaka wapate maoni ya wananchi through a referendum. Kwa mfano, ukiangalia kipengele number mia mbili tisaini na nne Article 294 sub-Article 3, hizo ndizo sehemu ambazo Bunge haliwezi kubadilisha. Kwa mfano:-

- Mipaka ya Kenya,
- Uhuru wa wananchi wa Kenya,
- Mambo ambayo ni muhimu katika Kenya,
- Philosophia ya Kenya,
- Haki za kimsingi za binadamu kwa mfano tumesema, katika haki ambazo unapewa na katiba ama zinatambuliwa na katiba, katiba haikukupa imetambuwa tu, ni kuwa wewe kama mwananachi una haki ya kumiliki mali mahala popote katika nchi hii. Wabunge wakae waseme no, tunapitisha sheria sasa tunabadilisha hiyo sehemu na kusema huna haki ya kumiliki mali mahali popote katika nchi ya Kenya. Itakuwa imevunja haki ya msingi, tunawaambia no, mpaka tupate maoni ya wananchi wote.
- Au haki ya kusema kuwa elimu ya bure ya msingi ni haki ya kila mtoto. Wapitishe Bunge no, tunaondoa hicho kifungu no, kuanzia sasa sio haki ya kila mtu ni haki ya matajiri peke yao. Tunawaambia hakuna mumekeuka mipaka yenu mumepita mipaka mpaka mpate maoni ya wananchi ama mambo ya uraia lazima yapitie kwa maoni ya wananchi. Kwa hivyo, kuhusu ubadilishaji wa katiba kifungu mia mbili tisaini na nne, mia mbili tisaini na tano, mia mbili tisaini na sita, imepangwa hapa kuweka vikwazo.
- Kisha kuna kitu tunachoita interpretation, ufafanuzi, tunapozungumzia juu ya mtu ni nani? Tunazungumzia juu ya chama cha kisiasa ni kitu gani? Tunapozungumzia juu ya mahakama tunakusudia nini? Interpretation ziko katika Chapter 19.
- Kisha tunakitu ambacho tunaita Transitional and Consequential provision. Mambo ambayo yatafanyika baina ya sasa na mpaka katiba mpya iweze kupatikana yamewekwa katika kifungu mia mbili tisaini na nane, mia mbili tisaini na tisa, kuendelea mbele.

Ukiangalia sasa baada ya hapo mipaka ya Kenya yote imepangwa, katiba hii haikupanga mipaka ya Kenya kwa hivyo, imewacha mipaka ya Kenya hivi kwamba inaweza kunyakuliwa na mtu yeyote mahala popote au kubadilishwa na mtu yeyote. Katiba mpya imependekeza kuwa ni lazima kuwe na mipaka ambayo imetajwa katika katiba, kila sehemu imefikia wapi, imepitia wapi. Wanaosomea elimu ile ya survey wanajuwa, kwa mfano, ukiangalia hapo unaambiwa, mpaka wa Kenya na Uganda umeanzia wapi? Unaambiwa umeanzia katika maji ya ziwa Victoria on the pararrell 1 decree south latitude, kuna mstari ambao unaitwa latitude ambao umepitia sehemu fulani mpaka sehemu fulani kusini mpaka mwisho wake kwa hivyo, mipaka ya Kenya pia imehifadhiwa sasa chini ya katiba mpya isiwe ni kitu ambacho kinaweza kubadilishwa na mtu yeyote anavyotaka. Kuanzia hapo mpaka mwisho ni kuhusu mambo hayo na mambo mengine ambavyo utajisomea mwenyewe ni kama vile viapo mtu akichaguliwa kuwa Rais ni kiapo gani ambacho anatakiwa asome.

Kama mtu amechaguliwa kuwa waziri, waziri Mkuu, makamu wa waziri, Jaji na mtu mwingine, hayo ni mambo ambayo yametajwa huku nyuma. Na pia kuonyesha kwa mfano tumependekeza katika wilaya kutakuwa na serikali mpya, kutafanyika nini sheria mpya ikipita na kuna DC, yule DC aende wapi siku hiyu? PC aende wapi siku hiyu? DO, Chief na assistant chief waende wapi? Yote yameandikwa hapa kutafanyika nini baada ya sheria mpya kuweza kupitishwa na kuwa ndiyo katiba ya nchi.

Kwa mfano Provincial Administration imeandikwa moja kwa moja, sheria mpya ikipitishwa tu, moja kwa moja Provincial Administration inaondoka ukiangalia ni number seven under- I don't know what page it is in the magazine, lakini kule mwisho mwisho utaona imeandikwa kuwa, 'on the coming into force of this constitution, the system of administration comprising sub-chief, chief, DOs, DCs, PCs commonly known as the Provincial Administration shall stand dissolved.' Zitakuwa zimemalizika hapo hapo waondokee wale wanaochaguliwa na wananchi waweze kufanya kazi.

Kisha unaambiwa watumishi wote wa umma ambao watakuwa wanafanya kazi chini ya idara hiyo ya Provincial Administration, basi itabidi waende kwa Public Service Commission waweze kupelekwa katika sehemu zingine za serikali kuweza kufanya kazi. Kwa hivyo ndugu zangu ningependa kuwaambia kuwa vile vile tulivyoanza kwa kusema kuwa, hii si sheria mpya ni mapendekezo, draft. Ni mapendekezo hayajawa sheria na wala hayatakuwa sheria mpaka yapitie kwenye utaratibu wa kwanza ni kongamano la kitaifa National Conference ambayo itaanza tarehe ishirini na nane Bunge lisipovunjwa mpaka tarehe ishirini na nane mwezi wa kumi na moja, kisha baada ya hapo ipelekwe Bunge ndiyo tutakuwa na Katiba mpya kabla ya hapo haya ni mapendekezo. Yanaweza kuongezwa au kupunguzwa ndiyo sababu tumesema lengo letu la kuja hapa ni kuwahamasisha muendelee na mjadala kuhusu katiba hii au mapendekezo haya. Toeni mapendekezo yenu, mna yule ambaye ni muwakilishi wetu kupitia kwake mnaweza kutupitishia mapendekezo yenu ambao pengine mnaona yamewachwa kama vile alivyosema Bwana Ali, anaona kuwa jamii ya wafugaji haikutajwa wazi wazi katika mapendekezo haya, tumechukuwa.

Huyu Bwana Johnson ametoa mapendekezo yake na yule mwingine pia ametoa mapendekezo yake, yote tumeyachukuwa na yatatiliwa maanani. Kwa hayo machache ningependa kukomea hapo hivi sasa nitatoa nafasi chache sana za maswali tafadhalini halafu tuweze kufunga kikao tuna safari ya kuenda hadi Nairobi.

**Adam Ibrahim**: Mimi kuna swali yangu ni kuna ardhi ambaye hapo awali zilinyakuliwa, wakati wa ubeberu na wakati hii ambayo serikali yetu imekuja kutawala. Na hii ardhi ilikuwa ni ya jamii fulani na hiyo ardhi sasa hiyo jamii imenyakuliwa na hawapati faida yeyote kutoka hiyo ardhi, tuseme kama Kora, ama Tsavo, kuna mahali ambayo wananchi wakati wa mbeleni walikuwa wanakuja tu kuhamishwa bila kushauriana nao. Na kwa vile sasa imekuja katiba na wananchi wenyewe waunde, je mambo kama hayo hii katiba kuna kitu ambayo mumeguzia?

**Com. Lethome:** Lile ambalo ningependa kukuambia ni kuwa japo kuwa haikutajwa wazi wazi vile ulivyotaja wewe lakini kuna tume ambazo zimeundwa kuweza kuchunguza ni dhulma gani ambazo zilitokea na kuweza kuangalia hizo dhulma zinawezaje kuondolewa na bila shaka miongoni mwa hizo dhulma ni kama ardhi ambazo zilichukuliwa bila haki kuweza kurejeshewa wenzao, itakuwa ni majukumu ya hizi commission ambazo tumezitaja hapa.

**Adam Ibrahim:** Kwa hivyo haya malalamishi kama yako tukiweza kupeleka kwa hiyo commission wakati hii katiba itapita inaweza kufwatiliwa?

**Com. Lethome**: Ni lazima ifuatiliwe

**Kesana Godana**: Mimi ninasema mila ya watu Kadhi anaweza kufuta?

**Com. Lethome**: Mila ya watu?

**Kesana Godana**: Eh, kadhi anaweza kukataa?

**Com. Lethome**: Kadhi?

**Kesana Godana**: Na iko sheria ndani?

**Com. Lethome:** Unaniuliza swali mimi?

**Kesana Godana:** Eh.

**Com. Lethome**: Haya asante basi keti nitakujibu. Mzee anauliza Kadhi anaweza kukataa mila ya watu. Sasa kadhi anatumia sheria gani kuhukumu watu? Sheria ya Kiislamu ama sivyo? Sasa ningependa kukuambia hivi, sheria ya Kiislamu inatambuwa mila, imepinga zingine na zingine imekubaliana nazo. Sasa ikiwa ile sheria inakwenda kinyume na sheria ya Kiislamu, Kadhi ataikataa kwa sababu yeye anahukumu kulingana na sheria ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mila imekataana na sheria kwa mfano wewe sasa, ama sivyo, wewe ni Muislamu ama sivyo na ni Mu-orma ama sivyo? Kuna baadhi ya mila za ki-orma ambazo zinapingana na sheria ya Kiislamu iko?

**Audience:** Iko.

**Com.Lethome**: Sasa zikigongana unafuata gani ya Kiislamu ama ya ki-orma? Ninakuuliza kwa mfano mimi nitakuambia yangu sasa. Mimi ni Maasai si ndiyo, mila ya ki-Masaai inasema nikienda kuposa msichana ninataka kuoa lazima nimpelekee baba yake mtungi wa pombe, sheria ya Kiislamu inasema nini kuhusu mambo ya pombe?

**Audience:** Haramu.

**Com. Lethome**: Sasa nitafuata gani mila ama sheria ya Kiislamu?

**Audience:** Sheria ya Kiislamu.

**Com. Lethome:** Nitafuata sheria ya Kiislamu.

**Kesana Godana**: Sasa yaani desturi ile mimi ninasema sasa kama ndugu yako amekufa, bibi iko na watoto na wewe unataka kutunza halafu kadhi anachukuwa mkono yako anapatia mtu mwingine na watoto anabakisha kwako.

**Com. Lethome**: Sasa unajuwa ungesema wazi wazi unataka kuoa bibi ya ndugu yako. Nitakujibu unajuwa umepita kando huko ungekuja hivi straight sasa haya ni mambo ambayo tumepata sehemu nyingine mpaka inaitwa widow inheritance kumridhi mjane wa ndugu yako. Kwa sababu unataka kuhifadhi watoto ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa unataka kumuoa yule mke wa ndugu yako ndiyo uhifadhi watoto ama sivyo? Sasa unataka kumuoa kwa nguvu ama kwa hiari yake?

**Audience:** Kwa hiari yake.

**Com. Lethome**: Kwa hiari yake. Sheria ya Kiislamu inasema 'una haki ya kumuoa kwa radhi yake mwenyewe kwa mahari nyingine na *nikah* nyingine. Na anahaki pia ya kusema mzee sitaki kuolewa na wewe nataka kuolewa na mtu mwingine wa nje, ana haki hiyo pia. Na wewe una jukumu ya kuangalia watoto wa ndugu yako pia, sasa hapa Kadhi hawezi kumlazimisha aolewe na wewe wala hawezi kumkataza kuolewa na yule mtu wa nje na hawezi kumlazimisha kuolewa na mtu yeyote mwingine. Hiyo ndiyo sheria inavyosema hivyo mzee.

**Kesana Godana**: Sasa yeye.

**Com. Lethome**: Ama wewe uniambie unataka namna gani?

**Kesana Godana**: Hapana. Mimi ninataka, sasa watoto wakati yeye anampa mtu mwingine, tena watoto wananidai na watoto wanazaliwa kwa nikah, sitaki tena. Sheria hii iko watoto wananidai mimi na walizaliwa katika nikah?

**Com. Lethome**: Wadai kama mali ya ndugu yako iko, mali ya ndugu yako iko wapi?

**Kesana Godana**: Mali yake anasema hakuna mali yake nilipata na watoto wananishtaki wanasema hata watoto anampa bibi.

**Translator:** *Afsomali kuxathal maxatiri?*

**Kesana Godana:** *Maxawaye yacni waxa dintey wilkain, athiga iyo cilmaxaga awougi bataxai athi, cilmixi inath dacaleysatith aath rabta. Nakti yaa xathan abexethi ya ninkale kutharsathey, xathu ninkale kutharsathey cilmixi ba xathan lagugu xisabtey laguyiri cilmixi anale xathana. Sherecatha machirta xathi cilmixi nikah kudashen oo cilmixi mitka uyar sathax yir ki kale shan chir uu yaxai. Cilmixi na nakta walasisey oo lakushitakey oo summons lagugoyey oo kis lageye oo xathava kiis an damanini. Maya masruf xathu yaxai wa laacrki maogtaxai, uxuba yiri cilmaxa ana daley. Shercethasa tala xatha Hola, haya naag oo atho kuchirto sheric Mohamediya onan ninki dintey shan iyo tovan asho kabaryin sherci machira oo lagu nikaxo xathana? Nag shan beri kelix laga digtey oo xathan sheri lagu nikaho machira sherciga Mohamediya?*

**Com. Lethome:** Kwanza ile ya pili baada ya siku tano tu amefanya nikah nyingine ni harambu, lazima anakaa eda anamaliza eda halafu ndiyo anaweza kuolewa na mtu mwingine. Ndiyo sasa tumeweka sheria kama haujakubali ile uamuzi ya kadhi iko appeal. Unaweza kwenda appeal ingine na ile sheria ya mama kukaa na watoto, wale watoto ni wake amezaa yeye ako na haki ya kukaa nao. Baba akishaondoka ile mtu yuko karibu sana na watoto ni mama ya watoto, sasa sheria inasema akae na

watoto labda kama anadhulumu wale watoto na wewe kama ni watoto wa ndugu yako unawaangalia pia sio lazima umuoe yule mama kama hataki wewe umuo wacha aolewe mahali ingine lakini uangalie watoto.

**Kesana Godana:** Kama yeye anasema ingine ya watoto kweli lakini hapana sema na sitaki kuanza wakati sheria inafika kila kitu mimi ninachukuwa kwa sheria.

**Com. Lethome**: Basi hiyo maneno chini ya sheria mpya tutaangalia. Johnson?

**Johnson Mburu**: Ningetaka utufafanulie ama utuele kama kuna sheria inayotumika ya kuweza kuwa na ile haki ya kwamba kama sasa mimi nimeenda zangu America, nimeenda pengine kwa muda wa miaka mitatu na hapa nchini kuna uchaguzi wa kura nina haki ya kufanya uchaguzi wangu nikiwa America kwa hapo? Maana Kenya ndiyo wanachaguwana na mimi ni mwananchi wa Kenya, sijakuwa citizen wa America je kuna njia gani ambayo inaweza nichangia mimi nikiwa kule nifurahikie ama nijumuike na jamii yangu nchini Kenya.

**Com. Lethome**: Pendekeza?

**Johnson Mburu**: Mimi ningependekeza hivi, kwa vile haki inamlinda mwananchi yeyote katika nchi na yeye yule alienda kule ngambo ameenda kwa muda mfupi kwa hivyo apewe na yeye fursa ya uchaguzi, tusema kama ni Rais wake ni Mbunge wake, apewe fursa ama mbinu fulani kupitia Balozi aweze kupitia Balozi wa kule kama vile wa America wanavyofanya katika maBalozi zao nje.

Pia kuna jambo lingine pia linanitatiza hapa Bwana Commissioner kama vile tuna gharamika zaidi hasa kwa ndugu wetu viwete siku ya kuchaguwana unaona amekata card ya kura ana kitambulisho cha kura na ana card kama kawaida, lakini siku ya uchaguzi, kila mtu anajawa na hofu maana huenda kukabadilika kukawa na fujo pahala kwa hivyo yule kiwete hapati ile haki ya kuchaguwana. Kama hakuna sheria ningependekeza hivi, yule kiwete awe na mbinu ama iwe katika eneo kile kuwe na mtu kabisa wa kuangalia kama kuna viwete nao wapewe jukumu la kuanza uchaguzi.

Ninaona pia kuna ubamizi pengine wakati wa siku ya kufanya kura, maana unaweza kukuta mimi ni kama Mbunge wa hapa na ninaupinzani na vyama vingine tofauti unakuta kwa vile serikali inachochea mimi nichaguliwe, siku hiyo vijana wote wanapewa makazi ya ukarani na wanapelekwa mbali mbali. Unakuta zile haki zao wangeweza kuchaguwa katika yale maeneo huwa hazimulikwi, hazitolewi mtazamo kwa hivyo, ningependa ya kwamba ikiwa kutakuwa na uchaguzi yule karani anayeenda kutoka Bura ameenda Bokra apewe nafasi ya kwanza achaguwane kwanza pale. Maana hivi kura nyingi unaweza kukuta percent fulani inapotea maana inayumbishwa bishwa njia ya kwamba, yule anayetakikana na serikali achaguliwe.

So hupewa hii nafasi vijana wakapoteza haki zao kwa hivyo ningeona ya kwamba kutafuta ama utupe mwangaza ama sheria ya kumuweza kumpata haki yeye ya kuchaguwana. Ni hayo tu, Bwana Commissioner.

**Kassim Dakane Kunow:** Mimi yangu ni ya kuwa hii National land Commission vile ulisema wao wanachaguliwa na Commission yenyewe. Sasa wanachaguliwa na commission au wanachaguliwa na..

**Com. Lethome**: Wewe pendekeza?

**Kassim Dakane Kunow**: Sasa mimi vile nilikuwa ninataka kupendekeza hawa watu wa National Land Commission wawe wakichaguliwa kutoka kwenye district. Kwa sababu wakichaguliwa kutoka Nairobi hatuna faida yeyote tuko na wao.

**Makka Abothole:** Mimi ninarudia pale pale kwa kadhi.

**Com. Lethome**: Jina mama?

**Makka Abothole:** Mimi ninauliza hapa kwetu bibi na Bwana wakikosana, bwana sana sana anamuambia bibi, *'xakkan kanke matta isinkedi'* sijui Kiswahili nitasema nini? Sasa sisi tunataka hiyo sheria iwe hakuna kwa sababu mwanamke hana uwezo wa kununua ndoa. Ikiwa wamekosana kama kosa ni kwa Bwana ama ni kwa bibi lakini bwana kwa vile yeye hana kitu anamuambia bibi *xakkan kanke matta isinkedi* hiyo kwa sheria ya Kiislamu iko ama ni mila ya hapa? Na kama iko iondolewe.

**Com. Lethome**: Kwanza mama ninataka nikuambie kitu kimoja ujue unapokuwa Muislamu unakubali amri ya Mwenyezi Mungu na sheria ya Kiislamu imetoka kwa Mwenyezi Mungu kwa hivyo hatuwezi kusema iondolewe ama iwekwe, ni kuuliza tu iko ifuatwe basi ama sivyo?

**Audience:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa hiyo mambo kama nimekufahamu vizuri, kuhusu mambo ya mwanaume kumuambia mke wake sasa ninataka ununuwe hii talaka, sikupi talaka mpaka uinunue ama sivyo?

**Makka Abothole:** Ndio.

**Com. Lethome:** Sasa sheria ya Kiislamu imesema hivi, Mwenyezi Mungu ametupa ndoa na akasema kuna sababu za ndoa malengo ya ndoa, kupatikane mapenzi ndani yake na rahma na watu kuweza kuishi pamoja. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu alivyoweka lakini wakati mwingine Mwenyezi Mungu huyu huyu aliyetuumba anajuwa kuna wakati hutokea ndoa inakosa kufaulu,watu inakuwa hawasikizani nyumbani, hakuna kuhurumiana hakuna mapenzi. Inakuwa ni jahannam ile nyumba, sheria haikumdhulumu mwanamke kuna watu wengine wanafikiria mwanamke hata ndoa ikiwa mbaya vipi hawezi kujitowa lakini sheria ya Kiislamu haikumdhulumu mwanamke wala mwanaume, imewapa wote wawili haki, yule ambaye anaona hii ndoa imemkera zaidi hawezi kuvumilia tena ana haki ya kusema mimi sitaki hii ndoa. Kumewekwa taratibu, taratibu ya kwanza ni ile ya talaka. Talaka ni mwanaume mwenyewe anampa mkewe talaka, nimekupa talaka sasa. Anapopewa talaka mwanamke kuna utaratibu wake wakati mwingine wazee wengine huwa hawajui wa Kiislamu anafikiri tu unaweza kuamka saa sita usiku unamwambia talaka toka kwenye nyumba yangu. Ana haki yule mwanamke anapopewa talaka kama ulikuwa haujampa mahari

yake lazima umpe mahari yake saa hiyo hiyo, kuna mambo mengine anaweza kudai kama ana mali yake pale ndani ya nyumba ulikuwa umempa ni yake, hiyo ni yake lazima achukuwe.

Kama alikuwa amefanya kazi akanunua kitu fulani ama umemuandikishia kitu fulani ni chake anakwenda nacho. Na usimtoe katika nyumba ya ndoa kabla ya *eda* yake kuisha, miezi mitatu au haithi tatu, hawezi kutoka pale. Huu ni utaratibu wa kwanza, utaratibu wa pili kuna kitu kinaita *hulaq*. *Hulaq* ni pale mwanamke ndiyo anataka anasema mimi sitaki maya nimetosheka sasa na mzee huyu, sasa hapo mzee hataki. Suna ya Mtume (S.A.W.) ni mwanamke mmoja aliendа kwa Mtume akasema, huyu fulani mimi simtaki, hakutoa sababu yeyote alisema tu mimi simtaki huyu. Akaulizwa je utamrudishia mahari yake aliyekupa? Alikuwa amepewa mahari ya bustani, akamuuliza '*Atturduna Illaihi hathiqatahu?* Utamrudishia bustani yake? Akasema ndio. Kwa hivyo hapa sunna ni kuwa mwanamke pia hawezi kujifunga na ile ndoa anadhulumika lakini anajifunga tu, ana haki ya kutoa.

Kama yule mume alikuwa amekupa mahari sasa hapo unaweza kujitoa kwenye ndoa na ukamrudishia mahari yake. Na kama alikuwa hajakupa basi inapotelea hapo, unasema yale mahari ulikuwa hujanipa ndiyo hivyo, lakini isiwe ni sababu ya mwanaume unamdhulumu mwanamke halafu unamuambia nirudishie mahari yangu na hana chochote la, ndoa itakuwa hakuna na yale mahari yanaweza kuwa ni deni na pia kuna wazee wengine wanafanya kusudi tu kunyanyasa ili atoke amrudishie mahari yake. Sheria hapo inaangalia ni nani mwenye kusababisha ndoa ivunjike, ni nani mwenye kudhulumu mwenzake, kwa hivyo inaangaliwa hivi.

Sijui kama nimekujibu na hiyo sheria haiko hapa hiyo ni sheria ya Mwenyezi Mungu kwa hivyo haiwezi kutolewa ama kuwekwa upya ama haiwezi kufanyiwa marekebisho yeyote hiyo ni ya Mwenyezi Mungu hiyo. Lakini haikudhulumu mwanamke wala mwanaume wote wana haki sawa, wasidhulumiwe.

**Makka Abothole**: Bado niko na swali?
**Com. Lethome**: Haya endelea.

**Makka Abothole**: Kama sikuonana na Bwana yangu miaka miwili na huyu Bwana ananitesa hata nikimuambia mimi nimekuwachia mahari hataki kuniwacha na mateso yangu hata kwa wazee nimepeleka kila kitu wanaona tu.
**Com. Lethome**: Hiyo ndoa kwanza imeshavunjika, hiyo kukuwacha miaka hiyo yote ndoa imeshakuwa imevunjika. Mtume (S.A.W.) amesema, 'hakuna mwanaume anaruhusiwa kukaa mbali na mkewe zaidi ya mieze mitatu' mpaka akaamrisha waliokuwa katika jihad akawaambia warudi kwa sababu siku moja alisikia mwanamke akilalamika akitamani kufanya maovu kwa sababu mumewe alikuwa nje. Akamuuliza mmoja katika binti zake, katika *mas'haba ulafa*, mwanamke anaweza kukaa muda gani bila kuonana na hali yake, akaambiwa zaidi sana ni miezi minne, kwa hivyo akasema akatoa amri miezi mitatu lazima watu warudi majumbani kwa wake zao. Isipokuwa tu, kama mumesikizana na yeye, amekwenda kazi mbali mumekubaliana wewe kama mke na mume. La sivyo, mwanamke ana sababu ya kusema ile ndoa imevunjika hakuna mwanamke akifanya maovu kwanza uko nje, mume ndiye anayepata madhambi sasa. Akifanya lolote huko nje mume ndiye anayepata madhambi

kwa kumuacha hivyo.

Kwa hivyo kama kuna wazee wanasikiza hiyo kesi waisikize vizuri na wafanye uadilifu wasimdhulumu mwanamke. Nafikiri tutafunga kikao sasa jamani mnajuwa tumetoka kwenye katiba sasa tumeingia sheria nyingine.

**Interjection:** (inaudible) Ametoka tu nyumbani bila kisababu.
**Com. Lethome**: Sasa kama ametoka bila sababu mrudishe mke wako nyumbani kama kweli una haja naye. Swali la mwisho la Abubakar halafu tufunge kikao tafadhalini, Abubakar?

**Abubakar Diman:** Langu ni maoni ningetaka kusema kwamba Provincial Administration isitolewe kwa sababu tumeona kwamba hivi kwenye uchaguzi zilizotangulia wananchi walikuwa wanapiga kura tatu kwa wakati moja na kwa wale ambao hawajasoma kama sehemu hii yetu, inakuwa ni vigumu sana watu kuchaguwa ma Councillor, kuwachuwa Wabunge na kuchaguwa Rais wakati ule ule. Kuwa hawawezi kujimudu kuweza kuamua kati ya hawa watu, sasa tukiongeza District Administrators, Locational Council, itakuwa ni kura tano ambayo wanajaribu kupiga. Kwa hivyo, mimi kwa maoni yangu ningeonelea kwamba, ikiletwe habari ya kwamba hawa Provincial Administration wakitolewa itakuwa tunaongeza ile taabu ya kutokuwa na kazi katika nchi kwa hivyo Provincial Administration ipewe vipengele vingine ambayo itaifanya wasiwe na hii power ambayo wako nazo saa hii lakini isitolewe asanteni.

**Com. Lethome**: Asante Abubakar sasa nafikiri tutafunga kikao, sasa ningependa kumrudishia microphone mwenyekiti wa 3Cs committee ambaye anamuakilisha District Co-ordinator aweze kutufungia kikao ili tuweze kuondoka. Tungependa kuwacha nakala hizi za documents ambazo zimeandikwa kwa Braille huenda kukatokea mtu ambaye ni kipofu anahitaji kusoma anaweza kutumia hiyo.

Tunawashukuru kwa subira yenu tangu asubuhi mpaka sasa, hiki kikao kimenifurahisha kuliko vikao vyote ambavyo nimewahi kuhudhuria. Kimekuwa very lively, kina uhai. (end of tape 4 side A).

**Mohammed Wario:** Ninaweza kusema ya kwamba hakuna Commissioners ambao wamekuja hapa na wakakaa muda mrefu na kuvumilia na kuongea kama vile Ibrahim alivyoongea mtakubaliana na mimi?
**Audience**: Ndio.

**Mohammed Wario:** Vile alivyoongea hata mimi ninamuhurumia kwa sababu yuko peke yake wale wengine walikuwa wanakuja wawili watatu, leo ameongea kutoka asubuhi mpaka jioni. Sijui kama anaweza kuenda kufanya kazi kwingine pengine programme officer wake ampeleke kwa garage akasafishwe koo kwa sababu ameongea sana ninamsikitikia lakini tunakushukuru. Na pia kulingana na maoni vile ilikuwa imetolewa mimi mwenyewe juzi wakati tulikuwa tumeona maoni ya Bura Constituency Bwana Commissioner nilishangaa sana hata kuna hawa CBOs ambazo zilikuwa zimejaribu kutusaidia na civic

education, walipokosa majina yao kwa ile karatasi ya maoni walisikia mbaya, tunaona imeandikwa ya Wajir ndiyo hata tukasema Commission iombee msamaha hata kupitia Radio kwa nini walifanya hivyo ndiyo ukasikia Bwana Ali alikuwa analalamika anasema hata hiyo maoni pengine ni za Wajir hata sio za Bura Constituency. Na ana haki ya kusema hivyo kwa sababu mambo mengi ambayo yalikuwa yamepatikana hapo ndani yalikuwa ni ya sehemu zingine kwa hivyo, nafikiri ukirudi huko pia mtafanya marekebisho na tuletewe copies za kutosha katika constituency hii ya Bura.

Na pia nafikiri wananchi leo wamepata katiba mpya ambayo mumeandika hatuwezi kuita mpya kwa sababu mpaka saa hii pia iko na njia nyingine mbili za kupitia kabla haijakuwa katiba. Lakini katiba ambayo imeshaandikwa wameisoma, wameipitia na wewe umewafafanulia nafikiri pia wataendelea kusoma na baada ya National Conference nafikiri haitapingwa na watu wengi na tunatarajia ya kwamba itatuongoza.

**Hasssam S. Mohammed**: Nataka kusema tu ya kwamba tuko na report aina mbili, tuko na hii ambayo tumewapatia, profile hiyo hapo juu tutarekebisha according to the way the situation is kwa sababu lazima irekebishwe lakini kuna report ya aina mbili. Kuna ile tunaita verbatim report, wakati mlikuwa mnapeana views yenu, kuna tape recorder ilikuwa ina record na mlikuwa mnazungumzia mnapeana majina yenu, kwa hivyo hiyo ni report tofauti inaitwa verbatim report hiyo inatayarishwa na hiyo inaonyesha kila mtu, kama ni wewe ulisema kama ni huyu alisema nini. Hii ambaye iko hapa ni ile ilikuwa inaandikwa na mkono na assistant programme officer kwa hivyo hawakuwa wanaandika majina, walikuwa wanaandika tu generally maoni ya aina gani kuhusu issues za constitution. Kwa hivyo wakati hizo verbatim reports zitakuwa tayari labda zitatumwa kwa constituency ama kama hazitatumwa kwa constituencies, zitakuwa record kamili, mtu yeyote anataka kuenda kuangalia anaweza kuenda kuangalia.

**Mohammed Wario**: Okay, asante sana kwa sababu mnaenda njia ndefu tutawachokesha tunawashukuru vile nilivyosema mumefanya kazi kubwa tungewapigia makofi lakini makofi siku hizi haitoshi lakini tunawaombea Mungu mfike salama salimin. Hiyo ndiyo ninafikiri maombi bora zaidi kuliko kuwapigia makofi kwa hayo machache nafikiri tutapata mzee mmoja au Sheikh mmoja aombe ili Commissioner na wasaidizi wake nafikiri swali tumemaliza Bwana Mburu? Nafikiri kuna watu wamechaguliwa kama sijakosea kutoka kila district watu watatu.

**Com. Lethome**: Asubuhi nilisema na ukiangalia gazetti ya jana utaona inakusanya Wabunge wote mia mbili ishirini na wanne. Commissioners wote ishirini na tisa, kila district ina watu watatu imewatuma huko, each registered political party ina mtu mmoja, professional bodies, the civil society, religious organizations. Wote jumla ya watu mia sita ishirini na tisa, tayari ukiangalia gazetti ya jana utaona majina yao yamekuwa gazetted sasa, hao ndiyo wawakilishi katika conference yenu.

**Mohamed Wario**: Sheikh mmoja tafadhali atuombe ili waweze kuondoka wageni wetu haraka, Sheikh Adam Ibrahim Aralle?

**Sheikh Adam Ibrahim Aralle**: *Bismillahi Rahman Rahim. Allahuma Rabana atina fi dunya hasanatan wa fil akhirata*

*hasanata wakina adhama nar, Rabana la tuzuq kulubana baatheytana wahablana min ladunka rahmatan inanka anta wahab, subhana rabika rabi izatina ama yusifuna wasalamu alal mursalin, wal hamdhullillahi rabil alamin, salalahu ala sayidina Muhammad waala alihi was'ahabihi wasalim. AMIN.*

The meeting ended at 4:35PM.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**